BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 29 Aprili, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-

Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALISILI NA UTALII):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Maliasili na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Maswali leo tunaanza na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Lameck Okambo Airo.

Na. 110

Uhamishaji wa Kituo cha Uhamiaji Shirati kwenda Kirongwe

MHE. LAMECK O. AIRO aliuliza:-

Wilaya ya Rorya ina vituo viwili vya mipaka ya Tanzania na Kenya ambavyo ni Shirati na Kogaja, lakini Serikali ya Kenya tayari imeishajenga kituo cha *Mihuru Bay* na kukamilika.

(a) Je, Serikali itahamishia kituo cha Shirati Kirongwe sehemu waliyojenga Serikali ya Kenya?

(b) Je, ni lini Serikali itawafidia wananchi wa Kirongwe ambao wametoa maeneo yao kwa ajili ya kituo hicho kuhamishiwa hapo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la kuhamisha kituo cha Uhamiaji cha Shirati kwenda Kirongwe limewekwa katika Mpango wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2013/2014 ambapo Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi katika kituo cha Kirongwe. Ujenzi huu unafuatia kutengwa kwa eneo la kutosha kwa madhumuni ya kujenga ofisi za taasisi zote zinazotoa huduma mpakani.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo la Kirongwe lipo chini ya Serikali ya Kijiji ambayo imelitoa kwa madhumuni ya matumizi ya kujenga ofisi za taasisi zinazotoa huduma mipakani, utaratibu wa kufidia wananchi waliotoa maeneo yao utafanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu za ulipaji fidia baada ya maeneo husika kufanyiwa uthaminishaji. *(Makofi)*

MHE. LAMECK O. AIRO: Mheshimiwa Spika, Rorya ni wilaya ambayo imekamilika; ina *DC,* Usalama wa Taifa Wilaya, Mshauri wa Mgambo wa Wilaya, TAKUKURU na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji mpaka sasa hawajahamia katika eneo lao la wilaya na tayari *DC* amewahi kutoa nafasi ili Afisa Uhaniaji wa Wilaya aweze kuhamia pale kwenye ofisi yake, lakini mpaka sasa Afisa Uhamiaji hajahamia pale.

Kinachotokea ni Wanarorya kufuata huduma hiyo Musoma na Tarime wakati Afisa Uhamiaji wa Wllaya ameishateuliwa, yuko Wilayani. Naomba majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nizingatie kwa makini sana tatizo ambalo ameliongelea. Lakini pia tunazingatia na kulifuatilia kwa ukaribu. Naomba nimhakikishie kwamba tutachukua hatua haraka inavyowezekana kuliondoa tatizo hilo. *(Makofi)*

Matatizo ya Kiulinzi Yanayoikabili Mipaka Yetu

MHE. FAKI HAJI MAKAME aliuliza:-

Mipaka ya nchi ni eneo muhimu sana ambalo lina jukumu la Ulinzi na Usalama kisiasa na kwa afya ya raia na nchi husika. Katika kutekeleza majukumu hayo walinzi na viongozi wao wamekuwa wakipata shida na matatizo makubwa ya kudhibiti mipaka yetu hasa katika mpaka wa Tanzania na Zambia.

Je, ni lini Serikali itamaliza matatizo yanayowakabili walinzi wetu hususan pale Tunduma katika ulinzi wa afya ya Watanzania?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mbunge wa Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge ni kweli mazingira ya eneo la Tunduma yanazifanya shughuli za ulinzi mpakani kuwa ngumu. Serikali imekuwa ikilitafakari suala la kuzibomoa nyumba zilizojengwa kiholela kwenye eneo la mpaka.

Hata hivyo, uamuzi huu una gharama kubwa sana. Kwa msingi huo Serikali imeviagiza Vyombo vya Ulinzi na Usalama viimarishe shughuli za ulinzi na ukaguzi wa eneo la Tunduma ili kudumisha usalama wa nchi yetu wakati ikiendelea kulitafutia suala hili ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahalifu wanaweza kujifanya wafanyabiashara wakati wanapotaka kutimiza dhamira zao, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji hushirikiana ili kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama katika maeneo ya mipakani unalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali italipatia ufumbuzi tatizo la walinzi wetu pale Tunduma hali ya fedha itakapoimarika ili waweze kutimiza wajibu wao kwa Taifa. *(Makofi)*

MHE. FAKI HAJI MAKAME: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu hayo mazuri katika fani ya uandishi na usimulizi, naomba nimWulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa, Waziri ametueleza kuwa JKT, Polisi na Uhamiaji wanashirikiana katika kusaidia ulinzi wa lile eneo, na Kamati ya Huduma za Jamii kipindi kilichomalizika tulipotembelea eneo lile tulioneshwa mpaka zile njia za panya ambazo zinategewa kutumika kupitisha vitu kama dawa feki na biashara nyingine haramu. Mbona wale wafanyakazi pale hawakutuonesha ule ushirikiano wenyewe kwamba hapa katika uchochoro huu, njia za panya hizi, kuna huyu mlinzi wa usalama, huyu ni mlinzi labda wa JKT? Hilo ndiyo swali langu, hatukuwaona.

(ii) Kwa kuwa, *TFDA* wanajitahidi sana kukamata dawa kadhaa feki, vipodozi visivyofaa na dawa tiba ambazo hazifai zinazoingia nchini hukamatwa.

Je, Serikali inaisaidiaje *TFDA* kuweza kuwa na nguvu ya kuimarisha ulinzi zaidi kwa ajili ya usalama wa raia? *(Makofi)*

SPIKA: Haya, swali la kwanza Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu. lakini hilo la pili sijui ni nani tena? Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Faki Haji Makame, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Ushirikiano upo, si rahisi sana kama alivyoambiwa na wafanyakazi kwamba lazima wamwambie kuna ushirikiano wa kiwango hiki. Kwa kadiri ninavyoelewa ushirikiano upo. Suala la kwamba zipo njia za uchochoro, nadhani ipo mipaka ya majukumu hapa kwa sababu yapo majukumu ya ulinzi wa mipaka na hili ni jukumu la Jeshi la Wananchi wa Tanzania na siyo kama alivyosema yeye JKT, Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ).

Lakini ziko shughuli hasa katika maeneo hayo ya kwenye vichochoro ambazo zinatekelezwa na Jeshi la Polisi. Lakini kwa kuwa Serikali ni moja, tumesikia jambo hili, tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Polisi ili tuweze kutekeleza wajibu wetu wa kulinda usalama na ulinzi wa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Swali la pili Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba *TFDA* wanafanya kazi nzuri kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tatizo lao ni uhaba wa wafanyakazi na vitendea kazi. Kwa mfano zile zinazoitwa min-*lab,* maabara ndogo sehemu za mipaka. Kama mlivyosikia ni kwamba tunatarajia sasa kupata vibali vya ajira. Tutawaongezea wafanyakazi *TFDA* pamoja na hizo min-lab ili waweze kutoa huduma hiyo kwa uhakika zaidi. Tatizo lao lilikuwa ni uhaba tu wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Kambi ya JKT Bulombora kule mkoani Kigoma imekuwa katika mazingira magumu sana hasa kwa kukosa nishati ya umeme ya uhakika. Kwa vile kambi hiyo imekuwa ikisaidia suala zima la ulinzi hasa katika mpaka wetu na nchi yetu na Kongo?

Je Serikali ina mpango gani hasa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, kusaidia kambi ya Bulombora eneo lile kuwa na umeme wa uhakika ili hali ya ulinzi wa maeneo yale yaweze kuimarika? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri si unaijua hiyo Kambi? Huyu alikuwa Tunduma.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Ni kweli kwa muda mrefu Kambi ya JKT Bulombora imekuwa na tatizo la umeme. Wizara yangu inalijua tatizo hilo, tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kulifanyia kazi na kulitafutia ufumbuzi. Tatizo linalotukabili sasa hivi ni upungufu wa fedha na kambi ambazo bado hazina nishati ya umeme ni nyingi. Lakini tutajitahidi kufanya hivyo kwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu ili katika kipindi kifupi kijacho kambi hii ya Bulombora nayo iweze kupata umeme wa uhakika ili hatimaye waweze kutekeleza jukumu lao la ulinzi katika eneo hilo. *(Makofi)*

SPIKA: Swali hili lakini lilikuwa jingine kabisa. Mheshimiwa Mama Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niongeze swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Swali la msingi la Mheshimiwa Faki lilihusiana na usalama wa afya na kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba niulize.

Je, tatizo la pale mpakani kuhusu afya ni idadi ya wafanyakazi tu na si vitendea kazi hasa magari kutokana na urefu wa mpaka ili waweze kudhibiti dawa na vipodozi visivyo halali vinavyoingizwa nchini? *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali hili, tatizo letu ni uhaba wa wafanyakazi pamoja na vitendea kazi. Lakini siyo rahisi kuweka hizo zinazoitwa *min-lab* mpaka mzima, ni lazima ziwe sehemu maalum. Tunachotegemea ni kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vitalinda hiyo mipaka ili kufanya watu wote wapite katika sehemu rasmi ambazo ndipo tutakapokuwa tuna wataalam wanaoshughulikia masuala ya afya.

Kwa hiyo, anachosema Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ni kwamba kwa kushirikiana kati ya vyombo vya ulinzi na usalama na vile vyombo ambavyo vinatoa huduma za afya wakiwamo mabwana afya katika maeneo yale pamoja na watu wa *TFDA*. Ni vyema tukahakikisha mipaka hiyo inalindwa na vyombo vya ulinzi na usalama ili watu wote wapite katika mipaka rasmi na bidhaa zao ziweze kukaguliwa.

SPIKA: Ahsante sana. Naomba tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu, atauliza swali linalohusika.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na kuipongeza Yanga kwa Ubingwa naomba sasa swali langu Na. 112 lipatiwe majibu. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa kuchomekea tu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

Na. 112

Agizo la Mheshimiwa Rais la kuwafungia Umeme Wananchi wa Somanga

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU aliuliza:-

Eneo la Somanga ndipo mitambo ya kuzalisha umeme ilipo; na kwamba pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais kuwa wananchi wa eno hilo wafungiwe umeme bado hawajafungiwa:-

(a) Je, kwanini agizo hilo la Mheshimiwa Rais halijatekelezwa?

(b) Je, kwanini maeneo ya Banduka, Mtandago, Miteja, Sinza, Puyu, Matandu na Njenga hayapati umeme licha ya umeme kupitia kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (**MHE. GEORGE B. CHAWENE**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais imekwishaanza kutekelezwa, ambapo tayari baadhi ya maeneo ya Somanga Fungu yana Umeme na wateja 200 wameunganishwa. Kwa sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi mdogo ambapo tunatarajia kuwaunganisha wateja wengine 50. Katika mradi huu, nguzo 60 zimetengwa na tayari 40 zimekwishasimamishwa.

Aidha, wananchi wa eneo la Somanga Fungu wanashauriwa kuanza kupeleka maombi ya kuwekewa umeme *TANESCO* Kilwa Masoko.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme maeneo ya Banduka, Mtandago, Miteja, Sinza, Puyu, Matandu na Njenga zimejumuishwa katika mpango kabambe wa Umeme Vijijini awamu ya pili chini ya uwezeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).* Zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Julai Machi, 2013. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kazi za kufikisha umeme kwenye vijiji tajwa hapo juu zinajumuisha: -

(i) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 0.4 urefu wa Km. 15.5;

(ii) Ufungaji wa *transoforma* saba (7) zote za kVA 50; na

(iii) Kuwanganishia umeme wateja wapatao 225. Gharama za kazi hizi zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania milioni 290.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na majibu ya Waziri yanawiana na ukweli halisia. Ningependa kumwuliza Waziri maswali ya nyongeza yafuatayo.

(a) Wananchi wameishapeleka maombi yao pale Kilwa Masoko na wataendelea kupeleka, lakini nilitaka kujua kwamba utekelezaji wa miradi hii itaanza lini katika maeneo kama kule Mkanyageni ambako ni kitongoji, ndani ya hiyo Somanga ambayo tunazungumzia? Vilevile Mitondo ambako ni eneo hilo hilo la Somanga, nguzo zipo bado hazijatandazwa.

Lini utaratibu huu wa utekelezaji wa miradi utafanyika? Siyo wakati wowote, tunataka kujua lini?

(b) *TANESCO* ina matatizo katika suala la uzalishaji na ukusanyaji wa mapato. Nini mpango wa Serikali kuivunja au kuiboresha pamoja na kuipa mtaji mwingine ili iweze kujiendesha kwa ufanisi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (**MHE. GEORGE B. CHAWENE**): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, nikisema wakati wowote ndani ya mwaka huu ninamaanisha ni *logistics* za utekelezaji utaratibu wa kupata mkandarasi. Lakini pia *mobilization* na vitu vingine kwa sababu miradi hii ya umeme inahusisha karibu malighafi kutoka nje, ikiwa ni *transformers* na vitu mbalimbali, tuna-*deal* na *suppliers* mbalimbali kwa hiyo ndiyo maana jibu langu linakuwa hivyo.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wenye miradi ya umeme hii ambayo tumeipanga toka mwaka jana kwamba, itaanza kutekelezwa wakati wowote ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni juu ya utendaji kazi na ufanisi wa Shirika letu la ugavi wa umeme *TANESCO* kwamba lenyewe ndilo linalozalisha umeme, kusafirisha umeme na kusambaza umeme.

Hii imekuwa ni ajenda kuu Serikalini na tumekuwa tukilifikiria, lakini tumehusisha wadau mbalimbali.

Tumeweka katika Tovuti yetu ya Wizara na tumepokea maoni ya watu mbalimbali wasomi na wadau wote kwa ujumla, katika nchi nzima na tumekuwa tukifanya hivyo hata tukipata mawazo ya watu mbalimbali na hata nje ya nchi.

Nia na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaiboresha na kuifanya *TANESCO* iwe na ufanisi na uamuzi wake utatokana na maoni tuliyoyachukua na ushauri wa kitaalam juu ya namna gani *TANESCO* iwe.

Mheshimiwa Spika, tumepokea maoni mengi sana na sasa tunayapanga ili tuweze kujua nini tufanye na nini tuamue kulingana na hali ya uendeshaji wa Sekta hii ya nishati katika maisha ya kisasa ya duniani. *(Makofi)*

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mwaka jana Serikali ya Holland wasaini Mkataba na Serikali ya Tanzania kueneza umeme Wilayani Ngara, Biharamulo na Mpanda.

Je, utekelezaji wa mradi huo utaanza lini Wilayani Ngara?

SPIKA: Jamani hilo ni suala jipya lakini sijui unaweza kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni suala jipya sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna miradi ya kufunga *transformer* mpya katika Wilaya za Ngara, Biharamulo na Mpanda.

Mheshimiwa Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kampuni itakayofanya kazi ile imekwishapatikana na shughuli ile itaanza kutekelezwa wakati wowote. Kampuni inaitwa Holiyon na shughuli zile nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati wowote kuanzia sasa mnajua tukishaingia kwenye mikataba hii ya utendaji wa kazi ni vigumu sana kusema sasa wamefikia wapi ili mradi *deadline* ile tuliyokubaliana kwenye mikataba haijapita basi sisi tunabakia kuamini kwamba atatekeleza kwa wakati, lakini Mkandarasi amepatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatoe wasiwasi wananchi wa Ngara, Biharamulo na Mpanda kwamba *transformer* zile zitafungwa mpya na watapata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

MHE. SUSAN A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Wilaya ya Kilombero ina tatizo kubwa sana la kuwekewa umeme hasa katika Tarafa ya Mgeta kwenye uzalishajli mkubwa wa kilimo cha mpunga yenye Kata tano na Kata nyingine.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleke huduma ya umeme katika Tarafa hiyo ya Mgeta yenye Kata tano na vijiji vingine ambavyo ndani ya Wilaya ya Kilombero havina umeme?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge unaamini kabisa hilo ni suala kabisa kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, pengine Mheshimiwa Susan Kiwanga alitaka watu wa Kilombero wamsikie, lakini tunazo progamu mbalimbali ambazo Mheshimiwa Mbunge anazifahamu pengine tuwasiliane aweze kujua ni wapi na kuna mradi gani katika maeneo haya aliyoyataja.

Tunazo programu mbalimbali, *TANESCO* wanasambaza umeme na tuna miradi inayosambazwa na *REA* na yote karibu nchi nzima tumeweka basi Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili aweze kujua programu gani itafanyika kupeleke umeme Kilombero.

SPIKA: Ahsante sana. Kazi kwako uwasiliane na Naibu Waziri huko.

Na. 113

Ujenzi wa Barabara ya Mbande – Kongwa Mpwapwa

MHE. FELISTER A. BURA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mbande – Kongwa - Mpwawa, kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande – Kongwa - Mpwapwa- Gulwe Kibakwe , yenye urefu wa Kilometa 106.52 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kwa sasa inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Usanifu huu unafanywa na Mhandisi Mshauri aitwaye *Inter consult Ltd* kwa gharama ya shilingi milioni 499.9.

Kazi hii ilianza mwezi Oktoba, mwaka 2012 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2013. Mara baada ya kukamilika kwa usanifu huu, na makisio ya gharama za ujenzi wa barabara kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajilil ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami. *(Makofi)*

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, barabara hii ahadi ya Rais, narudia tena. Kwa kuwa barabara hii ni ahadi ya Rais na kwa kuwa Barabara hii ina umuhimu wake kwa sababu pale Godegode kuna madini mengi ya *copper*, kuna rubi na bado kuna *gypsum* Godegode.

Kwa hiyo, barabara hii ina umuhimu wake Kitaifa na kwa kuwa ni ahadi ya Rais naomba kujua kama Serikali ipo tayari kuanza ujenzi wa barabara hii kwa mwaka ujao wa fedha? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimhakikishie kwa sababu kama anavyojua barabara hii ipo kwenye Ilani na ni ahadi ya Rais ya barabara muhimu na ndiyo maana tumeanza kufanya usanifu.

Kujenga barabara huwezi kuanza kabla hujafanya usanifu, ukishakamilisha usanifu ndiyo unaweza kuanza kujenga. Kwa hiyo, naomba niwape matumaini wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, siwezi kusema itaanza mwaka unaokuja wa fedha kwa sababu kazi bado haijakamilika ya usanifu.

Tunatarajia Mkandarasi Mshauri amalize Mwezi Juni, hivyo ndivyo Mkataba ulivyo, lakini inaweza ikafika mwezi Julai, inategemea na mazingira ya kazi yenyewe. Kwa hiyo, watakapomaliza Serikali inakuahidi kwamba itatafuta fedha na tutaanza kujenga kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Barabara haifanani na nyingine yoyote. Mheshimiwa Laizer.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, barabara ya Kamwanga Sanya Juu imefanyia usanifu na kila Bajeti inapangiwa fedha. Je, katika kipindi hiki fedha zilizopangiwa zitaanza kazi au zitapelekwa katika maeneo mengine kama Bajeti zilizopita?

SPIKA: Utakumbuka hata hicho kijiji alichokisema. Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ni fundi tu labda. Kama mtauliza maswali yasiyo yenyewe siwape nafasi ya kujibiwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kama fedha ziliishawekwa kwa mwaka huu wa fedha 2012 kwa ajili ya kazi ya usanifu hiyo kazi itatekelezwa kama ilivyopangwa. Barabara hizi nyingi ambazo tunazifanyia usanifu ni nyingi. Kwa mfano, mpaka sasa kilomita 11,174 zinaendelea kujengwa ndani ya nchi hii.

Kwa hiyo, kuna barabara zingine zinajengwa kwa kiwango cha lami na nyingine zinafanyiwa usanifu. Tutakapomaliza kazi ya usanifu zote tutaziweka kwenye kundi moja tunazitafutia fedha tunaanza kujenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

SPIKA: Haiwezi kufafana na mahali popote, tunaenda Wizara ya Elimu.

Na. 114

Mkataba wa Ajira kwa Nchi za Afrika Mashariki

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Nchi za Afrika Mashariki zimekubaliana kuridhia Mkataba wa pamoja wa ajira kwa wananchi wake hasa vijana.

Je, Tanzania ina mkakati gani wa makusudi wa kuwaandaa vijana wake kielimu ili waweze kushindana katika soko la ajira la Jumuiya ya Afrika Mashariki?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kilichoridhiwa ni Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na siyo Mkataba wa Ajira wa Nchi za Afrika Mashariki.

Ndani ya Itafiki hii, sehemu "D" kipengele cha 10 sehemu ya 8 kinahusu uhuru wa kufanya kazi nchi nyingine kwa mujibu wa Sheria, Taratibu za Mikataba na kiutawala kwa kila nchi husika.

Hivyo, inapaswa kuzingatiwa kuwa uhuru wa Ajira kwenye Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki unahusu Sekta binafsi na siyo ajira kwenye sekta ya umma, isipokuwa kama sheria za nchi husika zinaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika ngazi zote za elimu kwa nia ya kuwaandaa vijana wetu waweze kushindana katika soko la Ajira la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pamoja na utekelezaji wa mipango ya MMEM na MMES, Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) 2010 – 2015 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi (MMEU – 2013/2014 -2017/2018) ambapo mipango hii kwa pamoja inalenga kuvijengea uwezo Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi ili viweze kuzalisha wataalam wengi ambao watakuwa na uwezo wa kitaaluma na kitaalam kwa kuingia kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatekeleza Mpango wa Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu unaogharamiwa na Benki ya Dunia (2009-2013) wenye lengo la kuvijengea uwezo Vyuo Vikuu vyote vya Umma katika maeneo ya Rasilimali watu na Miundombinu ili viweze kuzalisha wataalam wa Sayansi na Teknolojia wenye uwezo wa kuingia kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Vilevile, Serikali imeanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Mbeya *University of Science and Technology* pamoja na kuimarisha Taasisi za Sayansi na Teknolojia za Dar es Salaam na Arusha. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, katika jibu la msingi Serikali imeonyesha mkakati mkubwa wa kuwaandaa wataalam wake hasa katika Vyuo Vikuu kwenye eneo la Sayansi kuliko fani zingine.

Je, Serikali inawaambia nini Watanzania kwamba ni kwa kiwango gani imewaandaa vijana wake katika fani za Uhasibu, uchumi, utalii na nyinginezo ili waweze kushindana na wenzao ukizingatia ukweli kwamba Bodi ya Mikopo haitoi mikopo kwa wanafunzi waliochukua fani hizo?

Swali la pili, Serikali inaweza kuwaambia vijana wa Kitanzania ni maeneo gani ambayo imehifadhi ajira hizi katika sekta binafasi hasa ukizingatia ukweli kwamba katika sekta ya Utalii hususan kwenye mahoteli makubwa ya Kitalii ni Wakenya tu ndiyo wamejaa wakifanya kazi hizo? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge anauliza kwamba Serikali imejikita sana kufundisha programu za Sayansi na Teknolojia katika Vyuo Vikuu. Suala hili ni kweli kabisa kutokana na ulimwengu wenyewe jinsi unavyoenda kwa sasa hivi. Wote hapa hata Waheshimiwa Wabunge tunakubaliana kabisa kwamba tunahimiza kusoma masomo ya Sayansi ili tuweze kukimbizana na hali ya dunia inavyoenda.

Lakini siyo kwamba tumeacha hizi programu zingine. Kwa sababu Vyuo Vikuu wanajiandalia *Curriculum* wenyewe kwa hiyo, vyuo vingi tunavyo Vyuo Vikuu vya Uhasibu hata hapa Tanzania vinavyotoa programu hizo.

Lakini vilevile tunatoa programu za Kiuchumi, tunatoa programu za Kitalii kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amejaribu kuvi-*mention*. Lakini sasa sana sana niendelee kusisitiza kwamba bado tunatoa Sayansi na Teknolojia ndiyo kitu kikubwa sana kinachoendana pamoja na nchi nyingine hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaandaa sera mpya ya elimu ambapo tarehe 19 Mei, 2013 tutakuja tuwapitishe kwenye rasimu mpya ya Sera. Kwa hiyo mambo yote mtakuja kuyaona humo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba vijana wengi na hasa Sekta ya Utalii kwenye mahoteli makubwa wanaajiriwa kutoka Kenya tu na siyo Tanzania. Linaweza kuwa na ukweli au lisiwe na ukweli.

Lakini ni kwamba kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi kwa sekta binafsi tumeridhia Itifaki kwamba Wakenya wanaweza kufanya biashara Tanzania, Watanzania wanaweza wakafanya biashara Kenya, kwa Waganda wanaweza wakafanya biashara Rwanda, Warwanda wanaweza wakaenda Burundi.

Kwa hiyo, siyo ajabu sana kuwaona Wakenya wanakuja kufanya kazi Tanzania na hasa katika sekta binafsi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, umoja wetu wa Afrika Mashariki tunashikiriana kwa mambo mbalimbali isipokuwa ajira za vijana kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye majibu yake. Kwa kuwa, vijana wetu wengi wamesoma na ajira nchini bado ni chache.

Je, Serikali haiwezi kuliweka hili mezani katika Umoja wetu wa Afrika Mashariki ili waweze kulijadili kuona namna ya vijana wetu watapata ajira Afrika Mashariki kwa ujumla?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika,alichokiongea Mheshimiwa Diana Chilolo hapa ni kweli kabisa na katika vikao vyetu vya *East Africa Community* vinaendelea kujadiliana na linaendelea kufanyiwa kazi. Lakini naomba vilevile tuchukue ushauri kwamba labda tulifanyie kazi kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Na. 115

Madai ya Fidia kwa Kampuni ya Kamwene Woodworks

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. JOYCE J. MUKYA) aliuliza:-

Kuwekuwepo na madai ya muda mrefu kwa Kampuni ya Kamwene *Woodworks* kwa Wizara ya Maliasili na Utalii tangu mwaka 1979 juu ya fidia ya hasara iliyosababishwa na Serikali, madai ambayo pamoja na Mamlaka za Serikali na Tume zilizoundwa kuafiki uhalali wa malipo hayo, bado wahusika wameendelea kuzungushwa:-

Je, ni lini Serikali italipa madai ya Kampuni ya Kamwene *Woodworks*?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya Kamwene *Woodworks* ina nia ya kuishtaki Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii wakidai jumla ya shilingi 556,510,000/= kama fidia ya magogo na mbao vilivyotaifishwa na *TANAPA* mwaka 1979 huko Morogoro baada ya kukamatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, suala hili kwa upande wa Wizara lilishamalizika tangu mwaka 2000 baada ya madai yao kufungwa na Kampuni hiyo kulipwa fidia ya jumla ya shilingi 5,468,280/=.

Hivyo, ushauri uliotolewa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kampuni kulipwa "*simple interest*" pamoja na fidia ya magogo 65 na mbao vipande 4,100 ulitolewa bila kupata maoni na mapendekezo ya Wizara.

Hata hivyo, Wizara ilishatoa msimamo kuwa madai yao hayana msingi na hawastahili kulipwa fidia yoyote zaidi ya malipo ambayo wamekwishalipwa.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) kikisomwa kwa pamoja na sehemu ya kwanza ya jedwali ya sheria ya Ukomo wa Muda (*The Law of Limitation Act*) Sura ya 89 *R.E. 2002* vinatoa mwongozo juu ya ufunguzi wa mashauri baada ya ukomo wa muda kupitia ambao ni miaka 3 tangu tarehe ya maamuzi kutolewa yawe *dismissed*.

Hivyo kwa vile maamuzi ya kulipwa kampuni husika yalishafanyika, walipaswa kutoa malalamiko yao ya kutoridhika na fidia hiyo na kuonyesha nia yao ya kuishtaki Serikali ndani ya kipindi cha miaka mitatu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuilipa kampuni ya Kamwene *Woodworks* kwa vile kampuni hiyo haikufungua kesi ndani ya muda uliopo kisheria.

Hii ina maana waliridhika na msimamo wa Serikali baada ya kulipwa kwa kiasi kilichotajwa hapo juu. Kwa sasa kampuni inachojaribu kufanya ni kuleta usumbufu ambao hauna tija yoyote kwani suala hilo lilishamalizwa na Wizara. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Naibu Waziri amesema kwamba walipata ushauri kutoka kwa Mwanasheria na kisha mnasema Mwanasheria hakupata maoni na mapendekezo kutoka Wizarani. Mwanasheria alijuaje kama kuna tatizo la Kamwene *Woodworks* kama hamkupelekea mapendekezo mliyokuwa nayo?

Swali la pili, kwa kuwa, kipaumbele cha Serikali yoyote ni maslahi ya watu wake, utu wa watu wao.

Je, Wizara haijaribu kutumia udhaifu wa wananchi wao ambao hawajui sheria kukwepa mwanya wa kuwalipa madai ambayo Kamwene *Woodworks* inadai?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, moja, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu, Sura Na. 323 ya Mwaka 2002, maeneo yote ambayo yamehifadhiwa ikiwa ni pamoja na Hifadhi zote za Taifa na Misitu ya Lindimaji inajulikana kama *Catchment Area* kwa Kiingereza na hifadhi asilia (*Natural Reserve)* na ningeweza kutaja mojawapo kama Amani, Uluguru, Kilombero na kadhalika; maeneo haya ni marufuku mtu yeyote kukata mti ndani ya maeneo ya hifadhi. Kimsingi, Serikali inapenda kusisitiza *Kamwene Woodland* walilipwa kimakosa na ingekuwa sasa hivi bado tusingewalipa na tunarudia mtu yeyote atakayekamatwa anakata miti katika Hifadhi zetu za Taifa, hata leo tukimkamata tutamfungulia mashtaka na tutamfunga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali inajali sana watu wake na ingependa matumizi ya rasilimali hizi tulizonazo ziwe rasilimali endelevu. Nchi yetu miti inapotea, jangwa linaingia kwa kasi na hii ni kutokana na watu ambao wanavunja sheria makusudi, wanafanya wanavyofanya na wanarejea kwa Serikali iwalipe, hatuko tayari tena kufanya hivyo.

Na. 116

Kuanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Mapori ya Akiba

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Serikali ilishaahidi kuanzisha Mamlaka itakayosimamia Hifadhi ya Mapori ya Akiba ya Wanyamapori badala ya Idara ya Wanyamapori:-

Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Ahadi ya Serikali ya kuanzisha Mamlaka ya Wanyamapori iko palepale na kwa sasa Rasimu za Kwanza ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka, Muundo na Majukumu ya Mamlaka na Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya 2009 zimekamilika. Hatua iliyobaki ni wadau kujadili na kutoa maoni yao kuhusu rasimu hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane wa Bunge hili, Serikali iliahidi kuwa ifikapo Desemba mwaka 2012, mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori utakuwa umekamilika. Hata hivyo, baada ya Kamati ya Uanzishwaji wa Mamlaka kupata maoni ya wadau, iligundua uwepo wa mambo muhimu yaliyohitaji kujadiliwa kwa kina. Kufuatia hatua hiyo, mpango kazi ulipitiwa upya ili kupanua wigo wa majadiliano na kushirikisha wadau wengi zaidi katika kujadili rasimu za sheria hizo. Kutokana na kupanuka kwa wigo wa wadau, kazi hii itakamilika ifikapo mwezi Novemba, 2013.

MHE. PAUL J. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ahadi hii imedumu muda mrefu toka Bunge la Tisa na si Mkutano wa Nane tu na sasa hivi tunaambiwa kwamba hii Kamati ya Uanzishwaji wa Mamlaka pamoja na wadau wanajadili mambo muhimu. Je, Naibu Waziri anaweza kutueleza mambo hayo muhimu ni nini kiasi cha kuchelewesha mambo hayo kwa muda mrefu kiasi hicho?

(i) Kutokana na ucheleweshaji wa kuanzisha Mamlaka hizo Mapori yetu ya Akiba hasa yale ya Rungwa, Kizigo na Muhesi, yanaendeshwa kwa tabu na Watumishi wa Idara ya Wanyamapori. Licha ya Serikali kupata mapato makubwa kutoka mapori hayo, lakini Watumishi wa Mapori haya wanashindwa kupata stahiki zao kama vile posho, hawana nyenzo za kufanyia kazi na mambo mengine muhimu. Je, katika kipindi hiki mpaka kufikia kuanzishwa kwa Mamlaka haya Wizara au Serikali inachukua hatua gani za

dharura kujaribu kuwakwamua hawa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu kiasi hicho?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahadi hii ya Serikali tunafurahi kusema kwamba, pamoja na muda wote ambao imechukua, sasa inakwenda kukamilika. Ilikuwa ni muhimu sana Serikali kupitia changamoto zote zilizopo katika tasnia ya uhifadhi, ilikuwa ni muhimu sana kuwashirikisha wadau wote kwa undani ili tuweze kuhakikisha kwamba, Sheria hii ambayo tutaianzisha na Mamlaka hii ambayo tutaianzisha itakuwa Mamlaka endelevu, itakayoweza kujiendesha kimfumo, kifedha na kiutekelezaji kwa majukumu ambayo kwa kweli ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kweli kwamba, tuna changamoto ya watumishi wanaofanya kazi katika mapori ya akiba nchi nzima. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ametembelea baadhi ya hayo mapori, amenituma mimi nimetembelea baadhi ya hayo mapori, tumezungumza na askari, tumeona maisha ambayo wanaishi na Serikali inachukua hatua zifuatazo za makusudi na za dharura wakati tunamalizia mchakato huu wa uanzishwaji wa Mamlaka:-

Kuanzia Julai, Wizara yangu imepata kibali cha kuajiri wafanyakazi wapya 400 katika tasnia hii ya uhifadhi na tunategemea wafanyakazi hao wote watakuwa wa wanyamapori. Kwa hiyo, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri aliwaahidi vijana pale Pasiansi na kama alivyonituma nikawaahidi pale Mweka, tunategemea kufanya kila tuwezalo ili ajira hii ipatikane, vijana hawa washiriki katika ulinzi wa maeneo yetu ya hifadhi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba turekebishe suala la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori siyo ahadi ya Serikali ni maamuzi ya Bunge ambayo yalifikiwa kwenye mjadala wa kuandikwa kwa Sheria ya Wanyamapori mwaka 2009. Kwa hiyo, Serikali inapochelewa kuanzisha Mamlaka haya maana yake ni kwamba, inachelewa kutekeleza maamuzi ya Bunge.

Sasa napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni lini Mamlaka hii itaanza kazi rasmi kwa sababu kutokuwepo kwa Mamlaka hii ya Wanyamapori kunapelekea tembo wengi sana kuuawa kwenye maeneo ambayo siyo ya hifadhi. Maeneo ambayo tembo wanakufa wengi ni ya nje ya hifadhi zinazomilikiwa na *TANAPA* na kadhalika. Kwa hiyo, naomba nijue ni lini sheria hii itakuja ili Mamlaka ianze kazi tulinde tembo wetu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ameyatoa. Kuhusu mamlaka ni kweli tunatambua kwamba hilo...

SPIKA: Inaonekana husikiki labda usogee mbele maana ni majibu yako. Sogea mbele hapa wanalalamika, ndiyo unayepaswa kujibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Kuhusu suala hili la msingi niseme kwamba, tunatambua na tunazingatia kwamba haya yalikuwa ni maamuzi ya Bunge kwamba Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania iwepo. Kwa kweli nikiri kwamba, imechelewa, lakini nataka nimhakikishie na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, azma yetu ifikapo Bunge la Novemba, tutaileta hapa ili iweze kupitishwa na baada ya hapo iweze kufanya kazi.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa *TANAPA* imeendesha semina mbalimbali hivi karibuni katika Kanda mbalimbali hapa nchini; Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati na wadau wanaozungumzwa wamejadili sana suala hili la kuanzishwa Mamlaka. Sasa ni wadau wengine gani tena wanasubiri ili jambo hili liweze kuanza?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara imeshirikisha wadau wengi. Tumezungumza na Taasisi zetu ikiwa ni pamoja na *TANAPA*

na Wananchi ambao wanayazunguka maeneo ya uhifadhi. Niseme tu kwamba, wigo wa wadau ambao ni lazima kutokana na umuhimu wa hii sheria wafikiwe ni mkubwa na tutakumbuka kwamba kuna baadhi ya mapori ya akiba ambayo yanapakana; kwa mfano, na nchi ya Msumbiji na tuna maeneo ambayo *eco-systems* zinaingiliana. Kwa mfano, *eco-systems* kati ya Tanzania na Kenya, kati ya Tanzania na Rwanda na tumeona kwa kufanya hivyo, sheria hii itakuwa yenye tija, itakuwa ina nguvu na ni matumaini yangu kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, sheria hii inakamilika mwaka huu mwezi Novemba na nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote, tushirikiane tuhakikishe tunaipitisha itakapokuja hapa Bungeni.

Na. 117

Vitambulisho vya Kupiga Kura Kutotambulika Zanzibar

MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar na Tanganyika ndiyo vinafanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

Je, kwa nini vitambulisho vya kupigia kura vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania havikutumika Zanzibar katika Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu dhahiri iliyofanya Vitambulisho vya Kupiga kura vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutotumika Zanzibar katika Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni masharti ya Kifungu cha 12A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya

343, iliyorekebishwa mwaka 2010. Kifungu hicho kinaitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutumia Daftari la Wapiga Kura lililoandaliwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, swali hili limekuwa likiulizwa mara kwa mara hapa Bungeni na hata mwuliza swali amewahi kuniuliza hata na mimi kwenye Kamati ya Katiba na Sheria na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi alikuwepo na hata kwenye vikao mbalimbali vya Kamati ya Bunge. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, suala hili naamini litaangaliwa upya mara baada ya kupitisha Katiba ambayo itakuwa imeweka utaratibu wa kuunda Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nataka nimwulize:-

(i)Je; Mheshimiwa Waziri hii huioni kama inapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani sheria mbili zinatawala suala la Muungano na ambapo Katiba ya Zanzibar peke yake haiwezi kutumika kwa masuala ya Muungano; je, hili hujaliona?

(ii)Kwa kuwa Katiba zote mbili zipo na suala hili lipo karibu vipindi vinne vya Uchaguzi. Je, Mwanasheria Mkuu alikuwepo wapi au linafanywa kwa makusudi na Serikali zote mbili kuwanyima Wazanzibari haki yao ya kuwachagua Wabunge? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa Zanzibar kwa wakati ule ilikuwa ni lazima itumike Sheria hii kwa sababu Zanzibar wana Sheria zao nyingine. Ili mtu apige kura kule, wana Vitambulisho Maalum vya Uzanzibari. Uhalali wa kupiga kura kwanza lazima uwe Mzanzibari. Sasa sisi huku watu wa Bara na Sheria hii ya Bara haiwezi ku-*define* nani Mzanzibari, Sheria ya Zanzibar ndiyo iliyo-*define* nani ni Mzanzibari.

Kwa hiyo, ukiwa katika *Territory* ya Zanzibar, utapiga kura kwa Sheria ya Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ndiyo iliyo-*define* nani Mzanzibari mwenye haki ya kufanya uchaguzi kwa chaguzi zote. Hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, naomba tena Mheshimiwa Mbunge kwamba, najua hili linawakwaza sana, mngependa sheria zote mbili zitumike lakini sheria kwa sheria kule na Katiba ya Zanzibar kule mnakoishi hairuhusu hili. Kule wanataka mpige kura zote za ndani ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria ile na mwoneshe Vitambulisho vya Uzanzibari ndiyo masharti ya msingi.

Kwa kuwa Katiba sasa tunaiandika upya, tuvute subira, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, mimi najua yote haya yameshaonekana ndiyo mambo ambayo tutaweza kuyarekebisha kwenye Katiba hiyo mpya.

Na. 118

Upigaji wa Kura Siku ya Jumapili

MHE. MCH. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kupanga kupiga kura katika Chaguzi za Kitaifa Siku za Jumapili kinasababisha Watanzania ambao ni waumini wanaoabudu siku hiyo kushindwa kupiga kura kwa sababu wanakuwa kwenye ibada jambo linalowanyima haki yao ya Kikatiba?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria za Uchaguzi pamoja na Kanuni zake, hazitaji wala haziainishi siku maalum iliyoteuliwa kwa ajili ya upigaji kura. Uamuzi wa Serikali kuteua Siku ya Jumapili ulitokana na sababu kuwa ni siku ambayo

Watanzania walio wengi hawaendi makazini na hivyo kuwa na fursa nzuri ya kushiriki katika zoezi la upigaji kura. Serikali inatambua kwamba, Siku ya Jumapili waumini wengi wa Madhehebu ya Kikristo huitumia kwenda kuabudu, lakini pia huweza kupata fursa ya kupiga kura kwa vile muda unaotengwa kwa ajili ya zoezi la upigaji kura unachukua saa chache kuanzia asubuhi inachukua kama saa tisa hadi kumi katika siku moja uchaguzi umeshakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, swali hili la Mheshimiwa Mbunge limejitokeza sana. Sisi tumeshuhudia katika mijadala mbalimbali iliyotolewa na watu mbalimbali wakiwemo waumini wa dini hizi, wametoa maoni yao katika marekebisho ya Katiba. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kutokana na maoni mbalimbali yaliyotolewa na waumini na Watanzania kwamba siku za ibada zisitumike, pengine Katiba mpya itakuja kurekebishwa au Sheria ya Tume ya Uchaguzi itakuja kurekebishwa kufuatia maoni ya Katiba mpya yatakavyoletwa na kupitiwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mshama, asubiri kwa sababu jambo hili limesemewa sana na waumini. Najua hata waumini wa Kiislam wasingependa ljumaa itumike, waumini wa Kikristo wasingependa itumike Jumapili. Kwa hiyo, tuvute subira pengine wakati wa marekebisho ya Sheria hii ya Uchaguzi ambayo itafuatiwa na mahitaji ya marekebisho ya Katiba Mpya, hili nalo litaangaliwa ili angalau tutafute siku mwafaka kwa Watanzania wote ya upigaji wa kura.

MHE. MCH. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i)Kwa kuwa kupiga kura Jumapili siyo suala la Kikatiba na ukiangalia katika Katiba yetu sidhani kama imeandikwa; bado ninaiuliza Serikali lini itafanya badiliko kusudi watu wengi waweze kushiriki kupiga kura ukizingatia kwamba katika kupiga kura watu wanakuwa na mambo mawili muhimu;

kuabudu au kupiga kura; mtu anachagua jambo moja analifanya na lingine linakosa nafasi?

(ii)Kwa kuwa nchi jirani ya Kenya ambayo juzi tu imepiga kura siku ya kawaida na ikawa *Public Holiday;* haioni ni vyema tu kutamka kabisa kwamba hiyo siku iachwe kama alivyokiri mwenyewe kwamba ni siku ambayo watu wengi wamelalamika ili watu wengi wapige kura ukizingatia wanaojiandikisha na wanaopiga kura ni vitu viwili tofauti? Naomba kuwasilisha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Wabunge wote waliosimama pamoja na Mbunge wa Tunduru, najua anataka kuuliza nini na wengine wote waliosimama, napenda kujibu maswali yao kama ifuatavyo:-

Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ...

SPIKA: Naomba mjibu Mheshimiwa Mshama tu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Ehee!!! Nimeoteshwa maswali yao.

Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Tume ya Uchaguzi inaamini Katiba hii italazimisha kuandikwa upya Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Ingawa haya mambo anayoyasema hayapo kwenye Katiba, lakini kwa makubaliano na mawazo yanayoendelea ndani ya nchi hivi sasa, jambo hili tunaamini litarekebishwa. Kwa hiyo, ni lini tutarekebisha ni pale wakati ukifika wa kuja kutunga au kurekebisha ya Tume ya Uchaguzi na jambo hili tutalirekebisha pia.

Na. 119

Viwango Vinavyostahili Kulipwa na Wawekezaji wa Zao la Katani

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kumekuwapo na utata juu ya wawekezaji wa Zao la Katani kulipa ushuru stahili kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza;-

Je, ni viwango gani stahili ambavyo wawekezaji hao wanapaswa kulipa kwa Halmashauri husika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa madaraka na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Toleo la 2002, kutoza ushuru na kodi mbalimbali kwa madhumuni ya kuziwezesha Mamlaka hizo kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za jamii kwa Wananchi walio katika maeneo yao. Kwa upande wa ushuru wa mazao, Halmashauri za Wilaya zimepewa madaraka ya kutoza ushuru wa mazao chini ya kifungu cha 7(g) cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Ushuru huu hulipwa na mnunuzi na hutozwa mahali ambapo zao linazalishwa na kwa bei ya mkulima, yaani bei ya zao kabla ya kuongezwa thamani.

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2010/2011, ambapo sasa kiwango cha kutoza shuru wa mazao shambani kilipitishwa kuwa ni kuanzia asilimia tatu hadi asilimia tano ya bei ya kuuza mazao shambani ili kuziwezesha Halmashauri kupata mapato ya ndani. Kwa upande wa ushuru wa huduma, yaani *service levy,* kifungu cha 7(z) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kinazipa uwezo

Halmashauri za Wilaya kutoza ushuru wa huduma kwa wafanyabiashara kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo *(turnover)* ya mfanyabiashara baada ya kulipa kodi ya ongezeko la thamani.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, wafanyabiashara wote wa Zao la Mkonge wanatakiwa kulipa ushuru wa mazao, yaani *produce cess*, ambao ni kuanzia asilimia tatu hadi asilimia tano kwa mujibu wa Sheria. Aidha, wasindikaji wa Zao la Mkonge wanatakiwa kwa mujibu wa Sheria kulipa ushuru wa huduma ambao ni asilimia 0.3 ya mauzo baada ya kulipa ongezeko la thamani na *exercise duty.*

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a)Kwa kuwa tangu mwaka 2002 Wafanyabiashara wa Zao la Mkonge hawalipwi ushuru wa mazao kama ambavyo Sheria inahitaji; ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

(b)Kwa kuwa imethibitika bila shaka kuwa wafanyabiashara hawa wamekuwa wakikiuka kulipa kodi na kwamba mashamba mengi sasa yametelekezwa. Je, Serikali ipo tayari kufanya uamuzi wa haraka wa kufuta hati za mashamba haya ili Wananchi waweze kupatiwa ardhi hii?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika,mapendekezo ya Wilaya Mkinga ya kufutwa Hati Miliki ya Maashamba yaliyotelekezwa katika Wilaya ya Muheza na Mkinga yamekwishapokelewa na baada ya uhakiki kufanyika yamewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya uchambuzi wa mwisho na hatima yake kupata kibali chake cha kufuta Hati Miliki hizo.Tunafuatilia hilo kwa kushirikiana na watendaji wa Ikulu ili kuweza kukamilisha taratibu zile ambazo zinatakiwa ili

kumuwezesha Mheshimiwa Rais kufuta Hati Miliki hizo na baadae tutawasiliana na uongozi wa Mkoa baada ya kupata kibali cha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Mbuunge pamoja na Wananchi wa Mkinga na wa Muheza waendelee kuwa na subira wakati taratibu hizo zinakamilishwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dunstan Kitandula, kama ifauatavyo:-

Alitaka kauli kwa kutokulipwa ushuru kwa wakulima wa Zao la Katani toka mwaka 2002, kwa mujibu wa Sheria, Halmashauri zinazo uwezo na haki ya kwenda Mahakamani na kuwashtaki wale wote ambao wamekataa kulipa ushuru ambao ni haki kulipwa kwa Halmashauri husika.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika msimu wa pamba mwaka jana kule Bariadi Mkuu wa Mkoa aliwaambia *Bariadi Council* kuwa walipwe baada ya msimu na mpaka leo hii hawajalipwa karibu bilioni moja na laki tisa. Je, Mheshimiwa Waziri unatoa ushauri gani sasa ili kuhakikisha kuwa ile amri ambayo imeleta hiyo hasara inafidiwa mara moja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cheyo kuhusu ushuru wa Halmashauri ya Bariadi; ni kweli alipotoa amri ile niliwasiliana na Mkuu wa Mkoa na ninakamwambia kuwa ahakikishe ushuru huo unalipwa katika Halmashauri.

Ninaomba pia nichukue fursa hii kuwaagiza wale wote kuwa ushuru wa Halmashauri ni haki na katu tusivunje Sheria, kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo; na ninaomba Mkuu wa Mkoa husika azisaidie Halmashauri kupata ushuru wake kama ilivyokusudiwa. Kwa sababu nilimtahadhalisha mwanzo kuwa huenda kwa kuweka mwisho Halmashauri

zisipate ushuru na yeye mwenyewe alinihakikishia; kwa hiyo, ninaomba aendelee kusimamia ahadi yake aliyoitoa ili Halmashauri zipate ushuru wao.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, kwa hiyo, ninaomba nitoe matangazo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rajab Mohamed, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, leo saa na robo mchana, watakuwa na kikao chao Ukumbi Namba 227. Mheshimiwa Mnyika.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Nilishamwita mtu mwingine.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 55(3)(f) kuhusu jambo linalohusiana na haki za Bunge ambazo ninaamini ...

SPIKA: Kanuni namba gani?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kanuni ya 55(3)(f) kuhusu jambo linalohusiana na haki za Bunge, ambalo ninaamini kwa kadiri ya umuhimu wake, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wataniunga mkono. Alhamisi, siku ya maswali kwa Waziri Mkuu nilimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

SPIKA: Ujue kuwa hii haihusu haki za Mbunge, haihusiki hiyo sasa uliza hoja yako.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hoja yangu inahusu haki za Bunge kufuatia habari iliyoandikwa na gazeti la jana la Jambo Leo, Sakata la Jairo, Serikali yakamilisha Ripoti yake, Bunge lachambuliwa kama karanga, Ripoti yaozea mikononi mwa Spika, Serikali yakumbushwa ya *RICHMOND,* yaani Bunge lachambuliwa kama karanga na Ripoti yaozea mikononi mwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ninaamini jambo hili linahusu Haki za Bunge kwa sababu nilipomwuliza swali Waziri Mkuu juu ya Ripoti hii, Waziri Mkuu alitoa jibu kuwa, bado Ripoti haijawasilishwa kwa Bunge. Nilipomwuliza lini ripoti itawasilishwa kwa Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu alijibu wakati wowote kuanzia sasa. Kwa mujibu wa gazeti hili, inaonesha Ripoti ilishawasilishwa kwa Spika muda mrefu sana na imekaliwa kwa Spika mpaka inaozea mikononi mwa Spika na kwamba Ripoti hiyo imelichambua Bunge kama karanga. Sasa ningependa kutoa hoja kuhusiana na haki ya Bunge kupewa taarifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kuwa Bunge halijapewa taarifa; sasa ukweli ni upi hasa kwamba Waziri Mkuu tarehe 25 hakusema taarifa ya ukweli kwamba alikuwa ameshaleta taarifa kwako lakini haijafika kwa Wabunge?

Nia ya kutoa hoja hii ni ili Wabunge tujadili na hatimaye tupitishe Azimio la kuiwekea muda Serikali na kuuwekea muda Uongozi wa Bunge ili katika Mkutano huu wa Bunge katika kipindi cha tarehe saba mpaka tarehe kumi na mbili Juni, ambayo shughuli za kawaida za Serikali zitasimama, shughuli za Bunge zitaendelea, basi taarifa hii iweze kuwasilishwa Bungeni na Wabunge tuweze kuijadili ikiwemo kujadili hizi habari za kwamba taarifa hiyo tuone kwa ukweli na uwazi.

Kama ni ukweli kuwa hiyo Taarifa imelichambua Bunge kama karanga, na kama ni ukweli vilevile kwamba Taarifa hiyo imekaliwa na Spika muda wote huo bila kuwasilishwa; ninaomba kutoa hoja kuwa jambo hili lijadili kama jambo la haki za Bunge na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

SPIKA: Na hoja hii siikubali, naomba mkae chini. Siikubali kwa sababu hakuna wakati wowote Bunge linafanya kazi na magazeti; la kwanza. *(Makofi)*

Angefanya utaratibu huyu kuwa hilo gazeti na maamuzi yameshatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa ataitoa hiyo taarifa, mimi kama Spika, ninakataa sina taarifa ya namna hiyo. Sasa mimi siwezi ku-*operate* na magazeti ambayo mara nyingi yanasema uwongo juu ya mambo mengi. Kwa hiyo, siwezi kufanya kazi kwa kufuata magazeti. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2013/2014
Wizara ya Maji

(Majadiliano yanaendelea)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika tatizo la maji na ufinyu wa bajeti ulivyoelezwa, Serikali imelitizama tatizo hili na kuangalia kwa umakini hoja za Waheshimiwa Wabunge na kutazama umuhimu wa maji kwa Wananchi wetu na kuungana na hoja za Waheshiwa Wabunge, kuwa tatizo la maji tulipe kipaumbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika kutoa kipaumbele zaidi kwa upande wa maji, Serikali imelifanyia kazi suala hili kiundani na kuangalia namna ya kuweza kupata fedha za ziada kwa kutazama mafungu mengine. Tumetazama kiundani na kuona mafungu mbalimbali ya posho ambayo hayaathiri sana utendaji wa Serikali yakipunguzwa, basi tuyapungeze mafungu hayo tuongeze fedha katika Mfuko wa Maji. *(Makofi)*

Tatu, katika kwenda kuitekeleza kazi hii, uchambuzi wa ndani kwa maana ya *details*, Wizara ya Fedha nitawasilisha katika kipindi cha kuwasilisha *Appropriation Bill* ili maeneo yale ambayo yatapunguzwa yalete afueni kwa ajili ya Bajeti ya Maji, *details* hizo nitazionesha kwenye *Appropriation Bill.*

Nne, katika kutekeleza hiyo kazi *details* hizo nitaziwakilisha kwa Kamati ya Bajeti husika ili Waheshimiwa wahusika wa Kamati ya Bajeti waweze kuyaona maeneo ambayo tutayagusa kwa ajili ya kusaidia kuongeza *Vote* ya Maji na katika hilo, tumezingatia ripoti iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na kiwango kile ndicho tulichokizingatia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Unaweza kutaja kiwango chenyewe?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Maji, alieleza kwa undani jumla ya shilingi bilioni 184.5 ndicho kiwango ambacho Kamati ilipendekeza na Waheshimiwa Wabunge waliunga mkono.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tulikuwa tunapewa taarifa halafu tunaendelea.

MHE. KABWE Z. KABWE: Mwongozo wa Spika, kuhusiana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

SPIKA: Ninaomba mtulie kidogo halafu mtauliza mwongozo baadaye.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, kwanza, naiomba Serikali ilongezee pesa Wizara ya Maji ili kuweza kuwapatia maji Wananchi hususan walio vijijini.

Pili, Serikali ifute kabisa kodi katika madawa ya maji ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa mamlaka za maji na hivyo kupunguza gharama kwa mtumiaji.

Tatu, naiomba Serikali iendelee na mikakati yake ya ujenzi wa Visima vya Kimbiji na Mipera ili Wilaya ya Kisarawe pamoja na Mkuranga ziweze kunufaika na upatikanaji wa maji kutoka chanzo cha mipera.

Nne, naiomba Serikali iendeler kuiangalia Kisarawe kwa jicho la karibu kwani tatizo la maji limekuwa kubwa sana.

Tano, naishukuru Serikali kupitia Wizara yake na Taasisi yake ya *DAWASA* kwa kuweka mikakati yenye kutia moyo ya kuisaidia Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Hotuba ya Wizara ya Maji. Hotuba iliyojaa nia nzuri ya Wizara na mipango thabiti ya kuweza kuwapatia Watanzania maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono michango ya baadhi ya Wabunge kuhusu kupunguza bajeti ya Serikali upande wa *Other Charges (OC)* kwa asilimia kumi na tano angalau itasaidia kuongeza kwenye bajeti ya maji.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali iunde Wakala wa Maji kama vile *TANROAD.* Naona ingeweza kusaidia na kutoa lawama kwa Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti hiyo finyu, ningeomba Wizara ya Fedha (Hazina), ipeleke pesa kwa wakati ili iweze angalau kufanya kazi kwa wakati. Miradi yote iliyopangwa bajeti iliyopita takriban robo tatu haijakamilika kutokana na kuchelewa kwa pesa toka Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Mikumi unaendelea kukua kwa kasi. Kwenye Mradi wa Vijiji Kumi vya *World Bank* tumepata katika Mji Mdogo wa Mikumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa Waziri aelekeze nguvu katika kumalizia Mradi huo. Visima viwili vimechimbwa na kufanyiwa majaribio na vinatoa maji safi na hayana chumvi. Naomba chonde chonde mpeleke fedha kumalizia Mradi huo kwa

kujenga matanki na kufunga *pump* ili maji yatoke kumaliza tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Mikumi.

Mheshimiwa Spika, shukrani.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, Bajeti iliyoombwa na Wizara ya Maji kwa mwaka 2013/2014 ambayo ni jumla ya Sh. 398,333,474,000; kati ya hizo matumizi ya kawaida ni Sh. 18,890,254,000, Miradi ya Maendeleo ni Sh. 379,443,220,000. Katika fedha hiyo ya Miradi ya Maendeleo, fedha inayotegemewa kutoka ndani ni Sh.138,266,164,000.

Mheshimiwa Spika, fedha inayotegemewa kutoka nje ni Sh. 241,177,056,000. Fedha hii siyo ya kutegemewa kwani hivi karibuni tumeanza kusikia kwamba, Nchi za Ulaya nazo zimepatwa na mtikisiko mkubwa wa kiuchumi kiasi kwamba, hakuna uhakika kwamba fedha hiyo kutoka nje itapatikana kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, sote tu mashahidi wa jinsi ambavyo Watanzania wengi waishivyo vijijini wanavyoendelea kuteseka kutokana na ukosefu wa maji hasa wanawake na watoto wa kike, ambao hutumia muda mrefu kutafuta maji ambayo mwisho wa siku siyo safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii iongezewe fedha za kutosha ili Miradi yote ya Maji ambayo ni ya muda mrefu; kwa mfano, Miradi ya Vijiji Kumi iweze kukamilishwa na hivyo kuwaondolea adha Watanzania waishio vijijini ambao ndiyo wengi.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Vijiji Kumi ilionekana ingewezekana kabisa kuwapatia Wananchi maji kwa kuwachimbia visima. Haipendezi kwamba vipo visima vilivyochimbwa ambavyo havitoi maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuna wataalam wa maji waliosomeshwa kwa gharama kubwa kwa kodi za Watanzania; na kwa kuwa kabla ya kuchimba visima utafiti

hufanyika kwanza ili kutambua kama eneo husika lina maji ardhini na hivyo linafaa kwa kuchimbwa kisima; je, inakuwaje fedha nyingi kupotezwa kwa kutumika kuchimba kisima eneo ambalo halina maji kabisa?

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo yamechimbwa visima na matokeo yake maji hayapo, ni nini mpango wa Serikali katika kuwapatia maji Wananchi waishio katika maeneo yenye visima visivyotoa maji?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. JITU VRAJLAL SONI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naiomba Serikali yetu iangalie suala hili muhimu la maji, maji ni uhai. Bajeti iliyotengwa ni ndogo sana. Tunahitaji kuwa na Mfuko wa Maji Kitaifa na pia uamuzi ufanyike kupunguza bajeti za Wizara nyingine na kuongeza katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyochangia awali, Wizara zote husika zishirikiane kutatua matatizo ya maji. Maji katika maeneo ambapo yapo yatunzwe, uharibifu wa vyanzo na maeneo ya kukinga *(catchment area),* maji yameendelea kuharibiwa sana na tunaendelea kuangalia bila kuchukua hatua. Nashauri maeneo yote ya vyanzo, maeneo oevu, maeneo yenye hifadhi ya chini ya ardhi pamoja na pembezoni mwa mito na maziwa, yaendelee kuhifadhiwa kwa nguvu zote, maji siyo endelevu kama hayatatunzwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri mpango kabambe uandaliwe wa kuchimba mabwawa ya kuvuna maji. Idara ya uchimbaji mabwawa na visima iendelee kuboreshwa. Tupatiwe wataalam wa kuandaa michoro ya mabwawa kitaalam, visima vipimwe ili hata halmashauri na wadau waweze kutafuta fedha na wafadhili wakisaidiana na Wizara au Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha kwa kurekebisha masuala machache katika Sheria ya Manunuzi. Sheria hii ni kikwazo kikubwa katika kutekeleza Miradi ya Maji na miradi mingine ya maendeleo; kwanza, inachelewesha muda wa utekelezaji, gharama zinaongezeka sana za manunuzi na huduma ambayo ni zaidi ya bei za kawaida sokoni.

Mheshimiwa Spika, nashauri kipengele cha bei ya vifaa kitajwe katika *tender* na bei ya kutoa huduma katika eneo hilo ili wakati wa kuchambua na kutoa maamuzi, Kamati au Bodi za Zabuni waweze kulinganisha na bei iliyopo sokoni kwa wakati huo. Pia baada ya hapo, hizo bei zibandikwe au zitolewe katika vikao vya maamuzi ya juu na fursa ya yeyote anayetaka kuona apate.

Mheshimiwa Spika, nashauri kodi mbalimbali ziondolewe kwa Miradi ya Maji ili kupunguza gharama za utekelezaji kwa fedha kidogo iliyopo. Kwa mfano, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* katika mabomba, viungo, *pumps,* mota za umeme, kwa anayetoa huduma, yaani mkandarasi. Mafuta ya vifaa vya ujenzi, matenki, sementi, nondo na kadhalika, itapunguza gharama kwa takriban asilimia 18 hadi 36. Maji iwe mjini au vijijini ni muhimu na maji siyo anasa *(luxury)* ni muhimu na hitaji kwa maisha *(necessity)*.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali pia ifute kabisa kodi kwa madawa ya kutibu maji na madawa yote yanatumiwa na Taasisi au Wakala wa Maji na kupunguza matatizo ya kiafya na kwa kuondoa kodi hiyo pia gharama ya maji kwa mtumiaji wa mwisho itapungua.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iboreshe kwa kuongeza uwezo wa ofisi zetu za mabonde. Mabonde mengi hayana uwezo wa kujiendesha na kutoa huduma muhimu kwa watumia maji kutokana na ufinyu wa bajeti zao hata udhibiti wa rasilimali maji unakuwa mgumu. Wapatiwe bajeti ya nyongeza ili wapatiwe vifaa vya kupima maji kwa usalama, vifaa vya kupima maji ya chini ya ardhi. Wakiwa na vifaa hivyo vya kutosha wataweza kupima maeneo

mbalimbali na halmashauri, wadau wengine mbalimbali wanaweza kutafuta fedha za kuchimba maji na kuweka miundombinu ya kusambaza maji hayo.

Mheshimiwa Spika, narudia kushauri kuwa, Wizara zote zishirikiane na ngazi za Halmashauri, Idara zote ili wakati wa kuandaa miradi na wakati wa utekelezaji, zipange pamoja ili kupata ufanisi. Kila Idara isije na mpango wake; mfano, Babati, Idara ya Kilimo ilibuni Mradi wa Maji kwa ajili ya umwagiliaji Gichameda, Mradi ulitekelezwa kwa gharama kubwa. Mafanikio yapo na pia migogoro ipo ya watumia maji wengine wa Mradi huo. Hapo hapo chanzo hicho kinapeleka maji kwa matumizi ya kawaida ya binadamu kwa Mji wa Magugu, Matufa na maeneo yote ya jirani. Sasa Mradi mwingine mkubwa umeibuliwa na Idara ya Maji na tayari utaanza kutekelezwa, kupeleka maji ya matumizi ya binadamu kutoka chanzo hicho hicho kutoka Darakuta kwenda Minjingo. Sasa kuna migogoro iliyopo kabla ya Mradi huu unaotegemewa kuanza, Mradi huu utaongeza kabisa migogoro. Sera yetu inasema maji ya kunywa ni kipaumbele cha kwanza, haya yote ni sababu ya kutoshirikishana katika Idara mbalimbali wakati wa mchakato wa kuandaa Miradi. Huu Mradi wa pili ungeweza kutumia chanzo kingine ambacho kipo jirani na hapo ambapo hakuna watumia maji wengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali iangalie Miradi ya Maji Babati Vijijini, kuna tatizo kubwa huko. Sehemu kubwa ya Tarafa ya Mwada maji ya chini hayafai kwa matumizi kwa sababu ya *fluoride*. Maeneo ya kanda ya juu Bashnet, Ufana, Nar, Dabil maji ya chini ya ardhi yako mbali mita 125 hadi 200. Maeneo yote yanapata mvua za kutosha, tunashauri Serikali itusaidie kuchimba mabwawa ya kuvuna maji. Pia Serikali itusaidie wataalam wa kupima maji chini ya ardhi na wataalam wa kusanifu na kuandaa michoro ya mabwawa ili na sisi Viongozi wa Wilaya na Mkoa tuangalie pia namna ya kuomba msaada wa vifaa vya kuchimba visima na kutengeneza mabwawa.

Mheshimiwa Spika, kuna visima 15 vilipimwa na wataalam wa bonde la kati miaka michache iliyopita kwa ajili ya maji ya matumizi ya binadamu na pia umwagiliaji, hadi leo haijapangiwa bajeti ya kuchimba na tayari Wizara ya Nishati imepeleka umeme maeneo jirani na hapo. Naomba mpange bajeti kwa visima hivyo.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, naomba kujua Mradi wa Maji Mvomero na Turiani umefikia wapi? Ni fedha kiasi gani imetengwa kwa mwaka huu wa fedha?

Nasikitika kuona mtaro tu pasipo mabomba kutandazwa katika Mji wa Mvomero, Dibamba na kule Turiani. Nasikia Mkandarasi anadai fedha. Naomba sana Waziri atamke wazi ni lini Miradi hii itakamilika na kwa kutaja fedha zilizotengwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, kwa nini Shule zote za Serikali za Msingi na Sekondari hazina maji; mfano; Sekondari ya Manda, Luana, Msembe, Lugarwa, Livingstone na Ludewa zote hazina maji? Vilevile Shule za Msingi watoto wengine wanaenda shule bila kunywa chai na shuleni hakuna hata maji ya kunywa?

Mheshimiwa Spika, wanawake wengi wanahangaika, hutumia muda mwingi sana kutafuta maji. Akina mama wa Njombe, Ludewa na Makete, muda huo wangekuwa wanazalisha hususan kilimo. Kwa kuwa wanawake wanatumia muda mrefu kutafuta maji umaskini unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la maji Kata ya Amani, Mundindi? Naomba majibu Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la maji.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya kuchimba visima na mabwawa bila miundombinu ya kutumia maji ni matumizi yasiyo na manufaa ya fedha za umma *(Nugatory Expenditure)*. Mifano ipo mingi na hotuba imetaja visima na mabwawa kumi bila kutaja Bwawa la Nkowa na Machari – Mugumu. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara ikubali kugeuza mtazamo huu na makisio yote ya Miradi ya Maji iwe kuchimba chanzo pamoja na miundombinu ya matumizi ya maji ambayo ni pamoja na miundombinu ya kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Nkowa ni mfano wa kuchimba chanzo cha maji bila miundombinu ya kusafirisha maji na kusambaza kwa vijiji kwa matumizi ya Hospitali ya Mwalushu, vijiji na wanyama na ikiwezekana umwagiliaji wa mashamba. Bwawa hili lina maji kwa miaka kumi na tatu sasa. Lilifunguliwa na Rais mwaka 2006 na kila Kiongozi nimemweleza juu ya hali hii ambayo ni pamoja na Waziri Mkuu, Waziri wa Maji, Katibu Mkuu (TAMISEMI) na wa Maji. Tathmini ya gharama ni takriban shilingi bilioni 2.5, naomba fedha hizi zitengwe kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Lagangabili ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Hilima na kijiji hiki hakina maji na sioni jitihada yoyote ya kupata maji katika kijiji hiki. Mpango wa Ziwa Victoria ambao utachukua miaka mingi na mahitaji ni ya sasa hivi, naomba kijiji hiki kichimbiwe kisima kirefu pamoja na miundombinu ya kusambaza hayo maji hayo na kuyasafirisha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti kila mara inaahidiwa fedha lakini pesa haitolewi na Hazina. Jambo hili lazima litatuliwe, Bunge haliwezi kuamua kutoa kipaumbele kwa maji na Wizara ya Fedha inabeza uamuzi wa Bunge. Serikali itoe uamuzi kuwa, fedha yote itakayotolewa na Bunge basi itolewe kama *first charge,* tusipopata *commitment* hii ya Serikali basi yote yanayoamuliwa na Bunge hayatasaidia katika kilio cha maji.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nawapa pole Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ya kujaribu kutatua tatizo la maji linalowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Wakazi wa Ngorongoro wapatao 270,000 ni sehemu ya Watanzania wanaokabiliwa na tatizo la maji. Tulileta maombi ya fedha kwa nyakati tofauti (Tsh. 200,000,000 na Tsh. 400,000,000) kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Mji Mdogo wa Loliondo – Wasso. Tulikumbushia maombi hayo mara kadhaa bila mafanikio licha ya mimi Mbunge kuleta barua hizo hapa Bungeni na Wizarani na kuzungumza na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na pia Katibu Mkuu Sayi na kukabidhi barua hizo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji kwa Wakazi wa Loliondo – Wasso ni lita za ujazo 500,000 kwa siku. Fedha zinazoombwa ni kwa ajili ya kujenga tenki la lita za ujazo 680,000 pamoja na kukarabati miundombinu ya maji iliyojengwa mwaka 1989. Tenki lingine la lita za ujazo 200,000 litajengwa katika Kijiji cha Sakala ili kuhudumia Kituo cha Afya cha Sakala na Wananchi wa eneo hilo. Kwa heshima na unyenyekevu, naomba kupewa fedha hizo kwa madhumuni hayo.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, tatizo la maji safi ni kubwa kuliko takwimu zinavyolifanya lionekane. Katika maeneo mengi, hasa vijijini na hata mijini, huduma ya maji safi ni adimu. Katika Wilaya nyingi, hasa zilizo pembezoni kama Bukombe, huduma ya majisafi na hata majitaka imebaki kuwa ni ndoto kwa watu wengi. Kama Wabunge wengi walivyothibitisha, hali ni mbaya sana kwani mahali pengi watu wananunua maji kwa bei kubwa sana au wanatumia maji ambayo siyo safi na salama ambayo yanapatikana kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, Serikali imeshindwa kupeleka huduma ya majisafi kwa Wananchi wengi kwa sababu zifuatazo: Maji safi hayajapewa kipaumbele na hivyo kwa muda mrefu bajeti ya maji imekuwa ndogo; na hakuna mpango mkakati ambao ungetekelezwa

hatua kwa hatua hadi matatizo ya maji yakaisha kabisa. Kilichopo sasa ni Miradi michache iliyotawanywa nchi nzima na mingi ya Miradi hii inasuasua.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo pia la Miradi mingi kukabiliwa na ubadhirifu wa fedha za maji kwenye ngazi zote. Kwa kuzingatia umuhimu wa maji katika maisha ya binadamu na katika shughuli za kiuchumi, kwa nini Serikali isitoe kipaumbele kwa maji na kuandaa mpango mkakati wa kitaifa utakaolenga kumaliza kabisa tatizo la maji?

Mheshimiwa Spika, sasa nitajielekeza moja kwa moja kwenye matatizo ya maji yanayowakabili Wananchi wa Bukombe. Lengo ni kuonesha tatizo lilivyo kubwa. Bukombe ni miongoni mwa Wilaya zinazokabiliwa na tatizo kubwa la maji safi na salama. Hakuna maji katika Shule za Msingi na Sekondari. Wanafunzi hutumia muda mwingi kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya shuleni. Hakuna maji katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Miradi ya Ushirombo na Uyovu inasuasua; Wananchi wamekuwa wakipewa ahadi hewa kwamba Serikali itatoa fedha kwa ajili ya mtandao wa mabomba kwa miji midogo hii.

Wanawake wengi wanahangaika kutafuta maji kila siku badala ya kufanya shughuli nyingine za kiuchumi. Mathalani, Wananchi wa Kijiji cha Nalusunguti huenda kutafuta maji katika Wilaya jirani ya Chato.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuungana na Wabunge wanaopendekeza kuwa na mpango mkakati wa haraka wa kutatua tatizo la maji nchi nzima. Fedha itafutwe kwa njia yoyote ili watu waache kuhangaika na tatizo hili.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa maji Tanzania ni kubwa sana, kiasi cha kuwanyima raha Watanzania, kwani bila ya maji hakuna maisha, kwa kuwa maji ni uhai. Tatizo hili liko mjini na vijijini.

Mwathirika mkubwa wa ukosefu wa maji ni mwanamke na mtoto. Wanawake wengi wanatumia muda wao mwingi kutafuta maji katika masafa marefu. Mwanamke huyo anataka kujitafutia riziki kwa kujiajiri mwenyewe, huyohuyo familia inamsubiri kutoa huduma za ndani kama vile watoto na baba watoto pia. Hivyo basi, naiomba Serikali ifanye kila rai, watoe fedha katika fungu ambalo uzito wake haulingani na ule wa maji.

Mheshimiwa Spika, hali ya maisha ya Wananchi wetu ni mbaya sana kiuchumi, sasa tunamwongezea na mzigo wa kununua maji kila siku kwa ajili ya matumizi ama ya nyumbani au hata akiamua kujenga bado badala ya kununua vifaa vya ujenzi, analazimika kununua na maji. Huo ni mzigo mzito ukilinganisha na kipato chake; mlo mmoja unampa shida, je, maji atatoa wapi?

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo ambalo linahitaji umakini mkubwa sana kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Maji ambayo hupelekwa kwa nini haitekelezwi, inaonekana kama vile kuna ujanja fulani unafanywa na Wananchi wanaendelea kuteseka, fedha zinatengwa lakini miradi haikamiliki; ni kwa nini? Naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu sana ili kuhakikisha azma ya hotuba hii na malengo yanafikiwa ili watu waondokane na adha hii ya ukosefu wa maji ambao pia huchangia kupata magonjwa ya milipuko kutokana na maji yasiyokuwa salama.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii nzuri yenye matumaini isiwe pambo, itekelezwe kwa uhakika ili Wananchi wafaidike.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kwa mambo yafuatayo:-

(a) Ahadi ya Rais aliyoitoa mwaka jana Itigi, Manyoni kuhusu kuupatia mji huo maji ya kutosha.

Mheshimiwa Rais, alimsimamisha Mhandisi wa Maji wa Wilaya na Mkurugenzi *(DED)* kwa muda wa nusu saa aelezee Wananchi kwenye mkutano wa hadhara mikakati ipi itachukuliwa kuupatia Mji wa Itigi maji ya kutosha. Walieleza na kuhitimisha kwa kuiomba Serikali itenge fedha ili kazi hiyo ifanyike. Mheshimiwa Rais, akaahidi Wananchi kuwa Serikali yake itatekeleza katika kipindi kifupi ili Mji wa Itigi upate maji ya kutosheleza mahitaji ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, sioni mpango huu kwenye bajeti hii, napenda kupata majibu ni kwa nini mpango huu na ahadi ya Rais, hakuna fedha zilizotengwa?

(b) Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba, mchakato wa kusaka maji ardhini na kuyapata kwa matumizi ya binadamu na mifugo bado ni kitendawili. Mara nyingi wataalam wa kupima maji, wamekuwa wakikosea na kusababisha hasara pale wachimbaji wanapochimba na kukosa maji. Eneo kubwa la jimbo langu hasara hii imetokea mara kwa mara.

Napendekeza kuwa kazi ya kupima na kuchimba maji apewe mkandarasi mmoja ili atakapopima na kuchimba akakosa maji, basi hasara iwe kwake na si kwa Serikali ili kuokoa fedha za Wananchi. Hatua hii itawafanya wawe makini zaidi katika kutafuta maji kuliko utaratibu wa sasa ambapo mpimaji ni tofauti na mchimbaji ni tofauti. Fedha nyingi sana zinapotea kwenye mchezo huu.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vyote vya Jimbo hili la Manyoni Magharibi wakazi wake ni wakulima na wafugaji. Maji ya visima virefu hayatoshelezi mahitaji. Naiomba Serikali ije na mkakati wa kuchimba mabwawa. Hatua hii itatoa ufumbuzi wa matatizo ya maji.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na ahadi ya Serikali ya kuchimba bwawa la Kijiji cha Rungwe, mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa. Napenda kujua ni kwa nini hadi sasa utekelezaji wa ahadi hiyo bado haujafanyika?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha kwenye Kata za Idodya, Ndole, Aghondi, Ipande, Kitaraka, Mwamagembe na Rungwa ili kujua kina cha maji maeneo haya. Mara nyingi uchimbaji umeonesha kuwa hamna maji ardhini. Aidha, nguvu zielekezwe zaidi kwenye uchimbaji wa mabwawa na malambo.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo:-

(i) Miundombinu ya maji taka hasa kwa Wilaya ya Arusha Mjini ishughulikiwe, kuna maji mengi na machafu yanazagaa wakati wa mvua kiasi kwamba inasababisha magonjwa ya mlipuko katika Mji huu na hata kugharimu maisha ya watu.

(ii) Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru, kuna vyanzo vingi vya maji; mfano, Mto Dututi, Mlima Meru, nashauri Wizara iende ikafanye utafiti ili maji yaweze kupatikana na gharama yake itakuwa nafuu.

(iii) Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la visima vingi kutokutoa maji na hili ni kwa sababu ya visima hivyo vilichimbwa wakati wa mvua na inapokuwa kiangazi maji hayo hayatoki na hivyo kupoteza fedha nyingi za Serikali. Inasikitisha kuona tuna wataalam wengi wa kutosha na makosa kama haya yanatokea.

(iv) Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tatizo hili lipo kwenye mabwawa ya maji, yanachimbwa kwa gharama kubwa za ajabu, baada ya mvua mengi hubomoka na kukauka maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri bajeti iongezwe, pia Wananchi waelimishwe kuvuna maji ya mvua.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa kazi zake katika kipindi cha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya maji ni mengi katika maeneo ya vijijini na athari zake ni kubwa. Tarehe 14 Aprili, 2013 Wabunge Wanawake tulipata fursa ya kushiriki katika Kongamano la Wanawake waliowakilisha Wanawake wa Kanda zote za Tanzania. Wanawake kutoka Mikoa ya Lindi na Mtwara walitueleza yafuatayo:-

(i) Wananchi hasa akina mama wanatumia muda mwingi kwa siku kutafuta maji ambayo yako mbali na maeneo wanayoishi. Wastani wa muda ni saa nane hadi kumi. Hawana muda wa kufanya kazi za maendeleo.

(ii) Maji yanayopatikana siyo safi wala salama kwani ni kama tope kabisa. Chanzo cha maradhi.

(iii) Ili kupata maji akina mama wengi hutafuta maji nyakati za usiku.

(iv) Wanapotafuta maji usiku wakati mwingine huumia kutokana na giza kwani hujikwaa kwenye visiki na mawe au kuanguka katika mashimo, kukimbia wanapokutana na wanyama na wabakaji lakini mara nyingine wanawake hawa hubakwa. Inasikitisha.

(v) Jambo baya zaidi ni pale mama anapoamka alfajiri akiwa amemwacha mumewe nyumbani na kwenda kutafuta maji. Inaposhindikana kabisa kupata maji wanawake hulazimika kufanya ngono ili wapate maji kutoka kwa wanaume waliowahi kuchota maji usiku.

Kwa kweli inasikitisha sana na sasa tulipofikia kama Taifa ni pabaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, iongeze fedha za ziada kwa ajili ya maji vijijini na ichukue hatua za dharura. Pale ambapo MIRADI ya Maji itaonekana

kuchukua muda mrefu ni vyema Serikali ijaribu kutumia mapaa ya Shule za Msingi na Sekondari pamoja na Zahanati ili kuvuna maji ya mvua katika kipindi cha mvua za vuli mwaka huu 2013. Haitakuwa lazima kujenga matenki kwani yapo matenki ya plastiki yanauzwa kwa bei nzuri tu. Serikali ichukue hatua tafadhali kwani kuna kaya zinakosa mlo wa mchana kutokana na ukosefu wa maji. Mihogo na viazi vinachomwa na si kupikwa kwani hakuna maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, fedha zilizopo zitolewe na nyingine ziongezwe ili maji yapatikane nchi nzima.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Musoma Vijijini, napenda kuchukua nafasi ili nichangie Bajeti hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimekua Mbunge wa Jimbo la Musoma mfululizo toka mwaka 2000 hadi sasa. Kwa kipindi chote Ubunge wangu, wamekuwa wakinituma Bungeni kueleza shida yao kuhusu maji safi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Jimbo kwa kiasi kikubwa, takriban asilimia 60, limezingirwa na vyanzo vingi vya maji kama vile Ziwa Victoria, Mto Mara, Mto Kyarano na Mto Suguti, bado Wananchi wengi wanaishi bila kupata huduma ya maji safi na hivyo kusababisha mlipuko wa maradhi mengi yatokanayo na maji wanayoyatumia.

Mheshimiwa Spika, kila Bajeti ya Maji ilipokuwa ikiletwa hapa Bungeni, nimekuwa nikilia kwamba, Miradi mikubwa ya Maji iliyobuniwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwenye Awamu ya Kwanza, yaani mwaka 1974, ilibuni Miradi mikubwa mitatu ya maji Wilayani Musoma kama ifuatavyo: *Trunk Route 1* ambayo ililenga usambazaji wa maji kwenye maeneo kame ya maji ya Bunda; *Trunk Route 2* ambayo ililenga usambazaji wa maji kuhudumia maeneo ya ...; *Trunk Route 3* ambayo ililenga usambazaji wa maji kutoka Mto Mara sehemu ya Kirumi na kuhudumia Tarafa nzima ya Kyagata yenye Kata tatu za Bwiregi, Buswahili na

Nyamimange; *Trunk Route 3* ambayo ililenga kutoa maji kutoka Mugango, Ziwani *Lake Victoria* na kuyasambaza kwenye maeneo ya Nyang'oma, Kwikuba, Mwiringo, Bwai Kwituru, Mugango, Kamugegi, Kyatungwe, Kyabakari, Buturu, Butiama, Muryaza, Bumangi, Busegwe, Tringati na Masaha.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nasikitika kurudia kuliambia Bunge hili Tukufu kwamba, imetelekeza Miradi hii yote mitatu hatua kwa hatua bila aibu kwamba ilianzishwa na Hayati Baba wa Taifa. Mheshimiwa Naibu Spika, tunalipeleka Taifa letu hili wapi?

Mheshimiwa Spika, leo hii nimeshangazwa kusikia Wabunge wenzangu waliopendelewa kujengewa Miradi mikubwa eti kwamba hiyo miradi mipya ilikuwa ni utekelezaji wa ahadi za Rais wa Awamu ya Nne; sielewi!

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani kila Rais aliyepita alitoa ahadi kwa Wananchi ili itekelezwe na kila Rais ajae. Je, sasa ndiyo kusema ahadi za Rais wa Awamu ya Kwanza zimefutiliwa mbali? Mimi nilidhani kwa kuwa ahadi alizozitoa Hayati Baba wa Taifa zilitolewa na Rais wa Serikali ya CCM, CCM bado ipo madarakani kwa nini basi Miradi hii mitatu itelekezwe hivi hivi bila kujali mateso wanayopata Wananchi wa maeneo husika katika ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 51, Waziri anatuambia hivi, ninanukuu: "Miradi mipya katika eneo la Ziwa Victoria. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na *AFD* na *European Investment Bank (EIB),* itaanza utekelezaji wa Miradi ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza. Vilevile Mradi huo utahusu uondoaji wa maji taka katika Manispaa za Bukoba na Musoma, pamoja Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Lamadi, Misungwi na Magu. Miradi hiyo itaongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 35 hadi asilimia 90 kwa Mji wa Magu, kutoka asilimia tano hadi asilimia 90 kwa Mji wa Lamadi na kutoka asilimia 45 hadi asilimia 90 kwa Mji wa Misungwi.

Mradi wa kuboresha usafi wa mazingira kwa Jiji la Mwanza utahusisha kupanua mtandao wa maji taka kutoka asilimia 13 hadi asilimia 30. Mradi wa maji taka kwa Jiji la Bukoba utahudumia asilimia 15 na Mji wa Musoma ni asilimia 20 ya wakazi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yaliyotajwa hapo juu yako kandokando ya Ziwa Victoria, Jimbo la Musoma Vijijini nalo lote liko kandokando ya Ziwa Victoria. Kwa nini basi Miradi mipya hiyo isingegusa pia maeneo sugu ya Mugango, Buswahili na Wegero ambako mafuriko makubwa ya maji ya Mto Mara yamiminikayo Ziwa Victoria yasingeingizwa kwenye Miradi mipya hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka mingi Mto Mara umekua kero kubwa kwa Wananchi wa Tarafa ya Kiagata. Mwaka hadi mwaka Mto huo umekua ukifurika na kumeza maeneo ya wakulima na wafugaji waishio Kata ya Buswahili na Bwiregi. Wananchi hao wamekua wakiishi bila maji safi kwa muda mrefu. Eneo kubwa la ardhi yao limemezwa na maji ya Mto Mara, ambao sasa umejaa magugu maji mengi yanayo-*emit gas* nyingi mno ambayo wataalam wanasema ni *environmental disaster*. Nini Serikali inasema kuhusu janga hilo la Mto Mara?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Trunk Route 3* iliyoahidiwa na Hayati Baba wa Taifa mwaka 1974 imetelekezwa, Wananchi wa Kiagata sasa hawana maji safi wala mashamba ya kulima au maeneo ya kufuga. Wizara ya Maji iliwaahidi Rambo Wegero. Mwaka jana Serikali ilitumia kiasi cha fedha karibu shilingi bilioni moja. Kutokana na ufisadi uliofanywa kwa kubuni Mradi huo wa Rambo, muda mfupi baada ya kulijenga, Mto Mara ulifurika na kumeza Rambo hilo. Je, Serikali inasema nini kuhusu ufisadi huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nasema katika mchango wangu wa kusema nilieleza kwa kifupi kwa nini siungi mkono hoja hii. Sasa basi nimeeleza kwa kirefu masikitiko yangu kuhusu utelekezaji wa Miradi mitatu maarufu *Trunk Route 1, 2, 3*. Wilaya ya Butiama imenyimwa maji safi

kwa kipindi kirefu tangu Baba wa Taifa alipotuacha. Serikali imeziba masikio; kwa nini basi niunge mkono hoja Bajeti hii. Narudia tena kusema siungi mkono hoja hii.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kidogo juu ya Wizara hii kama walivyokwisha kusema wenzangu, maji ni uhai, kama hakuna maji hakuna maisha. Nchi yetu kwa ujumla ina tatizo kubwa sana la maji na tatizo hili linawaumiza zaidi akina mama ambao hutumia muda mrefu kutafuta maji na kupoteza muda wa kufanya kazi zao za maendeleo. Mbali na kupoteza muda wa kufanya kazi, ndoa zao zimevunjika na watoto wetu kupata mimba ambazo hazikutarajiwa kwa sababu tu ya ukosefu wa maji.

Matatizo ni mengi sana hata ukiangalia katika shule zetu za bweni utoro unaongezeka kwa sababu ya ukosefu wa maji huwezi kumuweka mtoto wa kike siku mbili bila kuoga hasa ukizingatia akiwa kwenye siku zake. Lazima hawa watoto watakimbia kama hatutaweza kufikiri kwa upana tatizo hili la maji basi maendeleo tunayoyatarajia na umaskini kupungua havitatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, suala la Mradi wa Vijiji Kumi nini tatizo la Mradi huu; kila siku tumesikia ndani ya Bunge hili lakini hautekelezeki? Tunaomba majibu sahihi ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wamechoka kunywa maji ya tope ambayo siyo salama na husababisha maradhi kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ya Chama cha Mapinduzi ione umuhimu wa suala hili la maji kwa Watanzania. Kama kweli tunataka maendeleo lazima tuanze na maji ili hayo maendeleo yaweze kupatikana; elimu inahitaji maji, afya inahitaji maji na kilimo kinahitaji maji. Maji ni muhimu sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni kidogo sana kuweza kutatua tatizo hili la maji; hivyo, naishauri Serikali kukaa chini

na kupitia upya bajeti hii ili iweze kuongeza fedha kwa ajili ya kutatua tatizo hili la maji. Tumesikia mipango mingi mizuri lakini haitekelezeki, sasa tumechoka tunataka utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mchango wangu, nategemea utafanyiwa kazi kwa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hamna kitu muhimu katika maisha ya binadamu na viumbe vingine kama vile mimea na wanyama kama maji.

Mheshimiwa Spika, tangu tupate Uhuru hadi sasa ni takriban miaka 52, lakini tumeshuhudia adha kubwa ya maji vijijini na mijini licha ya nchi yetu kujaliwa au kubarikiwa vyanzo vingi vya maji. Tumeendelea kushuhudia akina mama wakitembea kilometa nyingi kutafuta huduma za maji, kitu ambacho kinadhoofisha uchumi wa nchi kwani akina mama wamepoteza muda mwingi wakitafuta maji huku wakishindwa kufanya shughuli za maendeleo kama biashara ili kujipatia uchumi. Tumeshuhudia ndoa nyingi zikivunjika kutokana na adha ya maji, pia watoto wengi wamekufa wakati wakiachwa majumbani na wazazi kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Mkoa wetu wa Mara. Mkoa ambao tumebarikiwa na vyanzo vingi vya maji kwa maana ya mito na mabonde, hata ziwa. Kuna shida au uhitaji wa maji kwenye takriban wilaya zote za Mkoa wa Mara ambapo tumeshuhudia akina mama wakitembea umbali mrefu kutafuta maji na hata maji yenyewe yanayopatikana siyo salama wala masafi, mengi ni machafu, yenye rangi ya kahawia, yenye matope na vijidudu. Hivi kweli kwa hali hii magonjwa nyemelezi yatokanayo na maji machafu kama kichocho, minyoo, amoeba, kipindupindu yataepukika kweli. Serikali haioni kwa kuto-*solve* tatizo la maji inajiongezea gharama kubwa katika kutibu magonjwa na pia hupoteza nguvukazi kwani hamna uzalishaji wenye tija kwenye Taifa lililojaa Wananchi wenye maradhi, wenye kupoteza muda mwingi wakitafuta maji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ni ya mwisho au ni kati ya Wilaya zilizosahaulika kabisa. Hatuna Miradi yoyote ya mabwawa inayofanywa, hakuna Miradi ya visima vifupi au virefu, wala mbadala wowote ambao ndiyo suluhisho la maji. Hata pale Tarime Mjini, kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime, wakazi wake wengi hawana maji safi na salama. Pale Tarime Mjini maji yanatoka mchana tu na ni ya rangi ya kahawia, udongo au chai. Usiku hakutoki maji kabisa na ikizingatiwa Tarime tumepakana na Mto Mara, tuna Mto Mori, Mto Mlale na kadhalika, lakini Serikali inashindwa kutupatia huduma ya maji.

Mwisho, Mradi wa Visima vya *World Bank* unaonesha kufeli kwani visima vingi vimechimbwa lakini havitoi maji.

Pia umuhimu wa maji katika miji na vijiji; ni aibu Jiji kama Dar es Salaam kuna tatizo la maji. Mfano, eneo la Goba, Wananchi wake wanateseka sana kwa kukosa maji na wananunua ndoo ya lita 20 kwa shilingi 500. Jamani huyu Mtanzania wa kipato kidogo mfano cha shilingi 100,000, atoe labda shilingi 50,000 kwa maji au shilingi 2500 kwa maji, yaani ndoo tano kwa siku ina maana kwa mwezi ni shilingi 75,000, hapo bado pango, bado chakula, bado matibabu, nauli hiyo balaa shilingi 25,000 itamtosha kweli?

Naomba Wizara pia iisaidie jamii ya Wana-Dar es Salaam, Goba, kuna miundombinu iliwekwa lakini hamna maji, kisa eti hawa *Goba Water User Association,* sijui kuna ubadhirifu au kuna kwa nukuu ya Nape Nnauye; eti walifunga maji kwa sababu Jimbo la Ubungo linaongozwa na Mnyika. Kama ni kweli hii, ni aibu kabisa kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Ninaomba Serikali ifanyie kazi.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nimesikiliza na kuisoma Hotuba ya Waziri wa Maji. Kazi kubwa inaonekana kufanyika ili kuwapatia Watanzania maji safi na salama. Kasoro kubwa, uwekezaji wa maji ni *lopsided*. Hauchukulii uwiano kwa maana ya vijiji vyote, wilaya zote na mikoa yote. Katika kitabu hiki, Mbinga hususan Jimbo la

Mbinga Mashariki, lina kijiji kimoja tu cha Mahande chenye Mradi unaotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, licha ya majibu ya Wizara ya Maji ya kusema itahakikisha maji yanapatikana kwa wingi zaidi katika Mji wa Mbinga, lakini dhamira hiyo haionekani katika bajeti hii. Maana yake Mbinga inayochangia sana uchumi wa nchi hii kwa mazao ya kahawa na mahindi, haitakuwa na maji. Hili ni jambo lisilokubalika. Vipo pia Vijiji vya Paradiso, Ndongozi, Luhagali, Mabuni, Litumbandyasi na Kingoli, vina shida kubwa ya upatikanaji wa umeme!

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2013/14, Wilaya na Halmashauri ya Nyasa itaanza. Katika utekelezaji wa Vijiji Kumi Mbinga ina vitatu. Naomba Wizara iangalie uwiano huo ili vijiji hivyo vigawiwe sawa 5/5 kati ya Wilaya hizi Mbinga. Kwa upande wangu nitazungumza na Mkurugenzi ili achukue zifuatazo. Wakati wa mvua tunapoteza maji mengi na mengi yanaelekea ziwani. Ninaomba tupatiwe Mradi wa Mabwawa angalau mawili tu makubwa yatakayoweza kuhifadhi maji na kuwa chanzo cha maji katika vijiji vile ambavyo vina matatizo ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, nirudie tu juu ya kuifikiria Mbinga hasa mjini pamoja na vijiji nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji lililokithiri katika taasisi za Serikali hususani shule, vyuo na hospitali. Maji ni tatizo sugu sana katika shule zote za msingi na za sekondari zilizoko vijijini. Tatizo hili linapelekea wanafunzi badala ya kusoma kwa masaa yanayokubaliwa na Wizara ya Elimu wamekuwa wakitumia nusu ya masaa yao kutafuta maji ambayo hupatikana umbali mrefu sana. Bila maji shuleni tusitegemee utulivu na ufundishaji wa amani katika shule zetu. Naishauri Serikali kufanya kila iwezalo kutoa kipaumbele kwa shule, vyuo

na hospitali ili kuepusha magonjwa ya mlipuko ukizingatia taasisi hizi zina mkusanyiko wa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la maji katika Mkoa wa Singida hususani Singida vijijini mfano vijiji vya Sepuka, Mtunduru, Ighombwe, Mgungira, Msosa, Mhintini, Kinyampembee Itito katika Tarafa ya Ihanji na Sepuka. Naitaka Serikali itoe kipaumbele cha kuchimba visima ili kunusuru wananchi wa maeneo haya ambao wengi huishi maeneo yenye wanyama kama Tembo na huhatarisha maisha yao wanapokwenda kutafuta maji usiku na kwa umbali wa takribani kilomita 10-15.

Mheshimiwa Spika, mpango wa visima 10 kila Halmashauri. Mpango huu umeonyesha kushindwa na kwa kweli umewakatisha tamaa wananchi ambao walijitolea kuchangia ili kuweza kuchimbiwa visima. Katika Mkoa wa Singida, kijiji cha Puma, Kata ya Puma, wananchi walishakamilisha michango yao tangu mwaka 2011 lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea kwenye visima hivyo. Serikali sasa itoe tamko ni kwa nini bado inaendelea kuwatesa wananchi ilihali walishamaliza sehemu yao ya mchango kama walivyopangiwa? Ni kwa nini Serikali inaendelea kutegemea fedha za wahisani katika suala nyeti kama hili la maji badala ya kuwa ni kipaumbele muhimu na kutenga fedha za ndani ili kumaliza miradi ya maji nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji ya mvua. Pamoja na maeneo mengi ya nchi kupata mvua za msimu, lakini kuna wakati mvua hizi huja na mafuriko makubwa. Ni kwa nini Serikali haina mpango mkakati wa makusudi wa kuvuna maji ya mvua ambayo hupotea kwa wingi wakati wa masika na baada ya muda mfupi wananchi wanaanza kuhaha kutafuta maji?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kupunguza bei ya vifaa vya kuvunia maji ya mvua ili wananchi walio wengi waweze kumudu kununua na kurahisisha utunzaji wa maji?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Wizara isione umuhimu wa kushirikiana na Wizara zingine kama Elimu, Afya ili kupanga mkakati wa kuvuna maji ya mvua katika idara na taasisi zote zilizo chini yake?

Mheshimiwa Spika, mfumo wa maji taka. Hili ni tatizo la nchi nzima na hasa limekuwa sugu katika Jiji la Dar es Salaam. Hakuna udhibiti au mkakati mahususi wa kutengeneza mfumo endelevu wa kudhibiti maji taka hasa katika kipindi cha mvua ambapo licha ya mafuriko makubwa ambayo huharibu miundombinu ya barabara, pia wananchi hutapisha vyoo vyao na uchafu hutapakaa barabarani na kwenye makazi ya watu, matokeo yake ni magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara ambayo huua watu kwa kiwango kikubwa. Hii pia ni aibu kwa Taifa lenye miaka 51 ya kujitawala.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 52 wa hotuba ya Waziri, kupatiwa Mji wa Namanyere Dora za Marekani 1,900,000, naomba Wizara itekeleze kama ilivyoahidi katika ukurasa 52 ili kuondoa adha ya maji Namanyere.

Mheshimiwa Spika, pia ukurasa wa 168, mpango wa visima kumi. Katika Wilaya ya Nkasi, vijiji vya Kabwe, Tambaruka na Mkinga hakuna chochote kinachofanyika kabisa na hakuna pesa kabisa zilizopelekwa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini na mzaliwa wa Mwambao mwa Ziwa Tanganyika, nina mshangao mkubwa, katika kijiji cha Kamwanda – Kirando, kuna matanki mawili makubwa ya maji tangu enzi ya Mwalimu na maji ya Ziwa Tanganyika yako mita 100. Cha kushangaa kabisa ni eti wameamua kuchukua maji ya mto ambayo hayana uhakika sana yanaweza kukauka au kuchafuka na mifugo na binadamu na huo mto sasa tunategemea kwa umwagiliaji wa Bonde la Lwati, sasa hayo maji yako wapi kwa mradi huo? Mimi kama Mbunge nilishauri

wachukue maji Ziwa Tanganyika, jibu la ajabu eti maji ya Ziwa sio salama, ajabu hayo ya mto yanaweza kuchafuka wakati wowote ule. Wamekwenda kuchukua maji kilometa 8-9 wakati maji yapo mita 100 tu. Je, huo si ubadhirifu wa pesa za umma? Wakazi wote wa mwambao mwa Ziwa Tanganyika wanatumia maji hayo, iwe ajabu watu Kamwanda. Naomba Wizara iingilie kati suala hili.

Mheshimiwa Spika, ajabu nyingine kijiji cha Mkinga eti hatuna maji wakati Ziwa Tanganyika liko mita 50 tu toka Ziwani, hii ni ajabu kabisa, inashangaza sana hawa wataalamu wanatupeleka wapi? Wakazi wote wanaoishi Mwambao mwa Ziwa Tanganyika, wanaoishi Zambia, Burundi, Congo wanatumia maji ya Ziwa waache kudanganya na kuitia Serikali hasara bure, maji ya kunywa washauriwe kuchemsha tu.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nafasi nami nichangie katika hoja hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kama tujuavyo, kila mtu anafahamu kuwa maji ni uhai. Cha kusikitisha ni pale ambapo Serikali imeshindwa kuona kuwa suala la maji ni la kipaumbele kuliko jambo lolote. Maji ni zaidi ya barabara, sasa inakuwaje kulundika mabilioni ya fedha kwenye barabara badala ya maji au ni kwa vile magari yanayomilikiwa na wanaume yanahitaji kupita kwenye barabara?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la biashara ya maji. Hili ni tatizo kubwa. Serikali isikubaliane kabisa kulifanya suala hili kuwa la kibiashara kwa vile maji ni haki ya msingi ya binadamu, hivyo kutowapatia maji wananchi tuliowapa matumaini ya maisha bora halafu tunawatosa sio haki. Maji ni mojawapo ya tatizo kuu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambayo imepata Uhuru zaidi ya miaka 50 kushindwa kuwapatia maji watu wake ni fedheha. Inakuwaje nchi zilizo Jangwani mfano Libya, Misri na sehemu nyingine zenye majangwa ziweze kuwapatia

watu wake maji safi na salama, Tanzania ishindwe? Hii inamaanisha Serikali haijapata kiini cha ukosefu wa maji pamoja na tafiti zote zilizofanywa, Serikali ijizatiti upya.

Mheshimiwa Spika, maji yanazidi kupotea na Serikali inaangalia tu, mambo mengine hayahitaji fedha bali ni kujipanga tu. Iwapo Serikali za Mitaa zingechukulia jambo hili kama ni la kufa na kupona kwa kutumia Sheria ndogondogo za kudhibiti uharibifu wa mazingira ingewezekana tu. Nasema hivi kwa vile kwa umri wangu nimeishi wakati wa *Native Authority (NA*), hizi zilijali sana mazingira pamoja na vyanzo vya maji. Watendaji wake walikuwa waaminifu na walifanya kazi kwa uzalendo mkubwa. Walizungukia maeneo yote muhimu na kukagua kwa umakini sana na kutoa adhabu papo kwa papo bila kupokea rushwa, kwa njia hii wakayaponya mabonde ya maji.

Mheshimiwa Spika, wameeleza Waheshimiwa Wabunge wengi tu juu ya kuwapunguzia wanawake na watoto wao adha ya maji. Kinachohitajika ni kupunguza mipango ya makaratasini na maneno bali tuweke katika vitendo, tutumie wataalamu kutoka *NGO'S* walio na ujuzi wa kuvuna (*tap-water*) maji kutokana na mvua zinyeshazo za msimu. Serikali iwatie moyo, matokeo mazuri yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, tuwahi kuokoa mabonde yanayokauka sasa Wilaya ya Rungwe wakati yalikuwa yamejaa maji yatiririkayo na chemchem za maji safi na salama, sasa hamna tena, watu wameanza kuhangaika. Hebu Serikali yetu ifanyie kazi ushauri mdogomdogo tuweze kuwanusuru mama, dada na watoto wetu katika janga hili la kuzurura kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kusisitiza kuwa tuache kushabikia Serikali kuwa imefanya vizuri wakati haya ni maneno tu ya danganya toto mwaka hadi mwaka. Bali

tuitake Serikali kuongezewa bajeti na kuipa *timeframe,* kumaliza suala hili kabla ya bajeti nyingine ya 2014.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Jumanne Maghembe (Waziri) kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika utendaji wake wa kila siku. Pia nampongeza Naibu Waziri Dkt. Mahenge kwa uwezo mkubwa alioonyesha kwa kipindi kifupi tangu uteuzi.

Mheshimiwa Spika, katika uwasilishaji wa hotuba, tumeona kuwa wananchi wanasisitizwa kuvitunza vyanzo vya maji, rasimali za maji na matumizi bora ya rasimali za maji lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira ziweke mkakati wa wananchi kushiriki kulinda na kuelimishwa umuhimu wa uhifadhi. Ifike wakati sasa miti na rasimali zote ziingizwe kuwa ni mali ya Taifa na ziwe zinakabidhiwa kwa uongozi wa vijiji kama (*assets)* ambazo zinafanyiwa *inventory* kila mwaka au kila baada ya muda fulani ambao utapangwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushukuru sana kwa mradi wa maji Kandawale, Ngea na Njinjo, bado nasisitiza kuwa miradi inayohusu *World Bank* hakika ni kero kwa maana kila eneo lina tatizo la aina yake. Ila katika Wilaya ya Kilwa tatizo kubwa lipo katika uchangiaji wa asilimia kumi. Naiomba Serikali kwa maeneo ambayo yana hali duni kimaisha basi yenyewe ibebe jukumu la kuchangia kwa niaba ya wananchi. Licha ya kuchangia pia Serikali iweke jitihada katika usimamizi wa miradi maana yapo maeneo mengi ambayo miradi imefanyika lakini hakuna mafanikio kwa maana maji hayakupatikana na Wakandarasi wameshalipwa stahili zao.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mtandango ambapo tulipewa mradi wa *World Bank* kwa bahati mbaya maji hayakupatikana. Hivyo, tunaiomba Serikali ikubali kubadilisha chanzo cha maji kwenda Mikereng'ende ambapo maji yapo mengi na si ya kuchimba sababu eneo hili lina chemchem.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mgawanyo wa fedha za maji uangaliwe upya maana maeneo ya mijini yanapangiwa pesa nyingi bila sababu za msingi na mara zote wao ndio wamekuwa chanzo cha matatizo kwa maana walishindwa kulipia *bills* za maji katika mamlaka husika hadi kupelekea mamlaka hizo kufilisika. Pia ukataji wa miti au uharibifu wa mazingira unachangiwa sana na mahitajio ya mijini. Napendekeza katika mgawanyo wa miradi, licha ya kubuniwa na Halmashauri au Wizara, tuweke mfumo ambao viongozi kama Wabunge na Madiwani washiriki katika usimamizi wa miradi au mingine ipitie katika mifuko ya Jimbo. Hali ya wananchi kutokubaliana na vigezo vinavyotumika sasa kwa maana ya idadi ya watu, wananchi wa vijijini kama Kilwa wana mazingira hatarishi zaidi kuliko mijini lakini pia izingatiwe kuwa ukubwa wa eneo la Kilwa kama Wilaya ni sawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, hatua madhubuti zichukuliwe ili kuimarisha ujenzi wa mabwawa ili kuhifadhi maji ambayo mengi yanapotea bila kutumika huku ikifika wakati wa kiangazi kunakuwa na upungufu mkubwa sana wa maji katika maeneo yote nchini haswa vijijini. Kama inavyoeleweka Tanzania haina tatizo la maji kwa maana vyanzo ni vingi mno, tatizo ni *management* ya maji haya.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sasa katika maeneo mengi haswa ambapo wananchi kwa nguvu zao wameamua kuchimba visima, lakini matokeo yake wanalazimishwa kulipia kila mwezi hali ya kuwa wametumia vyanzo vyao vya fedha kuanzishwa visima hivyo na wanatumia kwa matumizi yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia sasa kubuni mbinu mpya za mapato ili kuweza kuimarisha huduma za maji

vijijini haswa kwa kutumia mamlaka za maji mijini kama *DAWASCO, DUWASA, MUWASA* na kadhalika) ziwe zinatoa gawio kwa mfuko maalum utakaoanzishwa ili kumaliza tatizo la maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Maji akijibu swali langu namba 74 kwenye Mkutano wa Tatu, Kikao cha Tano, tarehe 12/4/2011, Serikali iliahidi kuunga mkono juhudi za wananchi wa Tarafa ya Mlola kwa kulipia michoro ya mradi wa maji unaoitwa Mtumbi *Water Supply* ambao ungehudumia vijiji katika Kata tatu za Kwekanga, Malibwi na (Kilole) Makole. Kuanzia hapo mwaka 2011 hadi hii leo ramani hazijachorwa na kukamilisha kazi hiyo, je, Serikali inatekeleza lini ahadi hii? Naomba ramani hiyo ikamilike na liingizwe kwenye awamu ya pili ya miradi ya *World Bank.*

Mheshimiwa Spika, maji mji wa Lushoto. Nashukuru ziara za Manaibu Mawaziri wawili wa Wizara hii ya maji Mheshimiwa Lwenge na Mheshimiwa Dkt. Mahenge kutembelea Lushoto kujionea na kusikiliza vilio vya wananchi wa mji wa Lushoto kuhusu uhaba wa maji. Mawaziri wote wameahidi kusaidia katika kutafuta suluhu au ufumbuzi wa tatizo la maji. Naomba Wizara itutumie fedha tulizoomba japo shilingi milioni 200 kupunguza tatizo hilo la maji kwa kujenga *tank* pale Magamba na kuunganisha maji kutoka Magamba kupelekwa kwenye matanki ya Kwembagon ili kupunguza tatizo hilo wakati tukisubiri mradi mkubwa wa maji utakaotekelezwa kwenye mpango wa maji mijini kupitia Benki ya Dunia. Nitasikitika sana kama sitapata msaada japo wa hizo shilingi milioni 200 japo tumeomba shilingi milioni 400 kama tulivyoandikia Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa vyanzo vya maji. Kwa wananchi tunaoishi milimani, tunahitaji msaada wa Serikali Kuu katika kulinda na kusimamia vyanzo vya maji hasa katika maeneo ambayo tunategemea maji ya mtiririko (*gravity*). Vyanzo vingi vimeharibika kutokana na usimamizi hafifu, maji

katika maeneo mengi ya milima hutoka kwenye chemchem, katika misitu. Tunaomba kama ikibidi Halmashauri itengewe fedha mahususi za ulinzi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya maji. Wananchi wameanzisha mifuko ya maji, nashauri mifuko ya maji igeuzwe iwe Mamlaka ya Mfuko wa Taifa wa Maji – Serikali ichangie na wananchi wachangie katika mfuko wa Taifa wa Maji. Serikali ibuni vyanzo vingine vya kuimarisha mfuko huo, kama vile *Road Fund* inavyofanya kazi, Mfuko wa Maji ukianzishwa kutakuwa na mtandao thabiti wa kuwafikishia wananchi maji kama barabara zinavyojengwa.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, hali ya maji katika Jiji la Dar es- Salaam bado hairidhishi. Pamoja na mipango mizuri ya Serikali kutatua tatizo hili kubwa la maji katika Jiji la Dar es Salaam, tunaomba sana Serikali ihakikishe ahadi ya kuondoa tatizo hili la maji ifikapo 2014/2015 inatekelezwa kama mlivyoahidi wananchi wa Dar es- Salaam hususani Jimbo la Kinondoni wamevumilia kiasi cha kutosha na ahadi hizi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya wananchi wa Jimbo la Kinondoni na Dar es Salaam kuwa haya mliyowaahidi mtayatekeleza. Hata hivyo, wakati tunaendelea kusubiri mipango hiyo, tunaomba haya maji kidogo yanayopatikana yagawanywe kwa wananchi bila upendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali idhibiti wauza maji ambao wamefunga *Water pump* na maji yote wanayaelekeza kwenye matanki makubwa na visima vikubwa walivyochimba kuhifadhi maji hayo na kuyauza kwa bei kubwa. Tena wanashirikiana na baadhi ya watumishi wa *DAWASA, DAWASCO,* tunaomba kuwe na udhibiti mkubwa kwa hawa wanaouza maji.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa majitaka katika maeneo ya Mwenge, Kijitonyama ni kero kubwa, chemba zinaziba, zinamwaga majitaka mitaani, kwenye makazi ya

watu lakini hakuna hatua za haraka zinazochukuliwa kuzibua au kukarabati na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi. Tunaomba Serikali ichukue hatua za haraka kukabiliana na tatizo hilo la kuvuja majitaka.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kinondoni, Block 41 na Kinondoni Shamba hakuna kabisa mtandao wa maji taka na eneo hilo ni oevu hivyo ni vigumu kuhifadhi majitaka kwenye mashimo. Tunaomba maeneo hayo yaunganishwe kwenye mtandao wa majitaka ambao unapita kandokando ya barabara ya Ally Hassan Mwinyi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, kitabu cha bajeti ya Wizara, ukurasa 54-55 kuhusu maji Magu Mjini, kinasema kwamba taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na kwamba kazi hiyo itaanza mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Wizara niliyoitaja hapo juu hailingani na kile kilichotendeka hadi sasa ukweli ni kwamba: Mtaalamu Mshauri alishafanya upembuzi na usanifu na kuja na kiasi cha gharama zinazohitajika kutekeleza mradi huu. Mtaalamu Mshauri huyu alitumia takribani Tshs millioni 900. Niliuliza swali hapa Bungeni nikajibiwa na Wizara kwamba zabuni imeshatangazwa. Leo anatamka kuwa anatafuta tena Mtaalamu Mshauri afanye tena upembuzi yakinifu ambao tayari ulishafanyika.

Mheshimiwa Spika, mimi naona Serikali haina nia thabiti ya kuwapatia wana Magu maji kabla ya 2015. Matokeo ya kutotekelezwa mradi huu ni janga kwa CCM kwa sababu: Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wana-Magu kuwa wasimuulize Mbunge kuhusu maji wamuulize yeye. Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alituhutubia Mkutano wa hadhara mwaka jana na kusema kuwa angetoa (ndani ya muda mfupi toka siku hiyo) fedha (nafikiri million 800) ili

utekelezaji wa mradi uanze kutekelezwa kwa lengo la walau kupunguza kero za wana–Magu kuhusu maji. Mimi toka niwe Mbunge miaka 12 iliyopita kila awamu nimekuwa nikiwaahidi wana –Magu kuwa chagueni CCM ndiyo suluhisho la tatizo la maji, waliniamini awamu tatu na nina mashaka tena iwapo wataendelea kuwa na imani na CCM 2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilikuja kuiunganisha Magu na Ngudu kabla ya bajeti hii na sasa Waziri anaiunganisha tena Magu (kwenye ukurasa wa 54-55 wa hotuba ya bajeti) na Bariadi na Mwanhuzi. Hii inashangaza na inakatisha tama, wana-Magu tutaenda tuwaambie nini tena? Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri/Naibu Waziri/Katibu Mkuu mje Magu ili muisaidie CCM kuelimisha wana Magu kuhusiana na hatima ya kero yao ya maji maana mimi sioni pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa unyonge sana.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Maji ni uhai, kiumbe chochote hakiwezi kuishi bila ya maji hivyo basi Serikali ni vyema ikaangalia ni namna gani ya kuweza kutatua tatizo hili sugu ndani ya Mikoa yetu, wanaoteseka zaidi ni wanawake na watoto, wengi wao wanahangaika mpaka usiku na watoto migongoni wanatafuta maji wengine wanaliwa na simba na wanyama wakali wanapoteza maisha yao kwa sababu ya kuhangaika kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze fedha katika Wizara hii ili iweze angalau kuongeza idadi ya visima katika yale maeneo ambayo yana matatizo makubwa. Pia kuwe na wataalamu ambao wanaweza kutoa elimu kwa wananchi wetu waache tabia ya kulima katika vyanzo vya maji. Hali hii ya wananchi kulima katika vyanzo vya maji inazidisha ongezeko la kupungua kwa maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Ziwa Victoria, kuna Ziwa Tanganyika ambayo yana maji mengi, hivyo basi naishauri Serikali isambaze maji angalau katika sehemu ambazo ziko karibu na Maziwa haya. Matatizo haya yapo hata katika maeneo yaliyo karibu na Maziwa haya. Pia kuna Mito katika baadhi ya maeneo yetu kwa mfano Mto Ruvu, Mto Nanyumbu, Serikali iangalie namna ya kutafuta njia ya kusambaza maji. Wananchi wanateseka sana na hili limekuwa ni tatizo la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, malalamiko makubwa ni kuwa miundombinu ni chakavu na baadhi ya wananchi wahalifu wanabomoa miundombinu na kuuza chuma chakavu. Naiomba Serikali itumie miundombinu isiyokuwa chuma, kama ni mabomba ya plastiki au mengineyo ili maji yaweze kusambazwa bila ya wahalifu hawa kutokuweza kuharibu miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itumie njia ya kuhifadhi maji ya mvua ili yaweze kutumika kipindi cha kiangazi.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa niaba ya wakazi wa Musoma Mjini, kwa mradi wa maji ambao sasa unatekelezwa, japo imechukua muda mrefu sana kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mbali na utekelezaji wa mradi huu ila bado kuna matatizo katika Mamlaka hasa katika shughuli za uendeshaji na hii ipo kwenye Mamlaka karibu zote hapa nchini. Mamlaka zimeajiri watu wa kukata maji kuliko kuunganisha maji, hili ni jambo la msingi la kuangalia maana inachounganisha raia na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara bado ipo mbali na Mamlaka za Maji za Miji ambapo utendaji wa baadhi ya Mamlaka umekuwa wa kusuasua na wakati mwingine umekuwa mbaya sana. Wilaya ya Butiama ikumbukwe, maana kijiji kile mbali na kutangazwa kama Wilaya bado maji yanatoka mara tatu kwa mwezi na imepelekea baadhi ya watu kutolipa ankara zao za maji.

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo makubwa sana ya maji pia Serengeti na Musoma Vijijini na Butiama. Ikumbukwe pia kuna mradi mkubwa sana unatekelezwa Musoma Mjini, kwa nini isiangaliwe namna ya kuyafikisha maji yale Musoma Vijijini, Butiama na Serengeti kama ilivyo mradi wa Ihelele unaotoa maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama kuelekea Tabora? Napenda sana kuona wakati Mheshimiwa Waziri anatoa majumuisho basi aje na majibu mahususi yenye mikakati thabiti ya kupeleka maji Butiama na Serengeti kwa kutumia mradi unaotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pia najua mahitaji ya maji yapo kwa aina tofauti, napenda kutoa rai yangu kwa Wizara kukaa na Mamlaka za Maji za Miji au Halmashauri ili tuone ni jinsi gani tunaweza kuweka *fire hydrants* kwa Miji inayokuwa ili itusaidie sana wakati wa uzimaji moto.

Mheshimiwa Spika, hujuma za miundombinu zipo katika maeneo ambayo mabomba ya maji yanapita na vijiji havina maji hapo hujaza hasira na kupasua mabomba. Nashauri sehemu zote zenye mikusanyiko zipatiwe maji kwa binadamu na mifugo yao ili angalau kupunguza sana hujuma zinazotokea.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na Wabunge na wote kilio chao ni maji. Napenda sana kukupa shukrani kwa mradi unaotekelezeka Musoma Mjini kwa ufadhili wa *AFD*, tafadhali sana mradi huu huko mbele basi maji yafike Musoma Vijijini, Butiama na Serengeti kama ulivyo mradi wa Ihelele.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, kila Bonde na Mamlaka husika wabainishe vyanzo vyote vya maji na mikakati ya kuvitunza na kuhakikisha *sustainability* ya *water resouces* kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maji Mjini Kibaya ijengewe uwezo zaidi ili iweze kutoa huduma kwa wakazi wa Kibaya wenye shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, usimamizi uboreshwe kwa ajili ya miradi hii ya vijiji 10 hali bado ni mbaya sawa na ilivyokuwa katika awamu ya kwanza ya mradi huu wa vijiji 10.

Mheshimiwa Spika, Wilaya zilizomo katika maeneo kame ikiwemo Kiteto, zipewe kipaumbele kwa ajili ya *programme* ya maji kwa binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge fedha ya kukarabati mabwawa yote yaliyovunjwa/bomolewa na maji katika masika ya 2013. Bado gharama ya ukarabati ni ndogo kuliko kujenga maeneo au mabwawa mapya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe Mfuko wa Maji ili utumike kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maji iongezewe fedha katika msimu huu.

MHE. MCH. DKT. GERTUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa ya maji Wilaya ya Kilombero. Tatizo sugu la maji Mji wa Kilombero, Ifakara, wananchi wanalia kwa kukosa maji safi. Tunaomba mradi wa maji wa Kiburuguto shilingi bilioni 213 ufanyiwe kazi, ni kilio changu Bungeni maji kwa wakazi wa Ifakara na Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, mito 38 iko Wilaya ya Kilombero, kila kijiji kina Mto wake, kijiji cha Sonjo kuna Mto Sonjo, Idete – Mto Idete Kiberege – Mto Kiberege na kadhalika. Tatizo ni nini? Mito hii mingi ni ya msimu. Tunategemea visima vya Mdundiko navyo ni vya msimu. Ahadi ya Rais daraja na maji 2005/2010 lakini mpaka leo shilingi bilioni mbili mnasema nyingi. Tunaomba mtukumbuke Kilombero.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

MHE. MAJALI K. MAJALIWA: Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri hali mbaya ya maji aliyoishuhudia akiwa ziarani na Mheshimiwa Rais kule Wilaya ya Ruangwa ambako aliona na kusikia wananchi wakilalamikia suala la ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga miundombinu ya maji kijiji cha Maudara, Makao Makuu ya Wilaya ya Ruangwa, Rais na Mhandisi walitoa matumaini ya kupata maji kutoka visima kumi (10) vya Kitandi ambavyo iliahidiwa kuunganishwa kwenye mtandao wa mabomba yanayosambaza maji mjini Ruangwa. Sijaona mpango huo kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwenye orodha ya vijiji vitakavyotekelezewa miradi ya maji vijijini, nashauri vijiji vya Naudagala na Ngau vianze kwanza kwa sababu ya hali mbaya iliyopo akilinganisha na vijiji vinavyoanza. Vijiji hivi vina mradi wa maji wa mwaka 1970 uliokuwa na mtandao wa bomba ambao ulikuwa unahudumia vijiji vinne (Naudagala, Ngau, Chimbila B na Namahima). Mahitaji hapa ni kuweka upya mtandao wa bomba ili maji yasafiri kwenye vijiji tajwa.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha za Mfuko wa Maji kwa Halmashauri ya Ruangwa hazitoshi kutokana na kuwepo kwa matatizo makubwa ya maji kwenye vijiji vyetu. Naomba mgao huo uangaliwe upya ili vijiji hivi navyo vipate maji kwa njia ya visima virefu.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu, nitapata majibu ya hoja zangu, ahsante.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji anifahamishe ni lini Mji Mdogo wa Laela utapata maji? Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Maji alifanya ziara katika Mkoa wa Rukwa na alijionea mwenyewe namna wananchi wanavyopata shida ya maji katika Mji Mdogo wa Laela na alishauri vichimbwe visima vya maji badala ya maji ya msererekо na akasema fedha ipo, hadi leo hii hakuna fedha

na Halmashauri inasubiri fedha hizo zipelekwe, je ni lini fedha hiyo itapelekwa? Maeneo ya kuchimba visima yameshaandaliwa, majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Maji yanasubiriwa ikiwa ni pamoja na fedha. Ni lini maji yatapatikana Mji Mdogo wa Laela? Namwomba sana Waziri atakapokuwa anatoa ufafanuzi wa hotuba yake, afafanue juu ya tatizo la maji Mji Mdogo wa Laela na atoe kauli tatizo ni fedha au nini?

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuiomba Wizara ya Maji kuisaidia Mtwara Vijijini katika kuondoa tatizo la maji kwani zaidi ya 60% ya wananchi wa Halmashauri ya Mtwara haipati maji kabisa (salama wala yasiyo salama).

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara inao mradi ambao *AMREF/EU* walionesha nia ya kusaidia katika Kata za Mruma, Kiromba, Njengwa, Mtiniko, Kiyanga, Mtimbwilimbwi na Nitekela. Cha ksikitisha sasa ni zaidi ya miaka mitano mradi umeweza kufikisha maji chini ya 30% (thelathini). Kitu ambacho wananchi kinawashangaza na kuwasikitisha ni kitendo cha *AMREF* kuanza kujenga matenki na kutandaza mabomba katika maeneo hayo kabla hata ya kuwa na uhakika wa chanzo cha maji. Mradi huu umekamilika kwa kukamilisha kujenga matenki na kuchimbisha wananchi mitaro na kuzika mabomba ardhini baada ya hapo wananchi wanaambiwa wameshindwa kupata chanzo cha maji. Namwomba Waziri au Naibu wake kutembelea Mtwara vijijini ili wakajione kiasi cha fedha kilivyotumika vibaya kwa kujenga miundombinu ambayo ni mapambo tu kwa wananchi.

MHE. CELINA O. KOMBANI: Mheshimiwa Spika, Mji wa Mahenge, Wilaya ya Ulanga waliahidiwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete mwaka 2008 kwamba atawapatia shilingi milioni 200 kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji katika Mji

wa Mahenge. Napenda kuwashukuru sana Wizara ya Maji wamefanikisha zoezi hili kupitia *MORUWASA* wametekeleza mradi huu kwa kiasi kikubwa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mradi huu umebakiza pampu ambayo inagharimu shilingi zaidi ya milioni 300 na vifaa vingine shilingi karibuni 150. Naomba katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014 watenge fedha ili kumaliza mradi huu wa maji Mahenge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, niipongeze Serikali na Wizara ya Maji kwa kazi nzuri inayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, jambo lililonikwaza ni kwamba katika mwaka huu *JICA* itaendelea kusaidia lakini katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini maeneo yaliyotajwa ni Mabama na Ufuluma lakini tayari Mabama mradi ulishaanza tangu mwaka juzi na Ufuluma walitoa ripoti kwamba maji yameshindikana kupatikana, sasa kuna nini jipya katika bajeti ya mwaka huu? Naiomba Serikali ione uwezekano wa kuongeza maeneo kwenye mradi huu wa *JICA* katika Jimbo la Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013 niliahidiwa kupewa shilingi 100 milioni ili kulinda vyanzo vya maji ya Chemchem lakini hadi leo hata nusu haijatolewa na vyanzo vinaendelea kuharibika. Naomba Serikali itusaidie haraka kutunza vyanzo vya maji ya Chemchem.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Bomba la Maji kutoka Shinyanga – Nzega –Isikizya – Tabora ambalo ni mkombozi kwa tatizo la maji Mkoani Tabora lakini bado tuko mbali sana na utekelezaji. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kuanzisha mradi huu lakini pia ione uwezekano wa kusambaza katika vijiji vinavyopitiwa na bomba la maji kwenda zaidi ya kilomita 12 ili tuweze kusaidia wananchi walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ione namna ya kuomba hela za *World Bank* zitoke kwa muda muafaka maana miradi ya *World Bank* katika Jimbo langu inasuasua sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Maji, atakapojibu aseme kuhusu ombi langu la maji kijiji cha Mwandiga na Kibingo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, mbona sijasikia wala kuona hela za kusambaza mabomba Makao Makuu Songe ambapo ni kero kubwa sana kama ulivyoona na inakimbiza sana Watendaji wazuri. Waziri alininong'oneza kuwa shilingi 400,000,000/= zimetengwa, nami jana nimewaambia kwenye *Finance* Kilindi na wakashangilia.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kwamaligwa linahitaji shilingi milioni 500 tu kujengwa upya baada ya kuvunjika na mvua zinaelekea mwisho. Bwana linasaidia vijiji 15, Kata nne, ng'ombe zaidi ya milioni 12, mbuzi, uvuvi kilimo cha umwagiliaji na maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nimejaribu kupitia mpango wa miradi ya 2013/2014 katika ukurasa 142, bado Halmashauri haikuweza kuleta maombi ya fedha kwa ajili ya ule mradi wa Muhunga Heru Juu na Kalunga, unaweza ukaona ni kwa kiasi gani hawajali. Hilo wanalifahamu tangu *last year please* naomba wa-*check* la kufanya kwa *project* hiyo ya *rehabilitation.*

Mheshimiwa Spika, aidha vijiji vya Kidyama, Kigondo havina maji kabisa na havipo mbali na Mji wa Kasulu. Mhandisi haoni umuhimu wa watu hao kupata maji?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri asahihishe katika kitabu chake ili walau ule mradi wa *Muhunga Ward* upate fedha mwaka huu.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu ya maji kwa uhai wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kuwa maji ni miongoni mwa changamoto ambayo inawakabili wananchi hasa wanawake waishio vijijini. Kwa hiyo, bado tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha changamoto hii inaondoka kwa gharama yoyote ile kwa uhai na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji mijini, naomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ya kuboresha huduma ya maji kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya maji na kupunguza tatizo la maji kwa kiwango fulani. Naipongeza pia mipango iliyopo ya kuhakikisha kuwa miji iliyobaki nayo inapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji vijijini. Naomba kuwasilisha kilio cha wanawake na wananchi waishio vijijini kuwa wanalo tatizo kubwa pamoja na jitihada zinazofanyika bado huduma ya maji iko chini sana. Naomba Serikali ijitahidi kutafuta fedha za ziada katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 ili ziweze kujenga miundombinu ya maji vijijini ili wanawake na wananchi waweze kuepukana na adha hii ya kushinda wanatembea umbali mrefu kutafuta maji. Nashauri wakati wa kuandaa bajeti 2014/2015 katika kuondokana na tatizo hili la ukosefu wa maji vijijini, Serikali iweke mkazo kwa kutenga fedha za maji vijijini kuwa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kodi ya madawa ya maji. Nashukuru mpango wa kupunguza kodi ya madawa ya maji. Ombi langu kodi hii ifutwe kabisa kama tulivyoondoa kodi nyingine kama hii ya maji ili Mamlaka za Maji ziweze kutoa huduma kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Maji zote nchini ziwe na uwiano ulio sawa kati ya wanawake na wanaume ili kutoa uongozi ulio bora.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa maji na wizi wa maji udhibiti ufanyike kwa kujenga miundombinu ya maji isiyochakaa. Vilevile Serikali iwachukulie hatua kali wale wote wanaohujumu miundombinu ya maji na wizi wa maji.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kuandaa bajeti hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa vijiji kumi kwa kila Wilaya wa Benki ya Dunia ulipokelewa kwa matumaini makubwa sana kwa wananchi. Pamoja na umaskini wao waliuza mazao na mifugo yao wakachangia fedha asilimia 20% iliyohitajika kama michango yao kwa mradi waliopewa. Asilimia hiyo 20 ya wananchi imekaa Benki na mpaka leo hawaoni maji na hawaelewi nini kinaendelea. Wanaendelea kuteseka kwa maji wakitumia muda wao wa kuzalisha shambani kwa ajili ya kufuata maji kilometa 8 - 10.

Mheshimiwa Spika, mradi huu umefeli, hakuna hata Wilaya moja ambayo imekamilisha hata vijiji vinne na hata visima vilivyochimbwa maji yakapatikana hayajasambazwa. Naomba Waziri aeleze Bunge visima ambayo maji yamepatikana na maji hayajasambazwa wala hakuna hata *pump* ya kuvuta maji wananchi wamebaki wanayaangalia tu, kwa nini maji haya hayanufaishi wananchi?

Wilaya ya Kaliua, kijiji cha Ushokola, maji yamepatikana kwenye kisima tangu mwaka 2011 hadi leo mkandarasi hakuwahi kurudi pale wananchi wakiuliza Halmashauri ya Wilaya hawana majibu wanayaangalia maji huku hayatumiki.

Mheshimiwa Spika, nini hatma ya vijiji tisa vya Kaliwa na Urambo ambavyo mtafiti alipima akasoma kuna maji, wachimbaji wakaja kuchimba wakakosa maji? Tangu mwaka

2011 walipoondoa vyombo vyao hadi leo hawakurudi na hakuna majibu yoyote yanayotolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni hatua gani zinachukuliwa kwa wakandarasi waliopewa *tender* ya kutafiti maeneo yenye maji, Urambo wakalipwa pesa zote na wachimbaji walipokuja wakakosa maji? Halmashauri ya Wilaya wametulia kimya na hata kwenye vikao hakuna anayezungumzia swala hilo. Serikali inatoa maagizo gani kwa Halmashauri ya Wilaya hiyo?

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumezungukwa na Bahari, tuna Mito, tuna Mabwawa, tuna Mabonde na tuna Misitu, Milima vyote hivi ni vyanzo vya maji. Kuna kila sababu sasa Serikali ikabuni mbinu za kutumia maji ya Bahari kwa ajili ya matumizi ya watu. Nchi nyingine tena zilizoko Jangwani mfano Namibia, Dubai wanatumia Bahari inayowazunguka kupata maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye utafiti kwenye nchi za wenzetu wajue mbinu za kuchuja, kuondoa chumvi na kuondoa/kuua wadudu kwenye maji ya Bahari ili yaweze kutumika ndani ya nchi kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe elimu kwa wananchi ili wavune maji ya mvua wakati wa mvua kwenye nyumba zao. Kutokana na wananchi kutojua umuhimu wa kuvuna maji hata wale wenye uwezo wa kuweka miundombinu ya kuvuna maji na wao pia wanategemea maji ya Bomba na Visima.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya maji ya bomba maeneo mengi imechakaa sana na hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha maji kupotea. Serikali iweke mpango wa kukarabati miundombinu kila baada ya muda fulani kutokana na uchakavu ili kuokoa maji yanayopotea chini huku wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia miundombinu ya maji machafu Mkoa wa Dar es Salaam, maeneo mengi yapo

hatarini, chemba ziko wazi, mifuniko hakuna, uchafu unatapakaa barabarani, magonjwa ya tumbo hayatapungua hata siku moja. Serikali inafumba macho huku wanaona yanayofanyika kule maeneo ya Kariakoo. Miaka ya nyuma zilijaa nyumba za kawaida za kuishi familia za kawaida na miundombinu ya maji machafu ilijengwa kwa kuangalia majengo yale. Leo zile nyumba zote zimebomolewa yamejengwa magorofa ya *floor* 10 – 16, miundombinu ya maji machafu bado ni ile ya zamani. Matokeo yake, hali ni mbaya sana, Halmashauri na Manispaa ya Ilala wanakusanya kodi ya soko kubwa la Kariakoo wala hawawazi kupanua miundombinu, ile mifereji imejaa vinyesi. Serikali ieleze Bunge nini kimepangwa kufanyika kuhusiana na miundombinu ya Kariakoo, Manzese na kwingineko?

MHE.ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo sugu sana katika nchi nzima na maji ndiyo uhai, hakuna shughuli inayoweza kufanyika bila maji kuhitajika. Tumekuwa tukishuhudia vifo vya Watanzania vinavyotokana na magonjwa yanayosababishwa na maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Mkoa wa Katavi, hali ngumu ipo vijijini. Mwaka jana katika Bunge la bajeti niliongelea suala la maji vijijini na kuvitaja vijiji ambavyo havina maji lakini Serikali hii wanayoita sikivu haisikii hata kidogo, shida ni ileile vijijini, wananchi wanateseka bila sababu yoyote na wapo karibu na Ziwa Tanganyika au Mto Ugala lakini Serikali imeshindwa hata kuvuta mabomba kutoa maji katika Ziwa au Mito iliyokaribu na vijiji ili wananchi waondokane na adha hii ya maji. Mpaka sasa wananchi wa vijiji vifuatavyo Ugala, Mbede, Chamalendi, Maji Moto, Iloba, Nkungwi, Kamsanga, Ngoma Lusambo, Ijenje na kadhalika wanaishi kwa kufukua kwa mikono ardhini kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa maji katika vijiji kumi katika kila Halmashauri. Mpango huu haujatekelezeka kwani hata katika hotuba ya Waziri wa Maji mwaka 2012 iliongelewa na vijiji vingi bado havina visima na wananchi wengi wanahangaika. Naiomba Serikali ielekeze macho vijijini kwa

kuwachimbia hata visima vifupi vyenye gharama ndogo kwani tatizo la maji haliko Katavi tu bali kuna maeneo mengi ambako wananchi wanakufa kwa magonjwa yanayotokana na maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara iwabane Wahandisi Wilayani kukagua miundombinu ya maji kama mabomba ambayo yanakuwa yamepasuka na kumwaga maji hovyo huku wengine hawayapati. Ni upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uboreshwaji wa miradi ya huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa mipya kama Mpanda, Mkoa mpya wa Katavi, kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ilivyoeleza ukurasa 52, tatizo hapa sio mipango na maelezo mazuri ya Serikali bali tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze wananchi wa Katavi miradi hii itakamilika lini? Maana muda ni mrefu umepita bila utendaji kazi kuonekana hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kuwa Mawaziri wanapofanya ziara za kikazi katika Wilaya au Mikoa wasiende kichama bali waende Kiserikali na kujionea wenyewe miradi inavyokwenda kuliko kuandaliwa Mezani taarifa huku wananchi wanakufa kwa adha ya maji salama.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na uzoefu mara nyingi juu ya mikataba ya uchimbaji visima na utafiti wa maeneo ya upatikanaji maji ambako kumepelekea kulitia hasara Taifa. Mfano ni mradi wa visima kumi (10) uliopo eneo la Kitunda ambao uliingizia Taifa zaidi ya hasara ya shilingi bilioni saba. Serikali haioni kwa sasa utafiti wa utafutaji maji uende sambamba na uchimbaji ili mkandarasi anayepewa kazi hiyo akabidhi visima ambavyo tayari vina uwezo wa kuzalisha maji? Mradi wa Kitunda ni visima viwili tu kati ya kumi ndivyo vyenye uwezo wa kutoa maji machache.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Kineng'ene uliopo Manispaa ya Lindi ambapo ulizinduliwa na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Aggrey Mwanri tarehe 27 Februari, 2012, Mheshimiwa Waziri hakukubaliana na mashine ya kusukuma maji iliyonunuliwa na Mkandarasi na kuagiza iundwe Kamati itakayofuatilia *BOQ* kuona ubora, lini na wapi imetoka mashine hiyo, mpaka leo Mkandarasi huyo ameikatalia Kamati hiyo kutoa namba ya injini ya mashine hiyo kwa madai kwamba ipo chini na imeshajengewa kwa zege.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mkandarasi huyo alitakiwa achimbe mtaro wa bomba wenye urefu wa *cm 100* lakini mpaka anaunganisha bomba urefu wa mitaro hiyo ni kati ya *cm 50* mpaka *cm 60*. Vilevile inaonekana hata ubora wa mabomba sio sahihi kwani wakati maji yanasukuma mabomba hayo yamepasuka hata katika maeneo ya viungio. Baya zaidi ni kuwa hata tenki alilojenga linavuja na taarifa nilizonazo ni kuwa anatafuta njia ya kuziba viraka maeneo yanayovuja haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili na wananchi wa Jimbo langu kuwa hatua gani zitachukuliwa dhidi ya ukaidi wa Mkandarasi huyo kwa kukataa kuonyesha *BOQ* za manunuzi ya mashine na vifaa hivyo ili kunusuru fedha nyingi zitolewazo na Serikali kutokana na kodi za wananchi.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa sana katika Vijiji vya Kongwa. Matatizo ni mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uwezo wa Mhandisi Wilaya na Idara ya Maji ni mdogo mno.

Pili, *Consultant A&O* na Wakandarasi, baadhi hawafai na miradi ni ya hela nyingi sana (ya *WB*) Kijiji kimoja kati ya Shilingi milioni 300 na Shilingi milioni 600. Tungekuwa na mamlaka katika Halmashauri ya Wilaya tungetumia wastani

wa si zaidi ya Shilingi milioni 100 kila Kijiji kwa *survey,* kuchimba tenki, pampu na mashine .

Mheshimiwa Naibu Spika, *Consultant* wa Halmashauri ya Wilaya zote Mkoa wa Dodoma ni *O&A* au *A&O* ni feki; hafai, hafai, hafai!

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Maji Vijijini kitaifa ni ndogo sana, hatukubali iongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, toeni madaraka makubwa kwa Halmashauri ya Wilaya Kongwa kuamua kiasi cha fedha cha kutumika kwa kila mradi kwa Kijiji ili tutumie hela tunazopata kwa Vijiji vingi zaidi badala ya hela kutumika na ma-*consultants* ambao hawana faida yoyote na Makandarasi feki.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili tu katika hoja hii kwa kujielekeza katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kutenga pesa kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 katika hotuba ya Waziri Ukurasa wa 52 na 53, kwa kuendeleza Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpanda. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umekuwepo mradi wa Halmashauri ya Mji, Mpanda wa maji wa lkolongo ambao hivi sasa unaendelea, pamoja na kwamba haujatengewa fedha Bajeti hii, isipokuwa, tayari Shilingi milioni 600 zimefika Mpanda kwa bajeti ya 2012/2013 na hazijatumika, na mwaka wa fedha unaishia 30 Juni, 2013. Kwa sababu tu Wizara haijatoa *letter of objection* ya kuridhia kusaini mikataba ya kutandika bomba kwa vijiji ambavyo Waziri amevitaja katika jedwali no 11, naomba sasa Wizara itoe hiyo *letter of objection* mapema na nitashukuru kama nitaarifiwa kama barua hiyo imetolewa au itakapotolewa ili kuharakisha kupunguza tatizo la maji Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni vyema sasa Wizara ikaweka kipaumbele katika kuvuna maji ya mvua kila inapowezekana kwa matumizi ya binadamu na mifugo, kwani akiba ya maji katika sura ya dunia inapungua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kubwa za kuwapelekea Watanzania huduma ya maji wakiwemo wananchi wa Singida, Manispaa ya Singida hususan Mjini kulikuwa na kero kubwa ya maji. Sasa maji yamepatikana kupitia mradi wa maji wa *World Bank* na *BADEA,* wananchi, hususan akina mama, wanafurahia matunda ya Serikali yao ya CCM. Ninawapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Profesa Maghembe - Waziri wa Maji, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuibua na kutekeleza mradi huu. Vile vile nawapongeza kwa kuandaa bajeti nzuri ingawa fedha ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kuieleza Serikali kuwa Jimbo hili lina upungufu mkubwa wa maji. Naamini Serikali inatambua tatizo ambalo limetokana na siasa, kwani miradi ya maji hutekelezwa kwa mpango shirikishi, wananchi huchangia fedha na kufungua akiba benki ndipo Serikali huchangia pamoja na wahisani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi walikatazwa kuchangia mradi wowote, naishauri Serikali kuacha tabia ya kuwatesa wananchi hususan wanawake na vijana wanaotembea mwendo mrefu kutafuta maji. Hivyo, ni lazima kauli ya Serikali itumike ili wananchi wakubaliane na Serikali, siyo mtu kwa maslahi yake. Nitashukuru kusikia kauli ya Serikali yetu yenye kuwajali watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili siyo dogo, kwani Vijiji na Kata ambazo zina tatizo la maji, vingi lazima Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuijulisha Serikali yangu kuwa inatakiwa kutoa kipaumbele kwa Jimbo hili la Iramba ya Mashariki kwani Vijiji na Kata, nyingi zina shida ya maji ili tusiwape Wapinzani nafasi. Naomba Serikai iombe taarifa ya tatizo la maji Wilaya mpya ya Mkalama ili nguvu kubwa ielekezwe huko. Vile vile tuwe na huruma kwa Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Salome Mwambu ambaye amekuwa na tatizo la kiafya muda mrefu. Nitashukuru endapo Waziri wakati wa majibu atasema kidogo kuhusu wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki wasikie, tafadhali. Mfano Matongo, ardhi ina mwamba, hivyo maji lazima yatoke Misenye. Vile vile Vijiji kumi tulivyopewa maji, yametobolewa na kupatikana lakini bado hakuna miundombinu ya kuunganishwa ili maji yaanze kupatikana Kata za Miganga, Nkalankala, Mwanga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Halmashauri ni kupatiwa fedha za Vijiji 30. Napenda kujua: Je, tumetengewa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiyopingika kuwa Dar es Salaam ndiyo Tanzania. Hivyo ni muhimu sana kuhakikisha ukarabati wa njia za maji unatiliwa mkazo, kwani hali ya maji Dar es Salaam siyo nzuri. Mfano mzuri ni Magomeni Mwembe Chai na Magomeni Kagera Mtaa wa Pongwe, wakazi wengi wamechimba chini ili wafungue njia za maji wapate maji, jambo ambalo ni kosa kubwa. Ili kuondoa adha hii ambayo pia imechangiwa na ujenzi wa barabara mpya, ni Jiji la Dar es salaam litengewe fedha za kutosha na usimamizi madhubuti. Haya maji ya kuchimba chini pia siyo salama, wananchi wataugua maradhi ya matumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuipongeza *DAWASA* kwa kazi zao nzuri za kusimamia miradi mikubwa ya maji na *DAWASCO* kwa kusambaza, hivyo watiwe moyo kwa kuongezwa fedha. Bila fedha, tutawalaumu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai. Bajeti ya Wizara hii ni ndogo hasa ukizingatia nchi yetu imeanza kunyemelewa na mabadiliko ya tabianchi. Vyanzo vingi vya maji vimeharibika, ukame upo hasa katika Mikoa ya Kanda ya Kaskazini, mito imekauka na hivyo hata visima vitakavyochimbwa vinaweza visitoe maji ya kutosha au baada ya muda mfupi vitakauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isimamie mkakati wa kukemea na kulinda mifumo ya maji iliyowekwa katika Halmashauri ya Wilaya. Mfano, mradi wa Vijiji 10 katika kila Wilaya, lakini na miradi mingine yote inayotokana na fedha ya Wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa Vijiji 10 ulianza tangu 2004 na hadi leo katika Halmashauri na Wilaya ya Moshi Vijijini ni Vijiji viwili tu umeanza kutekelezwa vya Kovi Kaskazini na Kiriu Kusini ambavyo vilitengewa Shilingi bilioni 1.02. Vijiji vingine vitatu vya Mawanjeni, Matala na Kilimo Makuyuni gharama yake ni Shilingi bilioni 2.3, bado na hata mkataba haujatiwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Vijiji vitano vitakuwa havijashughulikiwa, mfano Vijiji vya Machame Juu na Machame Chini vitakavyogharimu Shilingi milioni 704. Wananchi wa maeneo haya hawajawahi kupata maji ya bomba, siku zote wameendelea kunywa maji ya mifereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya tatizo la maji katika Kijiji cha Matala ni kubwa. Wanawake na watoto wanatembea zaidi ya kilometa tano kutafuta maji, wenye matrekta na bodaboda wana-*take advantage* ya tatizo, kiasi ndoo moja ya maji inauzwa Sh. 1,500/= fedha ambazo ni nyingi kwa mkulima wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika Vijiji vilivyo chini ya Mlima Kilimanjaro, mfano Kijiji cha Mwika Maring'a Chini

wanapata mgawo wa maji na mara mbili kwa wiki. Naiomba Serikali itekeleze mradi wa maji katika Vijiji vitatu vilivyobaki na hasa Kijiji cha Matala kuondoa adha ya ukosefu wa maji, gharama kubwa ya kununua maji na unyanyasaji wanaopata wanawake na watoto wanaotembea mwendo mrefu kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha iliyotengwa kwa Mfuko wa Maendeleo katika Halmashauri ya Moshi mwaka 2012/2013 ni Sh. 601,830,844/=. Mwaka 2013/2014 fedha hiyo imepungua kufikia Sh. 525,238,522/= kipindi ambacho Mkoa wa Kilimanjaro unakabiliwa kwa kiasi kikubwa na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itekeleze mradi katika miradi ya Vijiji tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza naanza kwa kutokuunga mkono hoja iliyo mbele yetu na ninazo sababu za kwanini siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika kutokuunga mkono hoja kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 51 inayoanzia na kichwa cha habari miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji inayozunguka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisiloingia akilini kuwa Wizara inaweza ikawa haifahamu Jiografia na kuwa na uhakika Ziwa Tanganyika linagusa Wilaya za Kigoma, Mponda Vijijini, Nkansi na Kalambo na siyo Wilaya wala Mji wa Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kalambo yenye Makao Makuu yake Matai ina Vijiji vifuatavyo ambavyo vinategemea maji ya Ziwa Tanganyika kwa kunywa na shughuli zote za kibinadamu; Kipwa, Kapele, Kapozwa, Kilewani, Kasanga, Muzi, Somazi, Kipanga, Katili na

Kantalamba, Vijiji hivi vyote vina matatizo makubwa sana ya maji na hivyo hukumbwa na kipindupindu kila kipindi cha mvua kutokana na kunywa maji machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi ni sababu zipi zilizosababisha Mji wa Kasulu kuingizwa katika mpango huu na kusababisha pesa nyingi kiasi hiki cha Dola za Marekani milioni 4.6 kutengewa Mji wa Kigoma Kasulu, dola za Marekani milioni 2.3, Mpande 3.1 na Namanyere 1.9 na kuachwa Wilaya ya Kalambo na Vijiji vyote huku ikiwa inapakana na nchi ya Zambia. Ni sababu zipi zilizosababisha Mji wa Kasulu kuingizwa kwenye huu mpango wakati hakuna eneo lolote la Wilaya hii inapitiwa na Ziwa Tanganyika? Au ni kuaminisha kwamba nafasi ya Kalambo kwa maana ya Matai na Vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika imeporwa na Wilaya ya Kasulu ambayo haina sifa yoyote kuwa inanufaika na mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na upendeleo wa dhahiri kwa miradi mingi inayotekelezwa mwambao mwa Ziwa Tanganyika kuelekeza pesa nyingi Mkoa wa Kigoma na kuona maeneo mengine ya Mkoa wa Rukwa kama Apandage suala ambalo ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara inapotoa majibu itoe ufafanuzi na kutenga pesa kwa Wilaya ya Kalambo, kwani ndiyo yenye kustahili na siyo Mji wa Kasulu.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Maji na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa kuendelea kutambua uwepo wa mradi wa maji ambao unatekelezwa katika Mji wa Ikwiriri Wilayani Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni lini mradi wa maji unaotekelezwa katika Mji wa Ikwiriri utakamilika? Kwa sababu umeahidiwa na uliahidiwa kukamilika mwaka 2010/2011, haukukamilika; mwaka 2011/2012, haukukamilika; na leo tena mwaka 2013/2014 hotuba inaonesha mradi umefikia asilimia 95%.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kijiji cha Ikwiriri wamechoshwa na ahadi za Serikali ambazo zinatolewa kila mwaka na mradi haukamiliki. Wananchi wa Ikwiriri wanaomba mradi wao ukamilike ili waweze kupata maji safi na salama kama Watanzania wengine wanavyopata huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za Serikali katika Wizara ya Maji hauoneshi kabisa dhamira ya Serikali hii ya CCM kutaka kuwapunguzia wananchi wa Tanzania hasa wanaoishi Vijiji adha ya kukosa maji safi na salama ambayo wameyakosa kwa miaka mitano tangu tupate uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007 Serikali ilipanga Shilingi bilioni 16.8 kwa Wizara na kufikia mwaka 2012/2013 Serikali ilitoa Shilingi bilioni 3.8. Hii inaonesha dhahiri kuwa Serikali hii haina nia ya kuwakomboa Watanzania kuwapatia maji safi na salama kwa kuendelea kutegemea pesa za Wahisani kama ambavyo *World Bank* wanavyoyumbisha utekelezaji wa miradi ya Vijiji kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama tujuavyo, maji ni uhai. Bila maji hakuna maisha. Vita Kuu ya Nne ya Dunia itatokana na kugombania maji. Maji yanahitajika katika kila kitu; binadamu, mifugo, kilimo, hata mpaka magari tunayoendesha lazima yawe na maji ili uweze kuliendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na kuwa na mlima wenye theluji ya kutosha, lakini wakazi wa Kilimanjaro hususan Moshi Vijijini kuna uhaba mkubwa wa maji. Miaka ya 1970 kulikuwa hakuna shida ya maji kabisa, wananchi wa *Old-Moshi*, Kibosho, *Uru, TPC,* Mabogini walikuwa na maji mengi yakitiririka kwa mifereji kutoka Mlima Kilimanjaro. Walilima kilimo cha ndizi na kahawa kwa umwagiliaji wa mifereji. Maji yalikuwa ni safi na salama, kulikuwa hakuna magonjwa. Je, Serikali imefanya utafiti

kuona tatizo ni nini? Sasa hivi wananchi wa Moshi Vijijini wanapata maji kidogo tena kwa mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Sheria ndogo za Halmashauri hazifuatwi? Kwa mfano, bado watu wanaharibu vyanzo vya maji, wanalima kando kando ya mito, wanakata miti, kutokuwepo na maji ni kupoteza nguvu kazi. Mfano, akina mama Kata ya Mbokomu na kwingineko wanatembea zaidi ya kilometa tatu kutafuta maji, watoto wanasitisha masomo, wanakwenda kukinga maji badala ya kufanya shughuli za maendeleo kwa maana wanapoteza muda mwingi kuchota maji, watoto wanafeli kwa kukosa masomo darasani. Kwa sasa hivi maeneo kanda za chini Moshi, maji ya Mto Kisasago/Mto Rau, yote yanaelekea kwenye mashamba ya watu na kuharibu mimea iliyopandwa mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa nini Serikali isijenge Bwawa kubwa kule chini Mandaka wakavuna maji hayo na yakatumika baadaye kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, kwa kuwa shule nyingi za Serikali hazina maji, Serikali ifanye jitihada Shule ziwe na *running woter* ili kuepukana na magonjwa ya milipuko kama kuharisha, *typhoid* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kila mtu aweze kuhifadhi maji, Serikali ipunguze kodi kwenye vifaa vya kuhifadhi maji kama matenki *(Simtank),* ni ghali sana. Siyo hilo tu, pia bei ya maji haitofautiani na bei za soda na *juice.* Kodi zipunguzwe, maji ya chupa yapatikane kwa bei nafuu, kila mtu aweze kununua. Hii itasaidia sana kuepuka magonjwa ya milipuko. Je, miradi ya maji kwa Vijiji kwa visima 10 kila Kijiji kwa Mkoa wa Kilimanjaro vimetelekezwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba zote za Bajeti 2005 – 2013 Serikali imekuwa inalieleza Bunge hili kuhusu miradi hii; ni lini Serikali itatenga fedha za ndani kwa ajili ya maji Vijijini? Hili ndilo tatizo la kutegemea wafadhali wa *Wold Bank*;

hawatoi fedha za maendeleo kwa wakati na wakitoa hawatoi zote.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Wizara ya Maji, nikijielekeza kwenye hoja nilizouliza mwaka 2012 kwenye Bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya maji katika Jimbo la Mnvomero ni kubwa. Naomba kujua hatua za utekelezaji Mradi wa Benki ya Dunia katika Vijiji vya Kipera, Mlali, Doma, Kwadoli, Hoza na Salawe. Baadhi ya Vijiji hivi, visima vilishachimbwa, lakini usambazaji mabomba bado. Naomba majibu, nini kilichokwamisha awamu ya pili ya utekelezaji? Je, lini Vijiji hivi wananchi watapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Kipara na Mlaki, Kigugu na Bumu tunaelezwa kutakuwa na miradi ya maji kutumia vyanzo vya mserereko. Je, miradi hii itatekelezwa lini? Kijiji cha Mlumbilo kinatajwa katika Mradi wa Benki ya Dunia, nataka kujua, ni lini wananchi wa Kijiji hiki watapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012 niliishauri Wizara ikanijibu inayafanyia kazi maombi ya maji Kata ya Huale, Hagali, Buduki, Mgeta Tchengema, Kikeo na Nyandina wapatiwe maji kupitia vyanzo vya mserereko. Kwanini Wizara haijapeleka wataalam Tarafa ya Mgeta kujionea vyanzo vya maji ya mserereko ili kutatua tatizo la maji safi na salama? Wizara inatoa tamko gani juu ya maombi haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Maskati na Kinda zina vyanzo vizuri vya maji ya mserereko. Naiomba Wizara itafute wataam ili wananchi wa maeneo haya wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia baraka tele Mheshimiwa Waziri wa Maji katika kuwasilisha na kupitisha bajeti yao leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Vijiji vya Luhagara, Mabuni, Litumbandyosi, Kingoli na vingine ni Kijiji cha Paradiso na Ndongozi, vipatiwe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *DED* ameniambia *DDCA* ina mitambo yake, ipo Mbinga sasa. Napendekeza tutumie nafasi hii, wakati mitambo hiyo inafika kwa shughuli hiyo maalum watuchimbie pia visima katika maeneo tuliyoongea na hayo mawili. Tukiwezeshwa kifedha, pia tutashukuru sana.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri, naomba kujua yafuatayo:-

(i) Ahadi ya kupeleka maji Kagongwa – Isaka (hadi Tinde na kadhalika), iliyotolewa na Mheshimiwa Rais tangu mwaka 2008 imefikia wapi katika utekelezaji?

(ii) Ahadi ya Serikali ya kuweka birika za maji ya mifugo *(Cattle troughs)* maeneo yaliyofikiwa na bomba kuu la Victoria – Kahama, imefikia hatua gani katika utekelezaji?

(iii) Kuna Mradi wa Ubia baina ya Serikali na Mgodi wa Bulyanhulu kupeleka maji Bulyankulu na Bugarama. Mgodi walishatoa fedha za utafiti *(feasibility study),* lakini Serikali haijatoa *commitment* yoyote. Kwanini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi unahitaji Shilingi bilioni 10. Mgodi uko tayari kutoa 50%, mbona Serikali iko kimya? Je, Serikali iko tayari kushiriki katika mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi wa mambo haya, naunga mkono hoja hii.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hutuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2013/2014. Maji ni uhai, hakuna asiyejua hilo, na kila kiumbe kinategemea maji. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye mikakati mizuri kwa Watanzania. Mipango hii ikitekelezwa kama ilivyopangwa.

Basi matatizo ya kutokupatikana kwa maji yanayolikabili Taifa hili yatapungua kama siyo kwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua umuhimu uliopo katika Sekta ya Maji, kwani maji ni uhai, viumbe vyote hutegemea maji; bila maji hakuna uhai. Upatikanaji wa maji hutegemea zaidi vyanzo vyake. Kutokana na hili, tusipokuwa waangalifu na kutunza mazingira na vyanzo vyetu vya maji, basi tatizo la upatikanaji wa maji halitakwisha na litakuwa endelevu. Hapa nazungumzia zaidi ukataji wa miti ovyo, kutotunza vyanzo vya maji. Ukataji huo wa miti husababisha ukame. Kwa maana hiyo, vyanzo vya maji, mito, maziwa hukauka, mifugo hufa na binadamu kukosa maji kutokana na kutotunza vyanzo vya maji na ukataji miti pembezoni mwa mito na maziwa husababisha mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kwa jitihada zake katika Sekta hii ya Maji kujitahidi na kuhakikisha kupatikana kwa maji safi na salama kwa wananchi wake ingawa changamoto ni nyingi na Serikali haina budi kuzifanyia kazi changamoto hizo. Tatizo la upatikanaji wa maji safi kwa nchi nzima limezidi kukua siku hadi siku, na tatizo hili hupelekea hasa wanawake kupata shida kwa kutembea umbali mrefu kufuata maji huku wakiwa wamebeba watoto mgongoni na hata kukaa kwa muda mrefu kwenye foleni kwa kusubiri maji. Hali hiyo imepelekea wananchi kutumia maji yasiyokuwa salama na hatarishi kwa afya zao. Kwa Mijini, wananchi wamekuwa wakikesha usiku kucha kwa kusubiri maji, kununua maji kwa bei ya juu sana na hali ya kipato chao ni kidogo. Hali hiyo imekuwa ikizidisha ugumu wa maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji imekuwa ikifanyika na kwisha, lakini baadhi ya Miradi hiyo huishia kutokutoa huduma yoyote kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huu mradi wa mabomba ya kichina ambayo yaliwekwa karibu sehemu nyingi Jijini Dar es Salaam, lakini mpaka leo mradi huo haujaanza kutoa huduma yoyote ya maji. Mradi huu ungeanza kusambaza maji kwa wananchi, basi ungepunguza sana adha ya maji waipatayo wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, kwanini mradi huu mpaka leo haujaanza kufanya kazi kwa mabomba yake kuanza kutoa maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni jambo la kusikitiksha sana pale Serikali inapojitahidi kutatua matatizo haya ya upatikanaji wa maji safi kwa kuanzisha miradi ya kuchimba visima, lakini watumishi wasiokuwa waadilifu huihujumu miradi hiyo na kuitia hasara Serikali. Nashauri watumishi kama hao kuchukuliwa hatua kali za kisheria, kusimamishwa kazi, kufikishwa Mahakamani; wakikutwa na hatia, adhabu kali itolewe juu yao.

Vilevile nashauri Wizara iweke utaratibu wa kuwapa elimu ya kutosha wananchi jinsi ya kuvuna maji yatokanayo na mvua. Hii itasaidia kwa zile sehemu ambazo bado tatizo la maji ni kubwa, ili wapate mbinu hizo za uvunaji wa maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini kilio chao kikubwa na cha muda mrefu katika Wizara hii ni upatikanaji wa maji safi na salama. Wananchi hawa wamekuwa wakipata shida ya upatikanaji wa maji safi, kwani baadhi ya Vijiji wamekuwa wekitegemea visima vya kuchimba na mkono ambavyo ni vifupi sana, kwa hali hiyo maji yake siyo salama, lakini wanatumia maji hayo hivyo hivyo, kwani hawana namna nyingine ya kuishi bila maji. Ingawa chanzo cha maji cha Mto Ruvu kiko kwao na wao ndio watunzaji wa mazingira ya chanzo hicho kwa manufaa ya Taifa, lakini leo hii wao ndio wahanga wakubwa wa maji. Kwani maji ya Mto Ruvu yanapita Mlandizi kwenda kutumiwa na watu wanaoishi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nimelizungumzia sana katika Mabunge yaliyopita kuwa kilio changu kwa Serikali kupitia Wizara hii, ni kuwapatia wananchi wa Kibaha Vijijini maji ili na wao waondokane na adha hii. Leo hii inashangaza kuona kwamba wananchi wa Kibaha Vijijini hawana maji wakati chanzo cha maji kimetoka kwao. Kiukweli inauma sana! Naomba Wizara husika iwaangalie wananchi hawa kwa jicho la huruma ili na wao waondokane na adha hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Miradi mingi inasuasua katika utekelezaji wake. Kwa mfano, Mradi wa Chalinze Magindu hadi Lukenge hadi sasa utekelezaji wake unasuasua. Pia na Mradi wa Ngeta ambao unatakiwa upeleke maji katika Vijiji vya Kikongo, Mwanabwito, Soga na Kipangege. Pia kuna tatizo la mda mrefu la upatikajanji wa maji Kata ya Boko Mnemela Vijiji vya Kata ya Boko, Kijiji cha pili na Kijiji cha Mkalambati na kadhalika; tunaomba maelezo ya miradi hii kwa Wizara husika na ikibidi utekelezaji wake uanze ili wananchi hawa waondokane na shida ya kutokupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mazuri siku zote huigwa na tusiwe wavivu wa kujifunza kutoka kwa wenzetu waliopiga hatua katika Sekta hii ya maji, ni jinsi gani wameweza kupambana na changamoto na kufanya wananchi wao kufurahia huduma hiyo na kupata maji pasipo shida.

Pia kuna matatizo katika Idara ya Usambazaji wa Maji, kwani inafika mahali maji hukatika pasipo taarifa yoyote zaidi ya kutoa taarifa kwenye vyombo vya habari, yaani Redio na Magazeti. Lakini siyo mara zote hufanya hivyo. Ikumbukwe kwamba siyo kila mtumiaji wa huduma hii ya maji ana nafasi ya kusikiliza redio ama kununua gazeti. Nashauri Serikali kupitia Wizara kuandaa utaratibu mzuri pale mitambo hii inapotakiwa kufanyiwa ukarabati, basi kutoa taarifa za tatizo la maji angalau siku tatu au nne kabla ya utekelezaji huo, ili kuwasaidia watumiaji wa huduma hiyo muhimu kujiandaa kwa kutunza maji na kuweka akiba ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuishauri Serikali kuzingatia na kutilia mkazo Sekta hii ya maji, kwani ni muhimu sana na itapunguza kero kwa wananchi kuilaumu Serikali yao kwa kuona miradi mingi, lakini maji yenyewe hawayaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji ndiyo huduma ya jamii mama kwa kila Mtanzania. Huduma ya maji safi na salama na hata kumhakikishia mwananchi uhai na kinga dhidi ya maradhi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Kibaha Mjini pamoja na kupakana na chanzo kikuu cha maji yatumikayo hadi Dar es Salaam, bado asilimia kubwa ya wananchi hawapati maji ya bomba. Aidha, Miradi ya Benki ya Dunia ya Vijiji kumi haijatoa matunda katika Jimbo hili, ukizingatia kuwa miamba ya ardhi ya Jimbo hili halihifadhi maji na yakipatikana ni machache na yana chumvi sana, hayafai kwa matumzi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mipya ya Benki ya Dunia ambayo Serikali imekuwa inaahidi wananchi wa Kibaha, inachukua muda mrefu sana, licha ya kuhakikishiwa kuwa sasa tayari fedha zipo katika Wizara husika na kwa sasa Mradi huu wa Bomba Kubwa la Kipenyo cha 85 sentimita. Kutoka Ruvu hadi Kimara litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mkanganyiko ya kuwa sasa wananchi wa Kibaha watahudumiwa na bomba jipya au yale ya zamani? Je, ni lini mradi huu utakamilika? Mheshimiwa Waziri alisema Pwani hatutaweza kuwa na mamlaka ya maji, maana hatuna chanzo, lakini tutapewa Uwakilishi kwenye Bodi, basi tunaomba sana Uwakilishi huu ukamilike na usiishie kuwa maneno tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni muda muafaka, Serikali itamke wazi: Ni lini mradi huu utakamilika na wananchi wa Kibaha wapata maji safi na salama na ya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli usiofichika kuwa tatizo la maji ni kwa nchi nzima licha ya Tanzania kuwa na mito, mabwawa na maziwa ya kutosha. Hii inaonyesha wazi kuwa bado Serikali haijaweza kutumia vyema rasilimali hii asilia tuliyopewa na Mungu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali kwa makusudi ijikite kwenye mpango maalum wa kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama. Kikubwa, Serikali ijikite katika mito, maziwa na hata mabwawa na sasa ikubali kwa makusudi kabisa uwekezaji binafsi au uwekezaji wa kushirikiana *(GPP)* ili huduma hii iweze kuwafikia wananchi kwa urahisi na kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba bajeti ya Wizara hii huwa inapunguzwa. Kwa hakika kama hatutawekeza kwenye maji kwa wananchi, hatutamkomboa Mtanzania kutoka katika umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri bajeti ya maji ipandishwe hadi kufikia angalau asilimia kumi ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali itamke rasmi kuwa ni lini sasa Mradi wa Maji Ruvu – Kimara kupitia Kibaha kwa ajili ya wananchi wa Kibaha utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia Wizara hii kwani maji ni uhai. Pia maji safi hupunguza maradhi na kupunguza wagonjwa wengi ambao huugua kwa kukosa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri aniambie kuhusu mpango wa maji katika Manispaa

ya Ilemela, kwani katika ukurasa wa 51 ameongelea miradi mipya katika eneo la Ziwa Victoria, lakini Manispaa ya Ilemela haipo kwenye Mradi huo. Nimeona Jiji la Mwanza, Manispaa ya Bukoba na Musoma, pia ya Lamadi, Misungwi na Magu. Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua nini hatma ya Manispaa ya Ilemela katika Mradi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kujua baada ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kugawanywa kuwa na Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela, ni chombo gani kinachosimamia Miradi ya Maji katika Manispaa ya Ilemela? Au kukosekana kwa chombo hicho, ndiyo kukosekana kwa Manispaa ya Ilemela katika Wilaya ya Ilemela kutoonekana kwenye Miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kabisa Waziri akafahamu Tawala za Wilaya hizi mbili sasa ni tofauti. Nyamagana (Jiji) na Ilemela ambao ni Manispaa kwa fungu la pamoja huleta utata. Mfano, Mfuko wa Barabara ambao huja pamoja. Ni vyema mkatambua Manispaa ya Ilemela kama ilivyo. Au sisi ni watunza maji taka tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Maendeleo *(Volume IV) Sub Vote 4001* kasma ndogo 3341, Mradi huu unaonekana umetengewa fedha nyingi sana, kwani tumeshuhudia miradi mingi hutengewa fedha kwa awamu, na huu kutengewa fedha nyingi sana. Au kwakuwa Mkuu wa Mradi huu ni Waziri; au ndiyo “chukua chako mapema”, au ndiyo mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake? Ni vyema fedha hizo zikapunguzwa na kupelekwa kwenye miradi mingine ambayo imekwama kwa ajili ya malipo, kama Mradi wa Geita, au Jiji la Mwanza kwa Miradi midogo ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuondokane na dhana ya mwenye kisu kikali ndio hula nyama. Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye kisu, hivyo ni busara akakubali kupunguza fedha hii

ili kurudisha heshima na kuondoa fikra zilizotujaa Wabunge ya kujipendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. RECHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Maji ni Uhai. Nina maana kuwa binadamu yeyote hawezi kuishi bila maji, na siyo maji tu, bali maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachonisikitisha, kama siyo kunishangaza, ni Bajeti ya Wizara ya Maji kuendelea kupungua mwaka hadi mwaka, kana kwamba maji siyo uhai, huku mahitaji yake nayo yakizidi kuongezeka. Kuna haja sasa ya Serikali kuongeza fedha katika Wizara hii ili iweze kwenda na ongezeko la mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu wa bajeti ya Wizara, napenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu sasa wa kutenga fedha kwa ajili ya Vijiji 100 vilivyoko ndani ya kilometa 12 kutoka bomba kuu la maji yanayotoka Ziwa Victoria. Pamoja na pongezi hizo, wananchi wa maeneo haya wangependa kuona sasa kazi hii inafanyika na kwisha kwa wakati kama hotuba ya Wazri ilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameainisha maeneo ambayo upembuzi yakinifu utafanyika, pamoja na mtaalam mshauri kwa ajili ya Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Bariadi, Mwanhuzi, Lagangabilili, Magu na Ngudu. Lakini sijaona Mradi wa Maji kwa ajili ya Mji wa Kishapu, Mhunze, Kolandoto, ambako kuna Hospitali kubwa, na sasa ni Hospitali teule ya Mkoa pamoja na Tinde Shinyanga Vijijini. Je, ni lini sasa maeneo haya yatapata maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria, ikizingatiwa kwamba maji tayari yameshafika Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Kahama?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi katika Mkoa wa Shinyaga na Simiyu yanapata mvua chache sana katika mwaka na hata zinapokuwa nyingi, hakuna sehemu ambapo kumechimbwa mabwawa ya kuhifadhia maji pindi mvua zinapokuwa nyingi. Naomba Serikali iangalie haja ya kuchimba mabwawa ya kuhifadhia maji ili yaweze kusaidia wananchi katika kipindi cha ukame, kwani akina mama hutembea mwendo mrefu sana kufuata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona kuna maeneo ambayo nimeyataja hapo juu yapewe kipaumbele na baadhi yanatekelezwa na mengine yatatekelezwa katika Mkoa wa Shinyanga. Basi Serikali ifanye kama ilivyoahidi ili wananchi wa maeneo haya wapate maji safi na salama na hii itaongeza watumiaji wa maji pamoja na kuongeza pato katika Mamlaka zote, yaani *KASHWASA* na *SHUWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la miundombinu mibovu katika maeneo mengi sana, hii inasababisha upotevu mkubwa sana wa maji yakiwa yanasafiri kwenda kwa mtumiaji. Pengine Serikali kupitia Wizara na hasa Mamlaka katika maeneo husika, wawe na utaratibu wa kufanya marekebisho au *replacement* ya miundombinu ili maji yasipotee njiani na hivyo kuepuka hasara zitakazopata Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi kwenye maji na hasa ya kunywa, Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa kodi katika maji ya chupa ili hata wanafunzi wanapokwenda shule waweze kununua maji ya chupa ambayo kimsingi ni safi na salama. Hii itapunguza magonjwa ya milipuko kama kipindupindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Shinyanga kuna tatizo kubwa sana ambalo limekithiri ambapo wizi wa mabomba kwa wateja umekuwa mkubwa sana, na hii inasababishwa na biashara ya vyuma chakavu. Kila siku takribani wateja 20 huibiwa vyuma hivyo na kuacha maji

yakitiririka hovyo Mtaani, hivyo kuiletea hasara Mamlaka ya Maji pamoja na mteja kununua bomba lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara, ione sasa kuna haja ya kubadilisha mfumo wa mabomba yanayounganishwa na Mita ili yatumike yale ya plastiki. Hii itapunguza wizi huu ambao kimsingi umetia hasara Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali iangalie na kulinda sehemu zenye vyanzo vya maji visiharibiwe ili viendelee kusaidia maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maji na Wizara yake kwa ujumla kwa hutuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kuchangia juu ya upatikanaji wa maji Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam una wakazi 4.5 - 5 milioni. Hawa ni watu wengi sana. Kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa kuna maji ya kutosha katika Jiji hili. Maji yanahitajika kwa matumizi ya viwanda, majumbani kwetu, mahospitalini na umwagiliaji. Kukosa maji ya kutosha ni kurudisha maendeleo ya nchi yetu nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam bado siyo zuri. Mpango au mkakati wa kuboresha upatikanaji wa maji Jiji Dar es Salaam ulioanza tangu mwaka 2012, umesaidia kwa kiwango kidogo, lakini bado tunaiomba Serikali kuongeza juhudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya maji ni mibovu na inapoteza maji mengi sana Mjini. Pia ukataji wa mabomba hovyo unachangia sana upotevu wa maji na kuongeza tatizo kuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ichunguze na idhibiti upotevu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru mkakati wa dharura wa kupata maji katika Jiji la Dar es Salaam, lakini nimependekeza Serikali ifikirie njia nyingine ya kupata maji kutoka baharini kama kutengeneza *desalination plant* ili maji ya bahari yatumike na kubaini kupunguza tatizo la maji Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji katika nchi yetu ni kubwa sana. Mkoa wa Kagera umepakana na Ziwa Victoria. Wilaya ya Karagwe ipo ndani ya Mkoa wa Kagera. Pia Wilaya ya Karagwe inavyo vyanzo vingi vya maji ikiwemo Ziwa Victoria, Mto Kagera, Ziwa Kajunju, Ziwa Burigi, Ziwa Ngoma, Ziwa Kaberenge, Ziwa Tanganyika, chemichemi nyingi sana zisizokauka kwa mwaka mzima ikiwemo Chisulo Kata ya Ihembe, Kabagendela Kijiji cha Ihembe I, Chitanga, Charuhanga nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na neema yote hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Wilaya ya Karagwe inapata maji chini ya asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji mkongwe wa kibiashara wa Omurushaka wenye wakazi wengi unapata maji asilimia sifuri. Mji huu unapakana na chanzo cha maji cha Charuhanga umbali usiozidi kilomita tano. Ajabu Mji huu hauna maji. Mji huu unapakana na Vitongoji vya Nyakahanga, Bugene, Kishao na Ihanda. Vitongoji vyote hivi vinapata maji asilimia sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Serikali imejitahidi, imeshapeleka umeme kwenye chanzo hiki. Pia imenunua mashine ya kusukuma maji, bado inahitaji fedha kwa ajili ya kutandaza mabomba (miundombinu) na kukarabati matanki ya zamani ili kupeleka maji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Mkurugenzi wa Maji. Pia nimepata ahadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Maji Ndugu Yohana kutupatia fedha kwa ajili ya mradi huu. Ni imani yangu kuwa ahadi ya Serikali ya kuwapatia wananchi maji wa Omurushaka, Nyakahanga, Kishao, Bugene na lhanda maji.

Ninaomba na kumsihi sana Mkurugenzi wa Maji Ndugu Yohana, aguswe ndani ya moyo wake, usumbufu ambao nimekuwa nikimpatia katika kipindi chote cha kufuatilia maji ya Omurushaka. Naamini hataniangusha, kwani ahadi hii ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Benki ya Dunia, utafiti uliofanywa na Mhandisi Mshauri, unaonyesha kuwa maji yalipatikana katika maeneo ya Vijiji vya Nyakakika na Kayungu katika Kata ya Nyakakika na Kata ya Nyakabanga Wilayani Karagwe, lakini hatuoni juhudi zozote za kusambaza maji haya kwa wananchi. Naomba nielezwe, kazi hii ya kupeleka maji katika vijiji hivi, itaanza na kukamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashuri kupendekeza kwamba maji ya Ziwa Victoria yawanufaishe wananchi wa Mkoa wa Kagera na hasa Wilaya ya Karagwe kama yalivyopelekwa katika Mkoa wa Shinyanga. Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ina jiografia ya milima na miinuko, jambo linaloifanya ikose maji bubujiko, naomba Serikali itenge fedha za kutosha kupeleka mradi kabambe wa maji kutoka katika vyanzo vingi vya maji vilivyopo Wilayani Karagwe. Serikali ianze japo kidogo kidogo na itenge fedha mwaka hadi mwaka mpaka mradi mzima ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Nile Basin upo katika nchi mbili za Rwanda na Tanzania. Kuna fununu kuwa mradi huu unakusudia kujenga mradi wa maji nchini Tanzania katika Wilaya ya Karagwe Kata ya Nyakabanga kwa ajili ya kusambaza maji Wilayani Karagwe. Mimi kama Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Karagwe, naomba

nieleweshwe kama jambo hili lipo au la. Kama lipo, litaanza lini?

Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkondo hoja;

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ludewa ni Mji unaokua kwa kasi na watu wanaongezeka kila siku. Je, Wizara ya Maji ina mpango gani wa kupeleka maji safi na salama na ya kutosha katika Mji wa Ludewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maji hajisikii vibaya kuona kwamba Makao Makuu ya Wilaya ya (Ludewa) hayana maji ya kutosha?

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi mchango wangu huu uzingatiwe katika jambo hili muhimu linalogusa maisha ya watu wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu katika Jiji la Dar es Salaam kumekuwa na tatizo lililopitiliza la upatikanaji wa maji. Hii tunaelewa kwamba moja ya sababu iliyopelekea hali hii ni ongezeko kubwa la mahitaji kutokana na idadi ya watu kuongezeka katika Jiji hilo. Pia suala la mfumo mbovu wa usambazaji wa maji unatokana na miundombinu iliyozidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linatokana na Serikali kutojiandaa katika muda uliostahili kukabiliana na tatizo hili. Hivyo, pamoja na jitihada zinazoonekana kuchukuliwa, sasa ni budi Serikali kuongeza msukumo wa makusudi ili suala la upatikanaji wa maji safi na salama lipatiwe ufumbuzi wa kudumu na kuwapunguzia wananchi shida kubwa wanayoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigependa pia kuifahamisha Serikali kuwa ule Mradi wa Maji maarufu wa Mchina katika maeneo ya Mbezi/Kimara ni kwanini utendaji wake unaonekana ni wa kusuasua?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa maeneo yale waliweka matumaini makubwa na Mradi huu, na mpaka sasa bado hawajafuta imani hiyo. Hivyo ni jukumu la Serikali kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili lengo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Wizara yako iangalie hujuma inayofanywa na baadhi ya wananchi wanaoweka pampu na kuhifadhi maji mengi katika matenki kwa ajili ya kufanya biashara, hali inayopelekea raia wengine kukosa huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali Serikali iwafuatilie watu hawa, kwani kisheria wanaruhusiwa kufanya biashara ya kusambaza maji ni *DAWASCO* peke yake na siyo mtu au Taasisi nyingine yoyote kwa sasa hivi. Hivyo jambo hili ni muhimu lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ina jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji nchini. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba uratibu huo unalenga kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zinafuatwa ili kuhakikisha visima vina ubora kwa matumizi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, jedwali Na. 8 katika ukurasa wa 118 wa kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Maji - Mheshimiwa J. A. Maghembe, kuna orodha ya maeneo yenye visima ambavyo maji yake hayakidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru kuna maeneo yenye visima ambavyo maji yake hayakidhi viwango kutokana na maji ya maeneo hayo kuwa na *Chloride* kiasi cha Mg/L (ppm) 5.0 - 41.7. Maeneo hayo ni Kikatiti, Sawaria, Malula, Oleriani, Oldonyosambu, Ngongongare, Mbuguni, Olkun'gwado, Nsengony Owiro, Kisimirichini kwa Ugoro, Kikuletwa Nkwanekoli, Makiba Migungani, Lemong'o, Engareolmotony.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, baada ya Wizara ya Maji kugundua kwamba maji ya maeneo hayo hapo juu hayakidhi viwango, ni hatua zipi zimechukuliwa na Wizara ili wananchi waishio katika maeneo hayo wasiendelee kutumia maji hayo ya visima na hivyo kuendelea kuathirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali kupitia Wizara hii ya Maji, ina mpango gani wa kuweka/kupeleka maji ya bomba kutoka Ngerenanyuki kwenda maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Uongozi wa Awamu ya Kwanza, chini ya uongozi wa Hayati Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Kambalage Nyerere, kulikuwepo na maji ya bomba kutokea Ngarenanyuki kupitia Kingori, Sakila hadi Kikatiti na Samaria. Katika kila Kijiji nilichotaja hapo juu, yaani Kingori, Sakila, Kikatiti na Samaria kulikuwepo na tenki la maji yaliyokuwa yanatokea Ngarenanyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa, matenki hayo ni matupu na hakuna maji yoyote yanayotoka Ngarenanyuki tena kuja katika matenki hayo. Ningependa kujua: Je, maji hayo yaliyotokea Ngarenanyuki kwa bomba, yalipatwa na nini? Wananchi waishio maeneo hayo wangependa kujua, maji yale ya bomba nini kilitokea kwamba sasa hayapatikani tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwapo na desturi ya Watendaji wa Serikali kutokuwa waadilifu katika kusimamia vizuri miradi ya maendeleo ya wananchi ikiwemo miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ichukue hatua kali za kinidhamu kwa wale wote wanaobainika kutumia kwa ubadhirifu fedha zilizolengwa kwa miradi ya maji. Wananchi wengi waishio Vijijini kwa miaka mingi wameteseka kwa kunywa maji yasiyo safi na salama, wao pamoja na mifugo yao.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kuwa maji ni uhai, bila maji hakuna maisha. Hivyo Wizara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji salama ni muhimu sana katika kupigana na umaskini na matatizo ya afya. Watu masikini ambao wengi wao huishi Vijijini, wana nafasi finyu ya kupata maji safi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya mazao na matumizi ya afya. Cha kusikitisha zaidi, mbali na maji salama, hata hayo ambayo siyo salama hayapatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kuna adhari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi lakini Tanzania bado ina vyanzo vya kutosha vya maji kukidhi mahitaji yake, tena maji yaliyo juu na chini ya ardhi, asilimia saba ya ardhi imefunikwa na maziwa ya maji matamu ambayo yako mpakani licha ya maziwa mengine ambayo yako ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Tanzania Mungu anatupenda, tuna maziwa makubwa, mito na mabwawa, lakini cha kusikitisha, hata wananchi wanaoishi karibu na vyanzo hivyo vya maji hawanufaiki na neema hiyo. Wana matatizo ya maji kama watu walio mbali na vyanzo hivyo. Mfano, Ziwa Victoria, japokuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha mikakati mbalimbali ambayo inabidi tuiombee Mungu itekelezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, *I am sorry to say this, but* nina mashaka makubwa kuwa Serikali imeshindwa kuwasaidia Watanzania kupata maji safi na salama. Miaka zaidi ya 50 ya Uhuru mpaka leo Watanzania wanateseka na maji. Hivi kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuwasaidia Watanzania kujikwamua na janga hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, katika sakata hili la maji wanaoteseka kupindukia ni wanawake na watoto. Wanawake wanateseka sana kwa kuchota maji mbali na watoto afya zao zinakuwa mbovu, hawaogi inavyotakiwa na wanakunywa maji machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitaje maeneo machache ambayo nimejionea mateso ya kukosa maji; mfano Igunga, kule ndiyo nilijionea maajabu. Wananchi wa kule, maji wanayotumia huwezi kuamini! Maji wanayokunywa binadamu ni hayo hayo, wanakunywa n'gombe, mbuzi, mpaka mbwa ni hayo hayo! Kwa kweli maisha yao ni magumu na ya ajabu sana. Unaweza kudhani hawako Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Pangani Mkoa wa Tanga kuna tatizo sugu la maji. Vijiji vyote vya Wilayani huko vina matatizo ya maji. Naomba vile ambavyo vinajitahidi kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji mnawasaidiaje? Kwa mfano, kuna Kijiji kimoja cha Mwera Kata ya Mwera Wilaya ya Pangani, Serikali hiyo ya Kijiji inajitahidi sana, wamechimba kisima kwa pesa za Kijiji na nguzu za wananchi kwa Shilingi milioni 10 walizokuwanazo kwenye akaunti. Sasa hivi wanahitaji mabomba ya kutoa maji hayo kwenye kisima na kuunganishwa kwenye laini kubwa inayopeleka maji kwenye tenki la maji lenye ukubwa wa milimita 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, nitakuja kuona ili Wizara yako iweze kuwaunga wanakijiji hawa ambao wako tayari kujitolea kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Spika, nianze kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, naishukuru sana Wizara ya Maji kwa kutekeleza mipango mbalimbali ya kuhakikisha upatikanaji wa maji safi kwa wananchi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naishukuru Wizara kwa kutenga kiasi cha shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa uboreshaji huduma za maji safi Muheza na pia kutenga fedha za Miradi mbalimbali ya maji katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Tanga

hasa Korogwe, Handeni, Mkungu (Kasera) na Lushoto. Huu utakuwa ni ukombozi kwa wanawake wa Wilaya hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji na maendeleo ya wanawake; suala la upatikanaji wa maji safi lina uhusiano wa karibu sana na suala zima la usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake hasa walio vijijini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa jukumu la kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani/familia ni jukumu la wanawake na wasichana. Katika maeneo mengi ya vijijini nchini, wanawake na watoto wamekuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa la kutafuta maji, mara nyingi wanatembea umbali mrefu kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona wanawake wakitembea mwendo mrefu tena wakiwa na watoto mgongoni, wanahangaika kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuwekeza fedha za kutosha katika kuboresha huduma za upatikanaji maji vijijini. Upatikanaji wa maji vijijini utachochea maendeleo ya elimu kwa watoto wa kike nchini. Hii itapelekea kuchochea maendeleo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji vijijini pia utachochea maendeleo ya wanawake kwani badala ya wanawake kupoteza muda mwingi kutafuta maji watatumia muda huo katika shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo, mifugo, biashara na pia kutumia muda huo kwa malezi ya watoto na familia.

Mheshimiwa Spika, kuwekeza katika uboreshaji wa huduma za maji vijijini kutasaidia kupunguza mimba kwa wasichana wadogo na pia vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake hasa vitendo vya kubakwa na kudhalilishwa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, tunao ushahidi wa kuwepo kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na ongezeko la mimba

kwa wasichana wadogo vijijini kutokana na tatizo hili la ukosefu wa maji vijijini. Hivyo, napenda kuishauri Serikali/ Wizara kuhakikisha mipango/mikakati iliyopo yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji hasa vijijini inatekelezwa ipasavyo. Huu ndio utakuwa ukombozi wa kweli wa wanawake Tanzania hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya kuvuna maji ya mvua; wakati sehemu nyingi za nchi zinakabiliwa na ukosefu wa maji safi, inasikitisha kuona kuwa maji mengi ya mvua yanamwagika na kupotea ovyo. Maji haya yanatakiwa kuhifadhiwa na kutumika wakati wa kiangazi. Hivyo, nitoe rai kwa Wizara kuandaa sera/mkakati mahususi wa kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu amesema katika kitabu chake kitukufu cha Qur-ani: “Tumeujaalia uhai wa kila kitu kutokana na maji.” Nini maana ya Aya hii? Ni kwamba, bila maji hakuna maisha, hakuna uhai, maisha hayawezekani na hapa ndipo tunapopata kipimo juu ya umuhimu wa maji..

Mheshimiwa Spika, kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya miradi ya maji na zaidi ucheleweshwaji wa kuzitoa hizo fedha kidogo ni kufanya mzaha na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali kulalamika juu ya hujuma ya miundombinu ya maji kwa sababu ya biashara ya chuma chakavu ni kukwepa majukumu. Serikali ina dola, ina mkono mrefu, je, kuna yeyote aliyetiwa nguvuni na dola au Serikali imelala? Au kuna ubia wa biashara hiyo kati ya watendaji wa Wizara na wabadhirifu hao wa miundombinu ya maji?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tena haiwezekani kuwe na hujuma za namna hiyo bila ya wahujumu kukamatwa. Bila shaka kuna namna hapo, Serikali itafakari upya isiwe nayo ni mlalamikaji baada ya kuwa ni mtatuzi wa matatizo haya!

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kuna tatizo sugu sana la watendaji au wasimamizi wa miradi ya maji hasa miradi ya visima ni walafi wa fedha za miradi hiyo. Wanafanya mchezo wa kuigiza kuwadanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji Jijini Dar es Salaam limeendelea kukua siku hadi siku. Ni jambo la aibu na kusikitisha sana Mji Mkuu wa nchi, Makao Makuu ya Serikali kuwa hakuna maji safi na salama. Pia majitaka ni tatizo linalokwenda sambamba na la maji safi Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Dar es Salaam wanategemea maji ya visima ambayo uhakika na usalama wake haujulikani. Biashara ya maji ya visima imeshamiri bila ya kuzingatia ubora wa maji yenyewe. Visima hivi vya maji Dar es Salaam vina uwezekano mkubwa wa maji yake kuchafuliwa na maji taka ambayo yanatiririka ovyo kila mahali. Hii ni aibu!

Mheshimiwa Spika, hali ya ukosefu wa majisafi hairidhishi hata kidogo, Serikali ni lazima sasa iwe na mkakati madhubuti wa kumaliza kero ya maji kwa Watanzania. Ni wakati sasa wa kutafuta fedha za ndani kwa mkakati maalum ili kuondoa tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, bila ya utashi maalum wa kisiasa juu ya tatizo la maji safi hata juhudi za kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano hazitofanikiwa; kwani maradhi mengi hasa ya watoto na akinamama yanasababishwa kwa asilimia kubwa na maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Spika, wakati haumsubiri mtu, Serikali iache sasa, iamue na ifanye kazi ya kuondoa kero za wananchi ikianzia hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya kumi na mbili (xii), ukurasa wa 51 tunaomba ufafanuzi wa miradi ya maji safi na usafi wa mazingira *Lake* Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, katika makadirio ya miundombinu ya mabwawa kumi (10), niliwaomba wataalam waongeze Bwawa la Nkoma, tafadhali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo:-

Je, mnaposema Miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji inayozunguka Ziwa Tanganyika, mnamaanisha nini? Kasulu mmeitengea milioni 2.3 na mpanda milioni 3.1. Hatuelewi ni kwa ajili ya kutandaza mtandao wa maji, yaani mabomba au ni uhifadhi wa mazingira? Tusaidie ufafanuzi tuna kiu kweli ya kuelewa.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi juu ya Mradi wa Maji Vijiji Vitano mwaka 2013/2014, vitakavyofadhiliwa na Benki ya Dunia. Vijiji vilivyo katika Jimbo la Mbogwe ni Lugunga, Iponya na Ilolangulu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ukurasa wa 175 na anifafanulie kila kijiji kinatengewa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani kwa ushirikiano.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nami kuchangia hoja ya Wizara ya Maji kama ilivyoletwa mbele yetu. Nianze kwa kuunga mkono Hotuba

ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara hii muhimu ya Maji. Hakika suala la maji ni muhimu kwa viumbe hai wote hapa nchini. Hakika bila maji hakuna uhai wa kiumbe chochote utakaowezekana na hakuna ustawi wa mji au jamii yoyote utakaokuwa na ufanisi mahali popote.

Mheshimiwa Spika, suala hili la maji katika Hotuba hii ya Bajeti, umepewa au umetolewa umuhimu mkubwa sana maeneo ya mjini na kuachwa maeneo ya vijijini ambako kuna uhaba mkubwa sana wa maji. Ni suala ambalo halina ubishi, hili linatokana na ukosefu mkubwa wa miundombinu. Hii inasikitisha sana. Hakika idadi kubwa sana ya wananchi wapo vijijini ambao sasa kwao kupata maji safi na salama imekuwa ni ndoto isiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nikitaja baadhi ya maeneo katika Kata ya Nemba ambako wakazi wengi ni wafugaji na wakulima. Hakuna mabwawa ya kunyweshea mifugo na matumizi ya kawaida ya binadamu. Maeneo mengi katika Kata hiyo, suala la kuoga limekuwa la anasa na hivyo kupelekea kuibuka kwa maradhi mbalimbali ya magonjwa ya ngozi, kama si kuomba Mungu yasiibuke magonjwa ya milipuko maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Nyamigogo kuna hali mbaya ya upatikanaji wa maji, bwawa lilipo halikidhi haja na bado ukarabati wake haukukidhi kiwango, sehemu nyingi wakati wa kiangazi ni matatizo makubwa sana. Shule za msingi Nyanshimba, Nyamigogo bado hazina utaratibu ambao angalau unaweza kumsaidia mtoto apate maji ya kuosha mikono pale anapotoka chooni kama kanuni za afya zinavyotuongoza.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa pamoja na juhudi za Halmashauri zetu, basi Serikali ione umuhimu wa maeneo hususani pale penye mikusanyiko mingi na kambi za watumishi mbalimbali ili wapatiwe huduma ya maji. Naiomba Serikali kutoa kipaumbele cha mgao au huduma ya usambazaji maji vijijini na kubwa zaidi maeneo ya pembezoni ambako huduma za jamii ni duni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuongelea suala la Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi (10). Miradi hii imetekelezwa kwa kiwango cha chini sana au bila mafanikio. Yapo maeneo ambayo visima vilichimbwa lakini maji haya hupatikana na bado imerukwa kwenye maeneo ambayo miradi imetekelezwa. Naomba nishauri Serikali kuwa Wakandarasi hawa walipwe mara baada ya kukamilisha mradi wote. Pesa zimelipwa lakini maji hakuna, hii ni dhambi kubwa sana kwa kuwadanganya na kuwatesa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, katika taarifa zinazoletwa hakika hatupati taarifa za ujumla za miradi mbalimbali ya maji inapotekelezwa katika maeneo yetu. Mfano Mradi wa *CONCERN* ambao umekuwa ukitekelezwa katika baadhi ya Kata mfano Kata ya Nyabusozi. Hakika maji ni uhai na maji ndio msingi wa maisha ya viumbe hai wote.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga shilingi bilioni 398.3 ambayo ni asilimia mbili (2%) ya Bajeti nzima ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali ingetuletea mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa pesa ya ndani inatengwa kiasi kikubwa zaidi kuliko kutegemea fedha ya wafadhili. Miradi mingi sana katika Halmashauri zetu inakuwa haitekelezeki kwa wakati kwa sababu ya kutegemea pesa ya wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Wizara hii kwa matatizo makubwa ya maji katika miji na vijiji vingi vya nchi hii, Serikali ingetenga pesa nyingi zaidi za ndani kuliko za nje ili kuwa na uhakika kwa miradi ambayo imeainishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iweke utaratibu mzuri wa kusimamia miradi hii ya wafadhili. Wahandisi wengi katika Halmashauri zetu sio waaminifu kuanzia kwenye upembuzi yakinifu, kwenye uchimbaji wa visima na kumekuwa na udanganyifu mkubwa. Hata tenda zinatolewa kwa kujuana mpaka kusababisha miradi mingi kujengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono na nikubaliane na Wabunge wenzangu walioona umuhimu wa hii Wizara kuwa na Mfuko wa Maji kama ilivyo Wizara ya Ujenzi kuwa na Mfuko wa Barabara. Kuwepo kwa Mfuko huu kutasaidia ujenzi wa miradi mingi kufanyika na pesa kupelekwa kwa wakati kwa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipita katika maeneo mengi na kutoa ahadi nyingi za maji ningependa kujua utekelezaji wake ukoje? Maana nimesikiliza michango mbalimbali ya Wabunge, pia maswali ya kila siku inaonesha ahadi nyingi bado hazijatekelezeka. Ni vyema Wizara ingetambua idadi ya ahadi za Mheshimiwa Rais na zijulikane idadi ya ahadi zilitekelezwa na zile ambazo hazijatekelezwa na Serikali ingeeleza mkakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwenye Wilaya yangu ya Korogwe Vijijini kuna kisima cha maji Mombo mwisho wa shamba, Serikali ilisema kabla ya mwezi wa Sita maji yawe yametoka na kwenye mpango wa maji hakuna chochote.

Mheshimiwa Spika, kwenye Vijiji Kumi (10) vya udhamini wa Benki ya Dunia ni Mradi mmoja tu wa Makumba, mingine yote haijaanza. Sasa naomba Serikali iseme hivi Vijiji vingine vya Mashewa, Kwashemshi, Mmyuzi, Nugiri, Mwenga, Mlembule, Hale, Kwamkole na Changalikwa, Miradi hiyo ya Benki ya Dunia itaanza lini na wananchi wanalalamika. Naomba Serikali iangalie suala hilo kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi nichangie Bajeti ya Wizara ya Maji kama nilivyomalizia ushauri wangu wakati nikichangia Bajeti ya Ofisi

ya Waziri Mkuu, maji ni uhai. Hoja hapa ni kuwa kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu, tunapaswa kuisimamia kwa makini.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Wizara hii imeshindwa kukidhi matakwa ya hoja hiyo hapo juu. Kiasi kinachotengwa hakiwezi kukidhi mahitaji ya Miradi iliyoanishwa. Mbali na miradi iliyoanishwa kwa mwaka ujao vipo viporo ambavyo haieleweki ni kwa vipi vitaweza kukamilishwa. Kitendawili tata katika sekta hii ni hata hiyo miradi inapochaguliwa na kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mfano lile Jimbo langu ambayo yana shida kubwa sana ya maji hayajawahi kufikiriwa, acha kupangwa. Katika eneo hilo hilo kuna maeneo yenye afadhali, yaani wanaweza kupata maji kwa wastani wa mita 800, wamepewa hiyo miradi ya ahadi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maelekezo hayo hapo juu nielezee tatizo la utekelezaji wa miradi. Mfumo wa sasa ambapo Halmashauri za Wilaya hutumika kama msimamiaji na mtekelezaji wa Mradi imekuwa na upungufu au udhaifu mkubwa sana. Miradi imekuwa na ucheleweshaji, utendaji usiokuwa na ubora, ugawaji wa miradi bila kuzingatia utaalam na ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo, sekta ya maji hasa vijijini kusikokuwa na Mamlaka nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa haraka kadri iwezekanavyo miradi ya maji isimamiwe na timu maalum katika ngazi ya Mkoa. Timu hii isiwajibike kwa Mabaraza ya Madiwani, iongozwe na utaalam kwa kulenga mahitaji. Hii ni njia au suluhu ya muda, mpango wa kati na baadaye ni kuanzisha *TANWATER* kama ilivyo *TANROAD* ambayo itakuwa na watendaji, ngazi ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu wa *TANWATER* itakuwa rahisi na haraka kupunguza kama si kumaliza tatizo la maji nchini. Chini ya utaratibu huu tozo mbalimbali

zinaweza kuanzishwa chini ya Mfuko wa Maji wa 2009 na kutumiwa kujenga mifumo ya maji. Tukiwa na chombo hiki kwa pamoja kama Taifa tunaweza kuandaa nguvu kazi watu ili kuweza kumudu shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya *TANROAD* pamoja na mambo mengine yanachangiwa na nidhamu ya watendaji hasa Waandisi na Kada zote za kifundi kuwajibika kwa mamlaka moja. Hoja hapa ni kuanzisha mamlaka ambayo itakusanya rasilimali (chini ya Mfuko wa Maji) na kusimamia rasilimali watu kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, chini ya upungufu niliyoyaeleza hapo juu niwasilishe kwa Serikali kilio cha wananchi wa Jimbo langu wenye shida ya maji kupindukia. Kata ya Rutoro vijiji vyote vinne vinashida ya maji kupindukia. Kata ya Ngenge, Vijiji vya Kishuko, Ngenge na Kuzigembe matatizo yao ya maji ni kama maeneo aliyoyaelezea Mheshimiwa Ole Sendeka.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Omulanazi, Kata ya Mashabago mfumo wa maji uliofungwa umeshindwa kufanya kazi. Suluhisho mojawapo la mfumo huo ni kuweka pampu inayoendeshwa na mfumo juu (*Solar Energy*). Kipato cha watu wa sehemu ile hakiwawezeshi kumudu gharama ya kununua *Diesel* kila watumiapo mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwakilishe kupitia Bajeti ombi langu la kila mara juu ya Mradi wa Maji katika Mji Mdogo wa Kamachumu. Mfumo wa maji uliojengwa mwaka 1958 sasa umeshindwa kukidhi mahitaji ya wananchi. Watu wameongezeka sambamba na ongezeko la shughuli za kibinadamu zinazohitaji maji mengi na ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa eneo la Kamachumu chini ya uongozi wangu na Halmashauri ya Wilaya wameanzisha Mradi wa kuboresha mfumo huu kwa kupanga kutumia chemchemi za Kalinga. Mradi huu ukifanikiwa Vijiji vya Bulembo, Bunywambele, Kanoni, Bushangara, Irogelo na Kafunyo vitanufaika. Mafanikio haya

gharama yake ni ndogo kuliko gharama ya miradi mingine ambayo huduma yake kwa wananchi ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. RAMO MAKANI: Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji. Nianze na matumizi ya wataalam hasa Wahandisi Washauri; Serikali itumie kanzidata iliyopo Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(ERB)* ili iajiri na kuwatumia wataalam hawa wenye sifa na uzoefu katika *research*, *planning, design* na kadhalika. Hali ilivyo sasa ni hatari na gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya ambazo ndizo watekelezaji wa miradi katika ngazi ya ujenzi (*construction*) na matunzo/matengenezo (*maintenance*) ziwezeshwe kuwa na Wahandisi wa Maji, Mafundi Sanifu na Mafundi Sadifu wa kutosha kwa idadi na utaalam (ujuzi). Pale ambapo haitoshi, *resource sharing* itumike miongoni mwa Halmashauri.

2. Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya maji Tunduru; Tunduru Mjini, Mamlaka ya Maji Mji wa Tunduru ilianzishwa na kukabidhiwa mtandao wa maji chakavu (*almost* uliokufa) na kwa hiyo kushindwa kuanza kazi kwa kukosa mtaji (*initial lost*).

Mheshimiwa Spika,Halmashauri hii haina fedha na haiwezi kujiendesha kutokana na kukosa mapato kutokana na tozo ya huduma ya maji, maana hayapo, hivyo hakuna wateja wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mamlaka ya Maji, Tunduru ikamilishwe kimuundo, watumishi, ofisi, vifaa na Bajeti ili ianze kazi *seriously* mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maji Vijijini; hali ya upatikanaji wa maji vijijini Wilayani Tunduru ni taabani. Takwimu zinaonesha idadi ya vijijini vyenye hali mbaya,

kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kukosekana kwa *maintenance culture*.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itembelee Tunduru kujionea na kuchukua hatua.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 iliwaeleza wananchi kuwa ifikapo 2015 maji safi na salama yatakuwa yamewafikia wananchi kwa asilimia themanini (80%), suala ambalo limekuwa kitendawili. Pia Sera ya Maji ya mwaka 2012 ililenga katika kuhakikisha kuwa, wananchi vijijini wanapata maji safi na salama. Umbali usiozidi mita 400, kutoka kwenye makazi yao. Jambo ambalo ni gumu sana kutokea hata miaka ishirini (20) ijayo kama hakutafanyika mikakati ya makusudi.

Mheshimiwa Spika, mpaka Disemba, 2012 ndio kwanza waliopata maji ni milioni 20.6 ambayo haijafika hata asilimia hamsini. Je, mamilioni ya watu waliobaki watafikiwa lini ili nao wapate maji safi na salama? Hii inakatisha tamaa, shida kubwa ni kutokuwa na vipaumbele na vikatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji; mikakati ya kuhifadhi vyanzo muhimu vya maji zoezi hili limekuwa halitekelezwi ipasavyo. Katika Wilaya yangu ya Missenyi vyanzo vingi vya maji vimeharibiwa na hao wanaojulikana kama wahifadhi, maana vyanzo vyetu vilitengwa na simenti, hivyo vimeziba chemchemi zetu na matokeo vimekauka hasa na ukweli walijenga chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingi vya maji vya wilaya ya Missenyi ni vya asili, kinachohitajika ni kuvisafisha na kuviacha kama vilivyo maana kuvijengea kunaziba chemchemi na hivyo vinakauka kabisa na kusababisha usumbufu kwa kuwa vimebomoka na kuziba chemchemi.

Mheshimiwa Spika, suala la Vijiji Kumi kupata maji kila Wilaya kweli hilo linaweza kuleta tija ya kufikia wananchi wa Tanzania kwa asilimia themanini (80%) ifikapo 2015? Jambo hili sidhani kama linawezekana ukizingatia vijiji ni vingi sana, Missenyi tu kuna vijiji 74, na Serikali imeviwezesha vijiji kumi, hii siyo hata robo. Je, Serikali inaweza kunieleza mpaka kufikia 2015 vijiji vingapi vitafikiwa katika kupata maji salama?

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto za visima kumi (10) kila Wilaya; vijiji kumi vya kila Wilaya vimekuwa na changamoto nyingi.

(a) Watafiti walifanya mchakato na mwisho wakatoa majibu sehemu za kuchimba maji, lakini wachimbaji hawakupata maji katika maeneo mengi.

(b) Sehemu nyingi hawajaanza kuchimba kwa sababu ya maelezo ya tofauti yaliyopelekwa Wilayani, kusema kuwa maji hayawezi kuchimbwa mpaka hiyo asilimia itimie, sehemu nyingi wameambiwa asilimia ishirini (20%) ya fedha za mradi, kitu ambacho siyo sahihi, matokeo yake miradi imesimama.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutusaidia kujua taratibu zipi zifuatwe ili wananchi wachimbiwe maji safi na salama. Kama tulivyo waahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi wa CCM.

Mheshimiwa Spika, je, kwa wale waliochimba na maji yakakosekana, nani atafidia hasara, au ndio hasara kwa Serikali ukizingatia pia kuwa jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji ni duni, na Mheshimiwa Waziri amesema utaratibu huo unalenga kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zinafuatwa ili kuhakikisha visima vina ubora na matumizi endelevu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwapa makapuni 131 kuchimba visima na vikachimbwa visima 420, hakutwambia vingapi vimetoa maji na vingapi havikutoa maji na kama havikutoa maji hasara ya nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria; awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira Ziwa Victoria ilianza 2009, nchi husika ni Tanzania, Kenya na Uganda. Madhumuni ya Mradi huu ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za bonde la Ziwa Victoria kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika ziwa hilo. Kwa upande wa Tanzania, Mradi unalenga kuimarisha Taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo uharibifu mkubwa wa mazingira, kuvua samaki hata wasiofaa kuvuliwa na ukizingatia kuwa utaratibu wa kuachia uvuvi wa muda ili samaki wazaliane na wakue, ili kuzuia samaki wadogo na hivyo kufaidika kuvua samaki wenye kilo 29 kutosha na hivyo kupata fedha za kutosha, lakini zoezi hili limekuwa halifanyiki kwa nchi nyingine, Tanzania ikifunga uvuvi Uganda na Kenya wanaendelea kuvua.

Mheshimiwa Spika, kama Tanzania ndio imepewa kazi ya kuimarisha Taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki, Wizara inatueleza nini kuhusu kuweka mkakati wa kulinda ziwa hilo wakati wa zuio la kuvua ili kila nchi isivue wakati wa zuio na ikivua iwekwe faini au adhabu kubwa ili kukomesha uvunaji samaki kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chanzo cha maji cha Mto Kagera na Mto Ngono; Mto Kagera na Mto Ngono (Nkenge) ni mito ambayo inaweza kutoa maji ya kutosha na kumwagilia na hata kuzalisha mpunga kupitia mabonde ya mito hiyo na hivyo kuongeza kipato cha Wanamissenyi na kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuwapa maji ya mito hii kwa matumizi ya nyumbani yaliyo safi na salama ukizingatia Missenyi ni Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kilio cha maji licha ya kuwa ni cha nchi nzima, naomba kuweka mbele yako kilio cha watu wa Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mradi wa visima kumi (10) hadi sasa haujazaa matunda. Ni mambo manne (4) tu ambayo yameonesha dalili za kuwepo maji. Halmashauri inaomba fedha ambazo zimetengwa kwa ajili hiyo zitumike kwa ajili ya kujenga malambo kwa kukinga maji katika mito ya msimu.

Mheshimiwa Spika, ombi la kupatiwa malambo lilitolewa pia kwa Mheshimiwa Rais wakati akizindua barabara Jimboni. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba kabla ya kumaliza kipindi chake cha uongozi atatupatia malambo mawili. Wananchi wanasubiri kwa hamu utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pili, katika Bajeti ya mwaka huu unaomalizika, tuliomba maji ya Ziwa Chala yatumike kwa ajili ya wananchi. Jibu la Serikali lilikuwa kwamba, Mamlaka ya Bonde la Pangani inachunguza kama maji hayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu. Pamoja na kwamba majibu hayajapatikana, lakini wenzetu wa Kenya na Lake Chala *Safari Lodge* wanayatumia. Jambo hili linawapa wananchi hasira dhidi ya Serikali yao. Tunaomba mradi wa kusukuma maji hayo ili yawafae wananchi hasa wa ukanda wa chini ambao shida ya maji ni kubwa sana kwao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kampuni ya Maji *Kilwater* imethibitisha kwamba, imeshindwa kuwapa wananchi huduma ya maji kutokana na kushindwa kugawa maji kidogo yaliyopo kwa haki na kutawaliwa na rushwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Rombo tunaiomba Serikali kuivunja Kampuni hiyo na badala yake kuanzisha Kampuni nyingine au mamlaka ya maji ambayo itabuni vyanzo vipya na kusambaza maji kidogo yaliyopo kwa haki.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, maji ni muhimu na Bajeti tuliyonayo ni ndogo. Naomba Serikali izingatie maoni ya Kamati kwa kuiongezea Wizara hii fedha kiasi cha shilingi bilioni 185 ili kuweza kufikisha maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, imepata pesa kidogo ikilinganishwa na pesa zilizopitishwa na Bunge letu. Naiomba Serikali kuhakikisha katika Bajeti ya mwaka huu ziende kama ilivyokusudiwa ili kutekeleza miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, akinamama ni waathirika wakubwa sana wa tatizo la maji. Naiomba Serikali iupe mradi wa maji kipaumbele ili akinamama waondokane na adha hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kwa Vijiji Kumi (10) kwa kila Halmashauri nchini umekuwa wa kusuasua bila mafanikio toka ulipoanza mwaka 2003. Wananchi kwa upande wao wamefanikiwa kuchangia kiasi walichopaswa kuchangia kwa kila kijiji nchini. Hata hivyo haya yote yanatokea kwa kuwa Bajeti zetu zimebaki kutegemea wafadhili ili miradi itekelezwe. Hili ni hatari sana kwa Taifa na hasa kwa suala muhimu kama hili la maji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipunguze matumizi mengine na kuelekeza fedha nyingi katika miradi ya maendeleo. Hata hivyo, udhibiti wa mianya ya rushwa, ufisadi ni muhimu sana ili fedha zielekee katika miradi ya maendeleo. Serikali kwa kusimamiwa na Bunge inapaswa kufanya tathmini ya kina kwa Mradi huu wa Vijiji Kumi kabla ya kuanza kwa *programme* hii kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa maji taka; kulingana na ongezeko la watu nchini ndivyo ambavyo kuna ongezeko la maji taka katika miji mikubwa na miji inayokua hapa nchini. Tumeshuhudia katika miji mikubwa wakati mvua kubwa zikinyesha hapa nchini, maji taka nayo hutiririka na

kusababisha magonjwa ya milipuko na kuathiri nguvu kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuzisimamia Mamlaka za Maji Mijini kuweka miundombinu bora na ya uhakika itakayoweza kupitisha maji taka bila kuleta athari kwa jamii. Hata hivyo, elimu kwa wananchi inahitajika zaidi ili uelewa wa masuala ya maji taka na athari zake ueleweke kwa ufasaha.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba tatizo la maji ni kubwa sana karibu nchi yote. Katika Jimbo la Nyang'hwale napenda kusema Jimbo hili lina matatizo sana kwa upatikanaji wa maji safi na salama karibu Kata zote kama Bukwimba, Izunya, Kafita, Kharumwa, Nyugwa, Kakora, Shabakaba, Busolwa, Nyang'hwale, Nyijundu, Nyaburanda, Mwingiro.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la maji limesababisha baadhi ya mambo kama mimba kwa wasichana, kuvunjika kwa ndoa nyingi, akinamama kuota vipara, akinamama kutopata mapumziko vizuri, maradhi mbalimbali yatokanayo na kunywa maji ambayo si safi na salama, vituo vya afya na zahanati kutofanyiwa usafi wa uhakika na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupoteza vipindi vingi vya masomo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kupambana na tatizo la maji Jimbo la Nyang'hwale na kutuchimbia visima katika baadhi ya vijiji kama Nyalubere, Kitongo, Izunya, Kayenze, Ikangala, Kakora, Kharumwa, Bukwimba na Nyamtukuza. Visima vyote nane havitoi maji, kisima kimoja cha Kijiji cha Kharumwa hakijafungwa pampu zaidi ya miezi 18 tangu kichimbwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri wangu kuwa, zitengwe pesa zaidi ili kufufua mtandao wa maji uliopo Ziwani Nyamtukuza ambao ulisimama kutoa maji tangu 1975. Mtandao huo ulikuwa ukisambaza maji katika Vijiji vya Nyamtukuza, Kakora, Nyarubere, Kitongo, Ikangala,

Kharumwa, Izunya, Kayenze na Bukwimba, mtandao huo sasa ufufuliwe ili kupanua zaidi usambazaji wa maji katika Kata zote na vijiji vyote vya Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za maji katika Wilaya ya Nyang'hwale kiasi cha sh. 316,590,593/= kwa mwaka wa 2013/2014. Pesa hizi ni kidogo sana ukizingatia uhitaji wa maji Jimboni Nyang'hwale, naomba pesa zaidi ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali ijenge matenki ya kuvunia maji ya mvua kwenye mashule yote ya sekondari, shule za msingi, zahanati, vituo vya afya na vituo vya Polisi ili kupunguza tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii mpaka Serikali iongeze Bajeti ya maji katika Jimbo la Nyang'hwale.

MHE. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kuhusu hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kero ya maji ni kwa nchi nzima, hivyo napenda kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, utunzaji wa vyanzo vya maji; Serikali ihakikishe kuwa vyanzo vya maji vinatunzwa kwa gharama yoyote ile.

Pili, kuchukua hatua kali kwa wale wote wanaoharibu mazingira na vyanzo hovyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri afike katika bonde la Eyasi na kuangalia uharibifu wa chanzo cha Qanded, chanzo ambacho hutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Pia Serikali iboreshe skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji wa maji; Serikali iwekeze katika kutengeneza miundombinu ya uvunaji wa maji hasa katika Taasisi zote kwa shule zote za msingi/sekondari na kadhalika na kutengeneza mabwawa kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Serikali kuhusu mpango wa maji wa vijiji kumi (10) kwa Halmashauri zote. Mpango huu unasuasua sana katika Halmashauri yangu ya Karatu, kati ya vijiji kumi, vijiji nane (8) maji yalipatikana, lakini changamoto kubwa ni umeme. Nashauri Serikali iangalie mpango wa matumizi ya nishati ya umeme wa jua (*solar*) na upepo ili kuweza kupampu maji hayo.

Mheshimiwa Spika, kero ya maji katika Mji wa Karatu ni kubwa sana. Tarehe 18 Machi, 2013 Mheshimiwa Waziri wa maji Mheshimiwa Profesa Maghembe alifika Karatu na kutoa ufumbuzi wa dharura kwa wananchi wa Karatu. Mheshimiwa Profesa aliagiza kuwa ndani ya siku kumi (10) tayari Serikali itakuwa imeweka *pump* ya kuvuta maji na kuchimba visima viwili mpaka sasa hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kama kauli ile ilikuwa ni ya kufurahisha wananchi wa Karatu tu au anamaanisha kweli na lini kazi hiyo itaanza?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, maji ni muhimu sana katika Uhai wa mwanadamu. Tunaiomba sana Serikali hii iongeze bajeti ya Wizara hii kwani vijijini kuna matatizo makubwa sana ya maji. Kama Serikali haitawekeza kuongeza fedha hasa kwa wananchi wa vijijini nchi haitakuwa na maendeleo. Mradi wa vijiji kumi umeshindwa kabisa kukidhi mahitaji ya wananchi, ni vyema tukawa na mipango ya muda mfupi ya kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kuna Vijiji vya Ngomalusambo, Igagala, Kabungu, Kamsanga, Ifukutwa, Majalila, Vikonge, Katuma, Kasekese, Kabage, Sibwesa, Kapalamsenga, Isenga na Tarafa ya Mwese, kuna matatizo makubwa sana ya maji. Naiomba Serikali ipeleke huduma hiyo muhimu ya maji katika vijiji hivyo, tukipeleka huduma ya maji tutakuwa tumewasaidia wananchi na kukuza uchumi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kama miradi hii itatekelezwa katika vijiji nilivyovitaja hapo juu.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ukurasa wa 85, kuna maelezo kwamba, miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi zaidi imeendelea kujengwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi (10) kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika kitabu hicho hicho cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, jedwali Na. 11 kuhusu mpango wa kutekeleza vijiji 10 kwa kila Halmashauri, ukurasa wa 130, vijiji vitano (5) vilivyopewa kipaumbele katika Halmashauri ya Meru na vinavyotekelezwa kwa mwaka 2012/ 2013, ni Kasanumba, Kikuletwa, Mbunguni, kwa Ugoro na Ambureni Moivaro".

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua, je, ni kwa kiwango gani mradi huo umetekelezwa katika vijiji hivyo? Je, kazi ya mradi huo imemalizika katika vijiji hivyo na hivyo kuwa sababu ya kuongeza vijiji vingine vitano (5) kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 ambavyo ni Valeska, King'ori, Majengo, Patanumbe, Nkoarisambu, Nshupu na Kasanumba?

Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwamba, endapo kazi katika vijiji vitano (5) vinavyofanyiwa kazi/mradi kwa mwaka 2012/2013 haijamalizika, basi ni bora mradi ukamalizika kwanza na ndipo kuongeza mradi mwingine katika vijiji vipya vitano (5) kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kimsingi wananchi wa maeneo hayo katika Wilaya ya Meru wanapata adha kubwa ya maji kwa miaka mingi. Eneo la King'ori Madukani ambalo lina bomba la maji linalotokea maeneo ya Mlima Meru, wananchi hupata maji kwa mgao. Cha kusikitisha ni kwamba mkazi mmojawapo anauza maji ya bomba la Serikali katika eneo hilo la King'ori madukani, je, Serikali imetoa kibali kwa mkazi huyo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maji ni rasilimali inayotakiwa kufaidika kwa kila Mtanzania, ni kwa nini Serikali inakaa kimya wakati baadhi ya wananchi wanajimilikisha maji ya bomba lililowekwa na Serikali kwa faida yao wenyewe kama ilivyo King'ori Madukani ?

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifuatilie suala hilo ili kukomesha biashara hiyo ambayo inawaudhi wakazi wengine wa pale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Vijiji Kumi (10), Serikali iweke umuhimu mkubwa kukamilisha miradi hiyo katika Wilaya ya Meru ikiwa ni ile inayoendelea ya 2012/2013 pamoja na hiyo mipya ya 2013/2014. Hii itasaidia sana katika kuwapunguzia wanawake adha kubwa wanayoipata ya kusafiri umbali mkubwa kutafuta maji.

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, pamoja na kuunga mkono napenda kutoa hoja na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu upeo wa tatizo la maji Kitaifa; kero kubwa ya Watanzania kuliko zote kwa sasa ni upungufu wa maji, hasa vijijini. Takwimu za Wizara zinaonesha ni 58% tu ya wananchi vijijini ndio wanapata maji safi na salama. Wilaya ya Manyoni ni 53% tu, Serikali ikubali ushauri wa Wabunge kwamba tatizo la maji lisiendelee kushughulikiwa kwa utaratibu wa kawaida kupitia bajeti ya kawaida (*business as usual*).

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba, iundwe Wakala wa Maji Vijijini mithili ya *REA* (umeme), ili bajeti yake itoke Serikalini, Wahisani na mikopo ya nje na ndani, tusiendelee kutegemea fedha za mkopo wa *World Bank* pekee, lazima tuchukue hatua zingine nje ya miradi chini ya mkopo wa *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji Wilaya ya Manyoni, hasa Kata nane zilizo katika eneo la Bonde la Ufa kuna ukame

na maji yakichimbwa chini ya ardhi ama hayapatikani na yakipatikana yana chumvi nyingi. Hivi sasa kuna mradi wa *World Bank* katika Vijiji vya Kintinku na Lusilile, wataalam wamechimba visima, lakini wanakosa maji!

Mheshimiwa Spika, ushauri tunaoutoa kwa Wizara ni kwamba, maji katika vijiji hivi yavutwe kutoka mwinuko wa Mbwasa (*along Saranda escarpment*). Eneo hili tayari lina visima visivyopungua vitatu (3) na vyote vina maji mengi. Maji hayo tunaomba yawekewe bomba toka hapo kilipo chanzo cha maji (Mbwasa) hadi Kintinku. Aidha, vijiji vya njiani ambamo bomba litapita navyo vipatiwe maji, Vijiji hivyo ni Chelejeho, Maweni, Mvumi, Ngiti na Lusilile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ya kuvuna maji ya mvua; maji ya mvua takribani yote hupotea kila mwaka. Hii ni dhambi kubwa. Tujisahihishe, Wizara iagize uwepo wa sheria, kila mtu anayejenga nyumba ya bati au vigae ajenge tanki la chini la kuvuna maji kwa ajili ya familia yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara hiyo pamoja na Halmashauri za Wilaya ziweke fedha za kuvuna maji kwa kuweka makinga maji katika Mito ili tupate Mabwawa madogo (*Charcal dams*) ambayo yatapunguza sana tatizo la maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Spika, maji na umeme ni miundombinu muhimu katika kutukwamua kutoka katika dimbwi la umasikini. Kwa sababu hiyo, watumishi wa Wizara sharti wawajibike ipasavyo. Bahati mbaya Ngara tuna watendaji wabovu sana katika Idara ya Maji; Maji Mjini na Maji vijijini. Watendaji hao wanawaweka Wakandarasi ambao ni ndugu zao na hivyo kukwamisha miradi.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vitano (5) vya maji ya *World Bank* – ni Vijiji viwili tu vya Rulenge na Ngundusi vimeanza kushughulikiwa, lakini kazi inakwama kwama kwa sababu ya undugu wa Wakandarasi na Watendaji.

Mheshimiwa Spika, kuna Kijiji cha Mbuga ambacho kilikuwa kwenye orodha ya vijiji vya maji ya *World Bank*, lakini naona hakiko kwenye orodha tena wakati wanakijiji walichanga fedha zao. Kijiji hiki ni muhimu sana kwa sababu kina Sekondari mbili na Dispensary moja, naomba sana kirudishwe kwenye orodha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Ngara ina matatizo makubwa sana ya maji, karibu vijiji vyote 73 havina maji. Wilaya ya Ngara ina Mito mikubwa miwili ya Kagera na Ruvubu lakini hatufaidiki na maji ya Mito hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa sana kwa upande wa maji, kwetu Ngara ni watendaji wabovu na wabadhirifu na wanaotuchagulia Wakandarasi ndugu zao ambao hawakidhi viwango. Mwaka jana nilimtaja ndugu Rwegasira maji vijijini, mwaka huu naongeza Mkuu wa Idara ya Maji Mjini, ndugu Magai. Hawa watu wawili bila kuondolewa Ngara tatizo la maji litabaki pale pale. Najua hakuna siri Serikalini, lakini wananchi wamechoka na Wakuu hao wa Idara, nami siogopi kuwataja.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Maji, Mheshimiwa Waziri awasiliane na TAMISEMI (Serikali ni moja), watuletee watu wazuri na waadilifu. Maafisa hao waondolewe.

Mheshimiwa Spika, Ngara iko pembezoni mwa nchi, hivyo maafisa wanaopelekwa huko wanakuwa miungu wadogo, kazi ni kujitajirisha tu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza tena Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Wilaya yangu ya Ngara aone

ukubwa wa tatizo, Mji Mdogo wa Ngara una matatizo makubwa sana ya maji kwa sababu *system* ya Ngara *Hights* imechoka, mabomba yamechoka kwani yaliwekwa miaka ya 80.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, kikosi 821 cha Bulombora kimezungukwa na Ziwa Tanganyika. Cha kushangaza kikosi hiki hakina maji ya kutumia na kikosi hiki kinachukua wanafunzi ambao wanajiunga na JKT 3,000. Wanafunzi ambao wanajiunga na JKT pamoja na wakufunzi na wake wa wakufunzi hawana maji ya kutumia. Wakihitaji maji mpaka waende Ziwa Tanganyika, cha kusikitisha Ziwa Tanganyika kuna mamba na baadhi yao hupoteza maisha kwa kuliwa na mamba.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itayavuta haya maji kutoka Ziwa Tanganyika na kuingia kwenye kikosi 821 cha Bulombora na kuepusha adha wanayoipata wakufunzi pamoja na wanafunzi ambao wanakwenda kujiunga na JKT?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji safi; Mkoa wa Dar es Salaam kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa maji safi. Maji ambayo yanatoka *DAWASCO* yamekuwa si salama kwa kunywa. Wananchi wanalipia maji kila mwisho wa mwezi, lakini hawapati maji safi, wenye uwezo wananunua maji ya *drop* na kadhalika, kwa wasiokuwa na uwezo (hawawezi kununua maji ya *drop*) hutumia maji ambayo si salama kwa afya zao.

Mheshimiwa Spika, hii inasababisha milipuko ya maradhi ya mara kwa mara kwa mfano, kipindupindu, taifodi na kadhalika. Je, ni lini Serikali itahakikisha inasimamia vyanzo vyote vya maji na kusambaza madawa ya kutosha katika vyanzo vyote vya maji ili wananchi wapate maji safi na salama?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Mitaa wanajenga nyumba bila mpangilio, sehemu wanayojenga wananchi hao *DAWASCO* walikuwa wamepitisha mabomba ya maji safi na mulemule wananchi hao wanapitisha mabomba ya maji

machafu, hii itaepusha wananchi kutopata maradhi ya mlipuko!

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali haiwachukulii hatua hao ambao wanapitisha mabomba ya maji machafu kwenye vyanzo vya maji?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uchimbaji wa visima vya maji kwenye Mikoa mbalimbali; kuna hii miradi ya uchimbaji visima, wamekuwa wakichimba visima vikubwa na vipana kiasi ambacho hata walemavu wanashindwa kwenda kuchota maji na kusababisha maafa. Vile vile kuna baadhi ya visima havina maji, ni kwa nini visifukiwe au vikajengewa uzio na hivyo vinavyotoa maji vijengewe uzio maalum. Hii itaepusha vifo vya watoto pamoja na walemavu kwani kuna baadhi ya Mikoa imeweza kupata maafa kupitia visima hivyo kama Tabora, Singida na kadhalika.

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri iliyosheheni maoni mbalimbali ya kuboresha Sekta hii ya Maji. Wabunge wote waliochangia kwa maandishi, waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni wameonesha kuguswa sana na tatizo la maji katika nchi yetu, mijini, vijijini na mahala pengine panapohitaji huduma ya maji. Wabunge wote kwa pamoja wamefikia maamuzi yanayoonesha wazi kabisa kuwa, Sekta ya Maji ndiyo *key determinant* ya maeneo mengine zikiwemo Sekta za Afya, Sekta za Elimu na Sekta za Uzalishaji na wameonesha kuguswa kwao kuwa yale Malengo ya Milenia yakiwemo kupunguza umaskini, kuwapeleka watoto shuleni na kupunguza maradhi haya ya kuambukiza au ya mlipuko yanayochangiwa sana na tatizo la maji kutokuwapo.

Kwa maana hiyo, ninataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, yale yote mliyoyasema sisi kama Wizara tuliokabidhiwa dhamana hii, tutayafanyia kazi

na tutatoa ushirikiano yaweze kutekelezwa na Wananchi waweze kupata maji kama ilivyopangwa kwenye Sera zetu. Katika michango hii, lipo suala ambalo limejitokeza na limechangiwa na Wabunge mbalimbali, kwa hisia mbalimbali na hili ni la kupeleka Mradi wa Maji wa Same, Mwanga na Korogwe. Kweli katika hali tuliyo nayo ya ufinyu wa bajeti, katika hali ya kutokuwa na maji katika maeneo mengi ya nchi, inatoa hisia kwa Wabunge mbalimbali kwamba, huenda Mradi ule unatekelezwa kwa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa kabisa kama hisia alizonazo Mheshimiwa Blandes, ambaye amekuwa akifuatilia Miradi yake ya Maji, anaguswa na maji. Ninadhani *issue* hapa siyo nani kapewa nini, *issue* ni hali halisi kuwa maji yanahitajika sehemu nyingi katika miji yetu na ndiyo maana hisia zimetolewa kwa aina tofauti; wako waliotoa hisia kwa kuonesha kuwa wao wanahitaji maji katika miji yao, lakini wapo waliotoa hisia zao kwa kuonesha mbona haka kasungura kadogo kuna mtu kachukua sehemu kubwa zaidi! Tunalielewa hilo, lakini tatizo kubwa ni ufinyu wa bajeti ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kumshukuru sana Waziri wa Fedha, ambaye sasa ameonesha mwanga kuwa haya yote tunaweza kuyachukua na kufanya sehemu kubwa ya kutekeleza Miradi hii. Niseme tu kwamba, Serikali yetu kuanzia awamu ya kwanza, imekuwa ikitekeleza Miradi mbalimbali; ipo Miradi mikubwa hasa hii ya Miji ambayo uwekezaji wake ni mkubwa sana. Kuanzia miaka ya 1974 imejengwa Miradi ya *Handeni Trunk Main* ambayo ni mikubwa inayohudumia vijiji vingi.

Tuliweza kujenga Mradi wa Makonde unaohudumia Wilaya tatu za Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini. Hayo yalikuwa ni maamuzi makubwa, haikuwa na maana kwamba sehemu zote zina maji, lakini tuliamua kwamba ni lazima tuanze. Kwa kuzingatia misingi hiyo iliyowekwa na Baba wa Taifa, Serikali ya Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu imeendelea kutenga fedha kwenye Miradi mikubwa na mpaka sasa hivi tumeweza kujenga Mradi mkubwa wa Mbwinji – Masasi –

Nachwingea, ambao uko katika hatua za mwisho kukamilika na unagharimu shilingi bilioni 31. Tunajenga Mradi mkubwa wa Chalinze ambao unakaribia kukamilika na loti kati karibu tisa na Mradi huu unagharimu karibu bilioni 56. Kwa hiyo, hii ni Miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, ipo Miradi mikubwa ambayo ipo katika hatua mbalimbali za manunuzi, ikiwemo ya kutoa maji kutoka Shinyanga kwenda Tabora, kupeleka maji katika vijiji 100 vya kwenye bomba kuu linalotoa maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Shinyanga na Kahama. Kwa hiyo, kilichofanyika katika Mradi huu wa Same - Mwanga na Korogwe ni mwendelezo wa Miradi mingine ambayo ni azma ya Serikali ya kupeleka maji maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, maoni yao tumeyazingatia, lakini yote hii ni kwa sababu ya tatizo la fedha na haina maana kwamba kuna maeneo hatutafikia na kama ni lazima tuanze ili tuweze kuitekeleza Miradi hii yote. Ninawaomba sana muunge mkono hoja hii ili tuanze kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, imejitokeza *issue* kwamba, katika Mradi huu umetengewa fedha nyingi haziwezi kutumika zote kwa wakati mmoja. Mradi huu tunaugawa kwa loti tatu na sababu ya kuugawa kwa loti tatu ni kwa sababu unatakiwa utekelezwe kwa miezi 18, mwaka mmoja na nusu. Kwa hiyo, tutakuwa na wakandarasi watatu ambao mmoja atatoa maji kutoka pale Nyumba ya Mungu mpaka Kisangani na wawili watatoa kutoka pale Kisangani kwenda Same na mwingine kwenda Mwanga. Kwa hiyo, hizo fedha zitatumika kwa jinsi ilivyopangwa na kwa muda ambao tumeudhamiria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo machache, nawaomba Wabunge watuunge na nilete tafsiri ambayo siyo rasmi kwamba, tafsiri ya *www.com* tuseme *waache Wananchi wanufaike.com. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, niweze kupitia baadhi ya hoja za Wabunge ambazo wamekuwa wakichangia hapa na kwa sababu ya muda, nitapitia chache na tumeandaa kitabu hoja zote zimejibiwa na ufafanuzi wa kina umetolewa. Ipo hoja ya Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, aliyetoa pendekezo kwamba, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria umeonesha mafanikio kwa vile maeneo ya Mbozi, Ileje na Momba, yana shida ya maji. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua maji Ziwa Rukwa kama ilivyofanywa kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa ili kutatua tatizo la maji katika Miji ya Tunduma?

Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri, tunalipokea lakini kwa sasa tulichofanya ni upembuzi yakinifu uliokamilika mwaka 2012 unaonesha kwamba, Miji ya Vwawa, Miji ya Tunduma, Miji ya Chunya na Miji mingine ya Ileje kule Isongole, vyanzo vilivyopo vinajitosheleza kutoa huduma ya maji. Rasilimali ya maji ya Ziwa Rukwa inatakiwa tuiendeleze ili baadaye itakapobidi au itakapoonekana idadi ya watu imeongezeka, tuweze kutumia chanzo cha Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, alielezea ukosefu wa maji kwa Wananchi wa Jiji la Mwanza wanaoishi maeneo ya milimani hasa ya Jimbo la Ilemela.

Mheshimiwa Spika, Mwanza tunao Mradi wa kuboresha huduma ya maji unafadhiliwa na *European Investment Bank (EIB)* na Mradi huu utatoa huduma ya maji mpaka kwenye maeneo ambayo watu wamejenga milimani au juu ya usawa wa tenki ikiwemo Ilemela. Kwa hiyo, utakapokuwa umeanza kutekelezwa, Wananchi hawa watafaidika na huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, anaomba kasi iongozwe kukamilisha ahadi ya Rais ya kupeleka maji Tabora kutokea Kahama ifikapo mwaka 2014. Wizara imeshakamilisha taratibu za kuwapata Wahandisi Washauri wenye uwezo wa kufanya usanifu na uandaaji wa

makabrasha ya zabuni za ujenzi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Nzega – Igunga – Tabora, ambapo wahandisi washauri hao wamewasilisha mapendekezo tarehe 25 Aprili, mwaka huu.

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, ameuliza ni lini maji yatapatikana Namanyere ili kutatua tatizo sugu la maji. Pia amesema Serikali itenge fedha kutoka vyanzo vyetu vya ndani badala ya kutegemea wafadhili. Mwaka jana tulipeleka Wilaya ya Namanyere shilingi milioni 100 na ile kazi ya kuboresha huduma pale imeanza kufanyika, tumefunga pampu, tunapeleka mabomba na dira za maji, huduma hii itakuwa tayari mwezi huu wa tano, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za ndani, Serikali kama mlivyoona, itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya maji, kutumia hela zetu za ndani; na moja ya jambo ambalo tumelifanya kubwa mwaka huu ni kuanzisha Mfuko wa Maji ambao utaanza mwezi wa saba.

Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, aliuliza ni lini Serikali itawapatia maji Wananchi wa Tarime kutoka Mto Mara. Katika bajeti ya mwaka 2013/14, Serikali imetenga shilingi milioni 500 zitakazotumika kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Matokeo ya Haraka. Aidha, Serikali imekamilisha usanifu na uandaaji makabrasha ya zabuni kwa ajili ya Mradi wa Maji Safi. Ujenzi wa Mradi utafanyika katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vick Paschal Kamata, aliuliza tatizo la maji litaisha lini. Hapa tunao Mradi unaotekelezwa hivi sasa na Kampuni ya *Geita Gold Mine (GGM)*, ambao wanajenga chanzo cha maji kwenye Ziwa Victoria na wanajenga tenki kwa ajili ya kusambaza maji mjini na kulaza mabomba.

Mradi huu unagharimu dola milioni nne lakini sehemu ya pili ni sehemu ya kuweka mtandao wa mabomba katika Mji wa Geita na kupanua mtandao ambao unafanywa na

African Development Bank (ADB) na Serikali yetu, ambao ni Mradi unaogharimu dola milioni sita. Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya *GGM* unakaribia kwisha na kwa sababu sehemu ya pili ya kutanua pale mjini itachelewa, kwa sababu inafanyiwa upembuzi yakinifu, hii itakapokamilika ya *GGM* ianze kutoa huduma ya maji kwa kutumia mtandao wa maji uliopo. Tumelazimika kurudia kufanya upembuzi yakinifu kwa sababu imekuwa ni mahitaji ya wanaotoa fedha, *ADB,* wanataka wajiridhishe kwamba hata ile sehemu inayofanyiwa mtandao wa maji na *GGM* kama inafaa kwa ajili ya kuwekeza zile fedha. Kwa hiyo, Mradi huu ukikamilika, Wananchi wa Geita watapata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa amesema, Mwanza hawana maji wanahitaji mabomba mapya ili wapate maji. Vilevile amesema, Waziri wa Maji afanye ziara Mkoani Mwanza kwani Wananchi wa Mwanza wanahitaji maji kutoka kwenye mabomba ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Miradi mbalimbali; kama nilivyosema, kuna huu Mradi wa kuboresha huduma ya maji Mjini Mwanza, kuna Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka vijiji 100 Kahama na Shinyanga, kuna Miradi ya uboreshaji maji utakaojengwa kutoka Misungwi - Magu na Lamadi. Miradi hii ikitekelezwa, Wananchi watapata maji. Ombi la kwamba Mheshimiwa Waziri afike, tuko tayari tumepokea maombi na tutafika Mwanza.

Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe anasema, Mji wa Mugumu unapata huduma ya maji ambayo hayajatibiwa toka Bwawa la Manchila, tumelipokea na Serikali imetenga katika bajeti hii shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mtambo wa kutibu maji katika Bwawa la Manchila.

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, anasema Maji Dodoma Mjini yameongezeka; je, Serikali ina mpango gani kuhusu suala la uondoshwaji wa majitaka? Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya

uondoshaji wa maji Mjini Dodoma. Jumla ya kilomita 250 mitandao ya kukusanyia maji inatarajiwa kujengwa pamoja na mabwawa ya kudumu ya kutibia maji *(WSP)*. Jumla ya shilingi bilioni 102 zitahitajika kutekeleza Mradi huu ambao Serikali inatarajia kuanza kuutekeleza kwa awamu kupitia Programu ya Maendeleo Sekta ya *WSDP*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura anasema, katika bajeti ya mwaka 2012/13 ilitengwa fedha kwa ajili ya Bwawa la Farkwa, bwawa hili lingehudumia Wananchi wa Wilaya ya Chemba na Bahi, mpaka leo hakuna kazi yoyote iliyofanyika. Taratibu za ujenzi wa Bwawa la Farkwa kwenye Mto Bubu, Wilaya ya Kondoa katika Bonde la Kati zinaendelea, Bwawa hilo litakuwa chanzo cha maji kwa Manispaa ya Dodoma na Miji ya Wilaya ya Kondoa, Chamwino na Bahi.

Katika mwaka 2012/13 Mtaalamu Mshauri anayefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, kuandaa vitabu vya zabuni, aliajiriwa na ameanza kazi na tayari ameshaandaa *inspection report*. Kwa hiyo, matokeo ya kazi hiyo yataainisha uwezekano wa maji kutoka kwenye bwawa hilo kwa ajili ya umwagiliaji mifugo na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo anasema, Bwawa la Kwamarigwe linahitaji shilingi milioni 500 kujengwa upya kwa kuwa mvua zinaelekea mwisho ambapo bwawa hili linasaidia vijiji 15 na ng'ombe zaidi ya milioni 12 wanapata huduma hii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli bwawa hili ni muhimu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri mimi nimelitembelea. Serikali imelipokea hilo ombi na imetenga fedha kwenye bajeti hii shilingi milioni 500 kwa ajili ya kwenda kulifanyia ukarabati na kuona kama linaweza kuanza kutumika kwa madhumuni yaliyokuwa yamewekwa.

Mheshimiwa John Chiligati anasema, kuwepo kwa maji ya chumvi katika Bonde la Ufa na ushauri wa Mbunge maji yachukuliwe Milima ya Saranda katika visima vilivyopo

eneo la Ngwasa. Wizara itapeleka wataalam haraka kwenda maeneo yaliyopendekezwa na Mbunge kufanya tathmini na kushauri Wizara na Halmashauri ya Wilaya husika ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, mwingine ni Mheshimiwa Namelok Sokoine amesema, ufanyike utafiti wa maji katika Milima ya Meru, kuna vyanzo vingi. Tumelichukua hili ni wazo zuri, tutashirikiana na Halmashauri na Wataalam wetu kwenda kuona hivyo vyanzo na tuweze kuvitumia kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa Wananchi.

Mheshimiwa John Lwanji alisema watafiti wa maji ya visima pia wahusike katika kuvichimba ili vikikosa maji wasilipwe. Hili ni wazo zuri na ndiyo ambalo limetokea katika Miradi mingi ya uchimbaji visima kwamba, aliyefanya utafiti ni mtu mwingine, aliyechimba ni mtu mwingine na aliyekuja kujenga miundombinu ni mtu mwingine.

Kwa maana hiyo, visima ambavyo vilikosa maji tulishindwa kumpata aliyekuwa amefanya utafiti kwa sababu hawakuwa na mahusiano. Serikali kupitia Wizara ya Maji, tumesharekebisha hilo na Waziri atalisemea kwamba sasa tutaunganisha anayefanya utafiti na anayechimba itakuwa ni kampuni moja na kwa maana hiyo atawajibika kwa kile alichokifanya.

Mheshimiwa Rebecca amesema kukosekana kwa maji baada ya utafiti ni kweli tatizo hili limekuwa likijitokeza, lakini kwa hivi sasa tutakachofanya ndiyo haya ambayo nimesema, atapatikana mkandarasi mmoja atakayefanya kazi zote mbili. Yale maeneo ambayo utafiti ulionesha maji hayapatikani kitaalam, tutafanya utafiti maeneo mengine au tutaangalia teknolojia nyingine ya kuwapatia maji ikiwemo uvunaji wa maji ya mvua na teknolojia ya mabwawa.

Mheshimiwa Lekule Laizer alisema ni asilimia 15 tu ya Wananchi wa Halmashauri ya Longido wanapata maji, Miradi

ya *World Bank* imeonekana kufeli na Serikali itatue tatizo la maji katika Halmashauri ya Longido.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *World Bank* haijafeli, Serikali imeendelea kutekeleza Miradi katika Halmashauri zote nchini. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Longido inatekeleza Miradi katika Vijiji vya Longido, Sinya na Mndarara. Ujenzi wa miundombinu katika Kijiji cha Longido umekamilika kwa asilimia 55. Aidha, vijiji vingine navyo vitatengewa fedha katika awamu ya pili ya utekelezaji wa programu hii inayoanza mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini amesema, kuna vijiji havina maji ambavyo ni Katuo, Kikwea na Sadani. Kuna shilingi bilioni moja na nusu ambazo wafadhili wako tayari kuzitoa kwa ajili ya miradi ya visima. Kwa hiyo, Serikali itusaidie kupata *exemption*. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kupitia Halmashauri ya Mufindi, alete hayo maombi Wizarani tutayafanyia kazi ili hiyo *exemption* iweze kutolewa.

Mheshimiwa Suleiman Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini anasema, maji ni tatizo katika Vijiji vya Igagala, Katuma na Kasekese, anaiomba Serikali iongeze bajeti kwani maji ni uhai. Baada ya Serikali kukubali kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji, vijiji hivyo vimetengewa bajeti kama ifuatavyo: Igagala shilingi milioni 200.8, Kasekese shilingi milioni 368.2, Majalila shilingi milioni 267.8 na Katuma itatekelezwa katika bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Kondoa, ametoa shukrani kwa Serikali kutenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mradi wa Ntomoko na kwamba anasubiri ahadi hiyo itekelezwe. Ofisi ya Waziri Mkuu iliahidi kutoa shilingi bilioni 3.03 kwa ajili ya ukarabati wa Maporomoko ya Ntomoko. Serikali kwa kupitia Bajeti ya Wizara ya Maji, mwaka 2013/14 imetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mradi wa Ntomoko katika Halmashauri ya Kondoa na Chemba. Fedha zilizobaki zitakasimiwa katika bajeti ya mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Hussein Nassor anasema kuna matatizo ya maji Kanda ya Ziwa. Bajeti ya Maji izingatie kutatua tatizo la maji Kanda ya Ziwa. Katika mwaka wa fedha 2013/14, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kuvipatia maji vijiji 100 vilivyo kandokando ya bomba kuu la Mradi wa Kahama – Shinyanga, kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Wilaya za Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Uboreshaji huduma ya maji nchini utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa rasilimali za fedha.

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyetoa mchango wake ni Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere kwamba, Wanawake wa Kwimba wanahangaika kuchota maji usiku, hali hiyo inasababisha migogoro ya kifamilia.

Katika mwaka wa fedha 2012/13, Serikali ilipeleka kwenye Halmashauri ya Kwimba jumla ya shilingi milioni 574.9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji ambapo utekelezaji wa Miradi katika vijiji kumi unaendelea katika Vijiji vya Mwabilanda ambapo umefikia asilimia 65, Ishingisha imefikia asilimia 40.

Katika mwaka wa 2013/14, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 667.1 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Vijiji vilivyobaki. Aidha, baada ya Wizara ya Maji kuongezewa fedha, vijiji vitatu vya Wilaya ya Kwimba, vitajengewa Miradi ya Maji kama ifuatavyo: Lioma shilingi milioni 361.6, Igunguhya shilingi milioni 437.3 na Goloma shilingi milioni 414.4.

SPIKA: Ahsante muda umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Tuwasikilize kwanza, mwongozo unaweza ukasubiri tu hauna tatizo. Unajua mwongozo ni kusema ni sahihi au siyo sahihi. Kwa hiyo, naomba amalize Waziri kwanza halafu nitakuita.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, katika siku mbili za majadiliano wiki iliyopita, michango mizuri sana ilitolewa katika kuchangia hoja ya maji ambayo niliiwasilisha Siku ya Jumatano.

Mheshimiwa Spika, waliochangia waliisemea hoja hii kwa hisia kubwa na walitoa mawazo yao yaliyopo moyoni. Hata vyombo vya habari kama umeweza kuangalia na Wabunge navyo vimetoa ya kwao na vimeongea jambo hili kwa hisia kubwa kwa sababu ya ukubwa wa tatizo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba za Wabunge, Wabunge 46 walichangia hoja hii kwa kuongea hapa ndani ya Bunge na Wabunge 81 walichangia kwa maandishi. Wakati wa hoja ya Waziri Mkuu, Wabunge 29 walichangia hoja ya Maji.

Kanuni zetu za sasa haziruhusu kuwatambua mmoja mmoja kama walivyochangia katika hoja hii, lakini napenda nikuombe kwamba nawashukuru sana wote ambao wamechangia na kutoa mawazo ambayo yamejenga na kutuonesha njia ya kuelekea jinsi tunavyokwenda mbele katika kutatua tatizo hili.

Napenda niwashukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na niishukuru Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wadau mbalimbali ambao wametoa maoni katika Hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa waliochangia hoja na maoni yaliyotolewa ni mengi na Mheshimiwa Naibu Waziri amejaribu kujibu hoja mojamoja kati ya hoja zaidi ya 96 ambazo zimetolewa. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakubali kwamba, zile ambazo hatutaweza kuzijibu hivi sasa tutatoa kitabu cha majibu kabla Bunge hili halijakamilika.

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ambazo zimetolewa katika Bunge hili ni ufinyu wa bajeti ya Wizara na Sekta ya Maji. Katika Hotuba yangu niliyoiomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe shilingi bilioni 398.4 kwa ajili ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 18.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na zilizobaki, shilingi bilioni 379.4 kwa ajili ya maendeleo. Hisia za Wabunge, zilionesha kwamba, bajeti hii haitoshi kukidhi mahitaji ambayo ni makubwa, hasa katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, zilishawishi Bunge lijadiliane na Serikali, kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji, ili kutekeleza miradi zaidi katika sekta ndogo ya maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la mapendekezo hayo ni kwamba, wananchi wanaopata maji safi na salama huko vijijini hivi leo ni 58% ya wananchi wote. Hii ikiwa na maana kwamba, 42% ya wananchi wetu hawapati maji safi na salama na hili ni tatizo kubwa katika maendeleo ya nchi. Aidha, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 na Malengo ya Milenia, yanalenga kufikia 65% ya wananchi wote kupata maji mwaka 2015; hivi sasa tunatekeleza miradi ya vijiji vitano katika Halmashauri zote. Fedha zote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii huko vijijini imeshakwenda na ziko kwenye Wilaya zetu. Hivyo, utekelezaji wa miradi hii utakamilika mwezi Septemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine katika miradi hii zimechelewa, lakini hatua ambazo nitazichukua hapa leo, zitaharakisha miradi hii na kuifanya iweze kukamilika katika kipindi hicho. Miradi hiyo itakapokamilika mwezi Septemba, mwaka huu, idadi ya watu ambao wataongezeka wenye maji safi na salama katika nchi yetu ni watu milioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo yetu ya mwaka 2013/2014, tayari Serikali imetenga shilingi bilioni 105 kwa ajili ya maji vijijini. Fedha hizo tumezipitisha hapa kupitia Mafungu ya Mikoa, shilingi bilioni 94.9 na shilingi bilioni 10.3 tunaomba mkubali kuzipitisha katika Kikao hiki. Fedha hizo kwa pamoja zitajenga miradi ya vijijini katika vijiji 480. Vijiji hivyo vitakuwa ni wastani wa vijiji vitatu katika kila Halmashauri. Miradi hiyo itakapokamilika mwaka kesho, jumla ya watu 1,200,000 watapata maji; ukishapata watu 1,200,000 na wale 1,700,000 asilimia 60 ya Watanzania wanaoishi vijijini watakuwa na maji safi na salama. Sasa kwa *speed* hii, tutashindwa kufikia malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru sana Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kutoa mapendekezo mahsusi, ambayo yalisomwa hapa mbele yetu siku ya tarehe 24, ambayo yamekubaliwa na Serikali na utekelezaji wake utaongeza *speed* hii ya utekelezaji wa miradi ya vijijini na upatikanaji wa maji vijijini. Utatuweka vizuri katika kufikia na kupita malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Malengo ya Milenia na utaendana na Mpango wa Serikali wa *Big Results Now* – Tenda Sasa kwa Matokeo Makubwa. Kwa hiyo, Kamati ilipendekeza nyongeza ya bajeti ya ziada ya shilingi bilioni 184.5. Baada ya majadiliano ndani ya Serikali na majadiliano kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti na majadiliano kati ya Wizara yangu na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji; Serikali, imekubali kuiongezea Wizara ya Maji shilingi bilioni 184.5 kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Dokta Mgimwa, Waziri wa Fedha, hapa Bungeni hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zitatumika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 65, zitatumika kuongeza miradi ya maji ya vijiji viwili-viwili katika kila Halmashauri na kufikia vijiji vitano katika kila Halmashauri mwaka 2013/2014 na hivyo, jumla ya vijiji 840 vitatekelezwa nchi nzima katika mwaka huu wa fedha. Matokeo ya kazi hiyo ni kwamba, watu 62% watapata maji Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili litakalonufaika na fedha hizo ni kujenga miundombinu ya kusambaza maji katika mabwawa ambayo yamekwishajengwa tayari katika Wilaya kame za Simanjiro, Bunda, Monduli, Rorya, Musoma Vijijini, Nkasi, Iringa Vijijini, Nzega, Kilindi, Chunya, Itimila na Sikonge. Jumla ya shilingi bilioni 13 zitatumika na kuwapatia maji watu 480,000.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu litakalotumia fedha hizi ni kujenga miundombinu ya pampu na mabomba ya kusambaza maji katika visima virefu ambavyo vimeshachimbwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Gharama za kutekeleza miradi hiyo itakuwa ni shilingi bilioni 11.2 na mradi huu utawapatia wananchi 640,000 maji safi na salama pamoja na kupatia mifugo mingi maji.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni kupanua, kukarabati na kujenga miundombinu kwenye miradi katika Wilaya mbalimbali; miradi ambayo kwa sasa haitoi huduma ipasavyo kutokana na uchakavu, kwa gharama ya shilingi bilioni 10.8 na kufaidisha watu 440,000.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano, ni kujenga miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi kutoka katika miradi mikubwa ambayo usanifu umekamilika na miradi mikubwa inayohitaji ukarabati. Miradi hii inahitaji shilingi bilioni nane na itafaidisha watu zaidi ya 500,000.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita, ni kufanya usanifu na ujenzi wa mradi wa Ugala, utakaopeleka maji katika Mji wa

Urambo na Mji wa Kaliuwa na vijiji vilivyoko njiani Mkoani Tabora. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 12.1.

Mheshimiwa Spika, eneo la saba, ni miradi ya maji vijijini iliyoainishwa na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwenye Taarifa yangu niliyoipeleka mbele ya Kamati hiyo. Miradi hii ya vijijini itakuwa katika kila Wilaya na itagharimu shilingi bilioni 53.5 na miradi hiyo itafaidisha watu 614,780.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongezewa fedha, ni lazima tuchukue hatua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa na tunapokuja kukutana hapa tena mwaka kesho mwezi wa sita, tuwe tuna ripoti ya kukamilika kwa miradi hii ambayo tunaitaja katika ripoti hii. Miradi yote itawasilishwa kwenye Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo Wabunge watasambaziwa kabla ya mwisho wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa na ili kuhakikisha kwamba fedha ambazo ziko huko vijijini kwa kutekeleza miradi ya vijiji vitano na yenyewe inatumika haraka na miradi ya vijiji hivyo ikamilike na wananchi wapate maji, nachukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia leo tunafuta vibali vyote vya *No Objection* ambavyo vinangojewa huko katika Wilaya mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Miradi ambayo inajulikana imeorodheshwa, imesanifiwa na Wilaya zimepata fedha, ianze kutekelezwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ununuzi iwe Halmashauri za Wilaya kuanzia sasa badala ya Mamlaka hiyo kuwa kwenye Wizara ya Maji. Halmashauri itangaze, ifanye tathmini ya waombaji, ichague Mkandarasi na ihakikishe utekelezaji wa miradi. Waheshimiwa Wabunge, sisi wote ni Madiwani na tunashiriki katika Kamati ya Uchumi na Fedha, tushiriki katika Kamati hizi kwa sababu fedha ambazo zimepelekwa ziko huko tayari na fedha nyingi sana na tumezionesha kwenye jedwali ambalo tumesambaza pamoja na Kitabu cha Hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe kweli, badala ya kuja hapa kuuliza kwamba, mradi wangu umefikia wapi; tuhakikishe tunajua miradi yetu imefika wapi, utekelezaji wake unakwendaje, ili tushauriane maeneo na hatua za kuchukua kabla ya kuulizana maswali humu ndani. Kama tunaulizana yawe ni maswali ya kimsingi, ambayo tukiyarekebisha yatasaidia na Wabunge wenzetu wengi. Sekretarieti za Mikoa, Wizara ya Maji, watafuatilia utekelezaji wa miradi hii, watasimamia miradi hii kwa karibu na kutoa ripoti kila mwisho wa mwezi ili tujue maendeleo ya kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi, ninapenda kusisitiza kwamba katika utekelezaji wa hatua ya manunuzi, lazima Sheria ya Manunuzi ifuatwe. Kuondoa vibali, haina maana kwamba, tusifuate Sheria za Manunuzi, ni lazima Sheria zifuatwe na Sheria zile zikifuatwa kwa busara si lazima zichukue muda mrefu sana. Hivi sasa *circle* ya mradi wa maji kuanzia mradi wa maji unapobuniwa, kuanzia unapofanyiwa *study,* unaposanifiwa, unapotangazwa, mpaka Mkandarasi apatikane, inachukua wastani wa siku 234. Muda huu ni mrefu sana na hatuwezi kutekeleza miradi hii kwa kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapendekeza hatua ya nne hapa kwamba, Wilaya ziondoe vikwazo vyote vya utekelezaji wa miradi hii. Katika Wilaya zingine ambazo zimepokea fedha na zimepokea labda asilimia 80, kati ya kila shilingi 100, shilingi 20 hazijafika; uamuzi unafanywa kwamba tungoje mpaka fedha zote ziletwe kutoka Hazina au fedha zote ziletwe kutoka kwenye Halmashauri. Wilaya ziendelee na utekelezaji wa miradi kwa hatua zile ambazo zina fedha na wakati wanapofikia hatua ambazo sasa fedha zitakuwa na matatizo, watoe taarifa haraka, ili fedha hizo zitafutwe na miradi isisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, utaratibu wa miradi ni Serikali kutoa fedha au fedha za washirika wa maendeleo na wananchi wanahitajika kuchangia miradi hii, ili fedha za wananchi zinazochangiwa, zishiriki katika *operation and*

maintenance, yaani zishiriki katika kuendesha na kukarabati miradi kama inaharibika.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya zaidi ya 45, taarifa nilizonazo ni kwamba, Viongozi wa Wilaya wanangoja wananchi wengine wachangie 20% ya mradi au wachangie 5% ya mradi au wachangie 2.5% za mradi. Ule msingi wa kuchangia wananchi ni ili wananchi waone ushiriki wao na mradi ukishakamilika, ukikabidhiwa kwa wananchi, wananchi waweze kuwa na hela ya mbegu *(Seed Money),* ya kuanza kuendesha na kukarabati mradi wao, fedha zao sio kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha za wananchi zinazochangwa sio kwa ajili ya ujenzi, fedha za wananchi zinazochangwa ni kwa ajili ya kuendesha na kukarabati na kutengeneza miradi mahali ambapo imeharibika. Kwa hiyo, utekelezaji wa miradi katika Wilaya zote ufanywe haraka iwezekanavyo bila kuwa na visingizio ambavyo havina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itakapofika mwezi Septemba, tutazikagua hizi Wilaya zote kulingana na ahadi zao za kutekeleza miradi hii. Zile ambazo hazitakuwa zimetekeleza miradi hii, Maofisa wanaoshughulika na utekelezaji wa miradi hii, tutawachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuwaondoa na kuweka watu wengine ambao wanaweza kufanya kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi, Wizara, inaanzisha Ofisi kwenye Kanda. Madhumuni ya kuanzisha Ofisi hizi kwenye Kanda ni kuhakikisha kwamba, ufuatiliaji wa miradi, usimamizi wa miradi na pale inapohitajika maeneo ambayo Wilaya hazina Wahandisi, wanasaidia Wilaya hizo kuhakikisha kwamba, miradi inaanza na kutekelezwa kwa wakati. Kwa hiyo, wataalamu hawa watashirikiana na wataalamu kwenye Sekretarieti za Mikoa katika maeneo ya kitaaluma pale inapobidi na katika kusimamia miradi.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ambalo ninataka

kulichukulia hatua, nimeunda Kamati ya Wataalamu wa Ujenzi wa Miradi ya Maji itakayochambua gharama za ujenzi wa maji vijijini na kutoa ukomo wa bei za utekelezaji wa miradi hiyo. Katika miradi mingine huko vijijini gharama zake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeunda Kamati ya Wataalamu, itakayoongozwa na Profesa Idrissa Mushoro wa Chuo Kikuu cha Ardhi na ina Wataalamu ambao wamebobea katika maeneo ya ujenzi na gharama za ujenzi. Kamati hii pia itahusu washirika wetu wa maendeleo ili kuhakikisha kwamba, kweli, tunapata thamani ya fedha ambazo tunaweka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla, wajue kwamba, pale tunapochimba kisima na kuweka bomba la kwanza pale ili wananchi pale kisima kilipo wapate maji, sio gharama peke yake katika kutekeleza miradi ya maji vijijini. Baada ya kuweka pampu na kuweka bomba pale, kuna bomba la kusambaza maji kwenye vijiji na kwa kawaida kuna ujenzi wa ma-*tank,* kuna usambazaji, ili kuwe na maeneo ya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali ya vijiji na gharama zote hizi ni muhimu mkazielewa, lakini ni muhimu kwamba kila *component* ya gharama hizi inakuwa gharama ambayo inalingana na thamani ya kazi iliyofanywa na inalingana na uwezo wetu wa kupeleka maji vijijini. Kutokana na hatua hii Wilaya, zione umuhimu wa fedha zilizopo ziweze kuhudumia vijiji vingi zaidi. Wilaya ambazo zitakuja na *innovation* au ubunifu huo, zitapewa ruhusa kutekeleza miradi hiyo na zitasaidiwa na Wataalamu ambao watakuwa kwenye maeneo ya Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa sana wale watu ambao wanachimba visima kama Wakandarasi waweze kuwajibika zaidi. Katika mfumo wa mradi wa maendeleo ya maji awamu ya kwanza uliopo sasa Mtaalam Mshauri anakwenda aangalie atambue mahali pa kuchimba kisima, halafu Mkandarasi wa kuchimba kisima anaonyeshwa aambiwe chimba hapa ndipo mtaalam aliposema, Mshauri

analipwa anakwenda zake. Mtaalam anakuja kama hakuona maji ni kosa la Mshauri ambaye ameshalipwa ameondoka. Kuanzia sasa mtu ambaye anachimba visima lazima awe na ujuzi wa kujua mahali penye maji wapi na kwamba sisi tutalipa kisima kilicho na maji na wala siyo kisima kikavu na visingizio vinavyoungana na jambo hili tunataka tuviondoe ili tupate kweli wakandarasi ambao wana ujuzi na uwezo wa kuchimba visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tutawachukulia hatua kali wale wote ambao watakuwa na visingizio mbalimbali vya kutoanza miradi hii na kutotekeleza miradi kwa wakati. Tumefikiria pia kwamba tuwe na mashindano kati ya Wilaya na Wilaya ili zile Wilaya ambazo zinatekeleza miradi yake kwa haraka na kwa ubora unaotakiwa ziweze kupewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya huko mbele.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imetoa mapendekezo mengine mbalimbali ambayo Wizara yangu itaendelea kuyatekeleza na kuyafanyia kazi ili kuboresha huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mjini na vijijini. Maeneo hayo ni pamoja na kuendelea kujadiliana na Serikali ili kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye dawa za kusafisha maji.

Mheshimiwa Spika, pili kupitia Mpango Maalum wa Serikali wa 'Tekeleza Sasa kwa Maendeleo Makubwa' *(Big Results Now Program)* ili kuongeza uwekezaji zaidi katika eneo la maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itachukua hatua madhubuti ya kutunza vyanzo vya maji kwa kuendelea kuviainisha na kuvitengea maeneo yake kisheria na wananchi watashirikishwa katika kutunza vyanzo vya maji. Serikali itahimiza Halmashauri ambazo bado hazijatunga sheria ndogondogo za utunzaji wa maji na vyanzo na maeneo ya mito ili sheria hizo ziweze kutungwa na wananchi watunze maeneo yao ya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara itapitia tena utekelezaji wa mradi katika vijiji kumi ili kuondoa changamoto zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya changamoto nimezieleza hapa na ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe karibu sana na miradi hii na tuelewe kwamba fedha tayari ziko kule kwenye vijiji zile ambazo zinahitajika kutekeleza miradi hii mpaka mwezi Septemba na kufikia nusu ya vile vijiji kumi na baada ya fedha hizi za mwaka huu kuanza kupelekwa Wilayani, fedha zote ambazo zinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa vijiji vingine vile vilivyobaki vitano zitatolewa na miradi hii ambayo nimeianisha hapa na itaelezwa kinaganaga katika taarifa tutakayopeleka katika Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na vyenyewe vitekelezwe kwa haraka ili tuweze kuwafikishia wananchi maji na kwamba fedha hizi ambazo Serikali imetuamini imetupa, imesikiliza kilio chetu tuweze kuzitumia vizuri na kusiwe na visingizio ambavyo havina maana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote na ninaishukuru Kamati kwa kazi ambayo imeifanya ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na haya mabadiliko chanya katika bajeti ambayo tumeiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto ambazo zilitolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni kwamba *EWURA* inadhibiti zaidi sekta ya nishati kuliko inavyodhibiti sekta ya maji. Kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha *EWURA, EWURA* inadhibiti utoaji wa huduma kwenye sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, maji na usafi wa Mazingira. Kazi za kudhibiti zilizofanywa na *EWURA* katika Sekta ya maji zimeelezwa kwa kina katika hotuba yangu ya bajeti.

(Hapa Waziri alinyamaza kwa muda akisoma karatasi aliyopatiwa)

SPIKA: Mkimpelekea barua muda huu atachanganya mambo, wewe endelea tu kusema yale uliyoyaandaa.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kazi za kudhibiti zilizofanywa na *EWURA* katika sekta ya maji zimeelezwa kwa kina katika hotuba ya bajeti kuanzia kifungu 139 hadi 148, kazi hizo ni:-

(i) Kufuatilia utendaji wa Mamlaka za Maji mijini na kuzitolea maboresho ya kufanya ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

(ii) Kupitisha bei za maji katika miji mbalimbali kulingana na gharama ambazo zinatumika katika kuyazalisha maji hayo.

(iii) Kutatua malalamiko ya wateja kuhusu huduma ya maji safi na maji taka itolewayo au na *bill* ambazo wamepewa.

(iv) Kuanzisha utaratibu wa kudhibiti sekta binafsi ya kutoa huduma ya maji kupitia magari ya maji yaani *water tankers and water bowser* na kuangalia ubora wa visima binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti watoa huduma binafsi, *EWURA* imetayarisha mwongozo wa udhibiti wa biashara ya maji kwa kutumia magari binafsi katika eneo linalosimamiwa *DAWASA* na utekelezaji wake umeanza. Udhibiti huu unahusisha *EWURA* kupitisha bei zilizoainishwa na kukagua magari ya maji ili ubora wa maji ulingane na ukweli kwamba maji ni chakula na hivyo lazima wapelekewe wananchi yakiwa salama.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha, Bagamoyo wamechangia sana juu ya huduma ya maji ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Abuu Jumaa, Mheshimiwa Sylvestry Koka, Mheshimiwa Khatib Haji, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na Mheshimiwa John Mnyika. Katika jitihada za kutatua tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam Serikali inatekeleza miradi ya kuongeza maji ili maeneo yote yapate maji ikiwa ni pamoja

na maeneo yenye mabomba ya mchina. Kazi zitazofanyika ni pamoja na upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini ambao sasa umekamilika kwa zaidi ya 85% na unatazamiwa kukabidhiwa mwezi Julai mwaka huu, upanuzi wa Ruvu Juu na ambao utaanza mwezi Julai mwaka huu na kukamilika mwezi Desemba mwaka 2014 na uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera ulioanza mwezi Machi mwaka 2003 na unategemewa kukamilika mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii pamoja na fedha za kuchimba visima hivi, tumetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kuanza malipo ya wananchi ambao watapisha ujenzi katika maeneo haya. Miradi hii itaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 300 za sasa hadi kufikia lita milioni 756 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza sana na hili jambo nataka kulisema tena kwamba ujenzi wa bomba kubwa la maji kutoka Ruvu Chini mpaka Dar es Salaam au kutoka Ruvu Juu mpaka Dar es Salaam au kujenga miundombinu kuleta maji kutoka Kimbiji kuleta Dar es Salaam siyo kama kuweka chupa za soda kwenye *production line* ya kiwanda cha soda kwamba soda hizo baada ya dakika kumi na tano zitakuwa zimejazwa na zinatoka. Hii ni kazi ya ujenzi wa miundombinu, inachukua mpaka miaka mitatu, minne. Tumeeleza rasmi hapa jinsi ambavyo tumewekeza kama Serikali katika maeneo haya na nia yetu ya thabiti kabisa ya kuleta maji Dar es Salaaam.

Mheshimiwa Spika, katika kazi hii, tusinyang'anyane fito, tunajenga nyumba moja hakuna mtu mmoja atakayepata *credit* ya kazi yote kwamba kazi hii isingekuwa mimi isingefanywa, kazi hii inafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi haifanywi kwa ushabiki. Wananchi msidanganywe kuandamana kwamba bomba la maji linaweza kuwekwa siku ya ljumaa likafika eti muende Wizara ya Maji muandamane mdai mpewe glasi ya maji. Maji yatakuja katika kipindi ambacho kimeelezwa na tumeeleza jambo hili kwa kinaganaga sana. Wananchi tumewapeleka hata nyinyi wenzangu Waheshimiwa Wabunge mmekwenda

mkaangalia mkaona kazi inayotekelezwa. Tusifanye ushabiki, hii ni kazi ya kujenga nchi yetu, subirini maji yatakuja Dar es Salaam kama mwaka kesho miradi mingine haitakuwa imekamilika, tuulizeni lakini msiende kusumbua watu ambao wanajenga miradi kwa ajili ya ushabiki wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika miradi hiyo maeneo yote yasiyopata maji kwa sasa yatapata maji ya kutosha ikiwa ni pamoja na Kiluvya, Kibamba, Mlonganzila, Kwembe, Mbezi Luis, Mbezi Msumi, Masakuzi, Makabe, Mpiji na kadhalika. Maeneo haya yamewekwa katika taarifa mbalimbali ambazo tumezitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika majimbo ya Kibaha, Mjini na vijijini itakwisha baada ya kuongeza uzalishaji katika mtambo wa Ruvu Juu. Kazi ya upanuzi wa mtambo wa ujenzi wa bomba itaanza mwezi Julai na itakamilika mwishoni mwa mwaka kesho. Fedha kwa ajili ya miradi hii zimetolewa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwakilishi kwenye bodi ya *DAWASA* na *DAWASCO*, Mkoa wa Pwani unawakilishwa katika Bodi ya Wakurugenzi ya *DAWASA.* Wakati wa uteuzi wa Bodi ya *DAWASCO* utakaofanywa hivi karibuni uwakilishi wa Mkoa wa Pwani utazingatiwa. Hata hivyo nimetoa maagizo kwamba Bodi iliyoko sasa ikitumia Sheria ile iwaalike Wajumbe watakaopendekezwa na Ofisi ya Mkoa wa Pwani ili waweze kuendelea kuwakilisha eneo lao katika Bodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *desalination* ya maji ya bahari ili kutafuta ufumbuzi wa haraka wa maji ya Dar es Salaam, tulifanya uchunguzi wa vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya Dar es Salaam, teknolojia ya kutumia maji ya bahari kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilikuwa moja ya iliyochunguzwa. Matokeo ya awali yalionyesha kwamba maji ambayo yanafanyiwa *desalination* gharama yake ni mara tatu ya maji yanayotoka Ruvu Chini na Ruvu Juu, kwa hiyo

wakati ule mradi ule ulisimama. Hivi sasa tumepata taarifa kwamba kumekuwa na maendeleo katika teknolojia ya kuondoa chumvi kwenye maji na kwa hiyo Serikali ikishirikiana na mwekezaji binafsi, inafanya utafiti huo na kama shirika hilo binafsi litaweza kuonyesha kwamba linaweza ku-*desalinate* na kuingiza maji kwa bei ile ambayo imewekwa na *EWURA* kwa kutumika kwa maji yanayotoka Ruvu Juu na Ruvu Chini, Serikali haitasita kutoa ruhusa kwa kampuni hiyo kuingiza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa *program* ya maji, *program* ya maji hufanyiwa ukaguzi wa aina mbalimbali ikiwemo wa fedha, ununuzi, ufundi yaani *technical,* thamani ya kazi ikilinganishwa na fedha (*value for money)*, ufanisi au *performance*. Kazi hizi hufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa mujibu wa Sheria na Mamlaka ya Ununuzi Tanzania (*PPRA*) na Wakaguzi Binafsi au *Independent Auditors* kulingana na makubaliano ya Serikali na washirika wetu wa maendeleo. Aidha, kila taasisi zinazotekeleza *program* ya maji zinakaguliwa kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2010, ukaguzi wa kiufundi ulifanywa ambao uliangalia utekelezaji wa *program* kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2007/2008 hadi 2009/2010 na kampuni binafsi ya *M/S Artikines International* na CAG alifanya Ukaguzi Maalum yaani *Special Audit* katika kipindi hicho. Mwezi Desemba mwaka 2012, Mkaguzi wa nje *M/S UPI Mark* alianza ukaguzi wa kiufundi kwa kipindi cha miaka 2010/2011 na 2011/ 2012 na atawasilisha ripoti ya ukaguzi huo mnamo mwezi Mei mwaka huu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hufanya ukaguzi wa *program* kila mwaka ambapo taarifa ya mwisho wa mwaka wa fedha 2011/2012 ilishajadiliwa na wadau kama rasimu na iliwasilishwa mwezi Februari mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, katika kaguzi zote hizi, haijagundulika ubadhirifu wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na mradi wa maji wa *Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project* ambao kwa sasa ni sehemu ya *program*

ya maji. Hata hivyo, tutaendelea kumkaribisha Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili aweze kuangalia na sehemu za miradi hiyo kama sehemu ya mradi wa vijiji kumi, sehemu ya mradi wa Wachina huu ambao unasemwa kila siku ili kutuhakikishia kwamba fedha ya Serikali haikufujwa na kama kuna mtu ambaye amehusika katika kufuja fedha hizi za Serikali aweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko juu ya ugawaji wa rasilimali katika utekelezaji wa sekta ya maji. Serikali kwa kutambua kuwa upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki kwa wananchi wote, inajaribu na inafanya hivyo, inagawanya fedha rasilimali katika vijiji vyote 132. Mgao wa fedha katika Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa za kuendeleza huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini hufuata kanuni au *formula based allocation* ambayo ilikubaliwa kwa pamoja kati ya Serikali, washirika wa maendeleo, wadau wengine na sekta ya maji. Vigezo vya kugawa fedha kwa kila Halmashauri viliwekwa kutokana na majadiliano na makubaliano yaliyofikiwa katika Wizara ya Maji, Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Wizara ya Fedha. Vigezo hivyo ni idadi ya watu ambao hawajapata maji katika Halmashauri, aina ya teknolojia itakayohitaji kutumika katika Halmashauri hiyo kama ni mtiririko au ni visima vifupi au ni visima virefu na idadi ya wananchi katika kila Halmashauri. Kigezo cha idadi ya watu ambao hawajapata huduma ya maji, kina uzito mkubwa kuliko vigezo vingine.

Mheshimiwa Spika, katika kugawana fedha kwa Mikoa kuanzia Julai mwaka 2007 hadi Machi mwaka 2013, Mikoa mbalimbali imepata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi vijiji vyake kama ifuatavyo; Arusha shilingi bilioni 11.9, Dar es Salaam shilingi bilioni 2.6, Dodoma shilingi bilioni 10.5, Iringa shilingi bilioni 13.4, Kagera shilingi 15.5, Kigoma shilingi 10.2, Kilimanjaro shilingi bilioni 10.5, Lindi shilingi bilioni 11.3, Manyara shilingi bilioni 12.3, Mara shilingi bilioni 9.2, Mbeya shilingi bilioni 19.8, Morogoro shilingi bilioni 8.5, Mtwara shilingi bilioni 12.7, Mwanza shilingi bilioni 14.5, Pwani shilingi bilioni 11.8, Rukwa shilingi bilioni 9.7, Ruvuma shilingi bilioni 8.7,

Shinyanga shilingi bilioni 19.8, Singida shilingi bilioni 11.8, Tabora shilingi bilioni 11.6 na Tanga shilingi bilioni 15.1.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi mikubwa na ya Kitaifa na miradi ya maji mijini. Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya Kitaifa na miradi ya maji mijini awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mathalani ujenzi wa miradi mikubwa ya Kitaifa ya Makonde huko Mtwara, Wanging'ombe-Iringa, Mgangokyabakari-Mara, Chalinze-Pwani, Maswa- Shinyanga, Handeni *Trackmen*-Tanga na mradi wa Kahama -Shinyanga -Mwanza ilijengwa kwa vipindi tofauti kwa ajili ya kuwahudumia wananchi katika maeneo ambayo yanashida kubwa za maji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na gharama za ujenzi wa miradi ya maji mijini kuhitaji fedha nyingi, utekelezaji wa miradi hufanywa awamu kwa awamu kwa kuyapa vipaumbele kwanza maeneo yenye uhaba wa huduma hiyo. Miradi ambayo imetekelezeka na kukamilika katika kipindi cha hivi karibuni ni pamoja na maji safi katika Mamlaka ya Mji wa Mbeya, Iringa, Songea, Mwanza, Shinyanga na Babati na miradi ya miji midogo ya Wilaya kama Kahama, Igunga, Kibiti, Mpwapwa, Utete na Kongwa. Kwa kipindi hiki, miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na Musoma, Lindi, Bukoba, Singida, Kigoma, Tabora, Sumbawanga, Dodoma, Mtwara, Dar es Salaam na Morogoro na baadhi ya Miji ya Wilaya ikiwa ni pamoja na Mvomero, Turiani, Nansio, Masasi, Nachingwea, Kilosa, Sengerema, Kibaigwa, Orkesmet, Bunda, Namanyere, Bariadi, Muheza, Chalinze, Geita na miradi mingine. Utekelezaji wa miradi hii unaendelea. Pia miradi mingine kama alivyoitaja hapa Mheshimiwa Naibu Waziri inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, maandalizi ya mradi mpya mkubwa wenye thamani ya shilingi bilioni 105 katika miji ya Ramadi, Magu, Mwanza na Misungwi, yanafanywa kwa kushirikiana na *European Investment Bank* na Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Mradi huu pia utajenga mfumo wa kuondoa maji taka katika Mji wa Bukoba na Musoma. Kiasi

cha fedha ambacho kinatumika kama nilivyosema ni *Euro* 105 milioni na miradi hii itaanza kutekelezwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ambayo itaanza kutekelezwa ni katika makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Washirika ya Maendeleo kwamba washirika watapeleka fedha zao moja kwa moja kwenye miradi na watateua mkandarasi na kusimamia ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na malalamiko kwamba fedha nyingi zinaenda mijini kuliko zile zinazokwenda vijijini. Baada ya nyongeza ambayo Serikali imekubali kuipatia Wizara ya Maji, shilingi bilioni 184.5, hivi sasa fedha za maendeleo za ndani kwa ajili ya vijijini katika Wizara ya Maji zitafikia shilingi bilioni 315, ukilinganisha na shilingi bilioni 241 za kutoka nje. Kwa hiyo, mwelekeo ni mzuri na Serikali inafanya kila iwezavyo kuhakikisha kwamba inaongeza uwekezaji katika sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi waliongelea uwezekano wa kuanza Mfuko wa Maji. Tumeshatengeneza Kanuni na zinangojea kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali na tumetengea mfuko huu shilingi milioni 100 kama *seed money*. Baada ya mfuko kuwepo, tutaleta mapendekezo mahsusi ili tuangalie vyanzo vya fedha kwa ajili ya mfuko huo ili sasa mfuko huu ukishakuwa na vyanzo ambavyo ni kamili, sasa tuweze kuanza Shirika la *TANWATER* ili tuweze kutekeleza azma yetu ya kuwa na fedha za kuaminika kabisa ambazo zitakamilisha na kumaliza shida ya maji ambayo inatukabili vijijini kwetu, katika miji yetu ya Wilaya na katika Miji Mikuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kabla ya kumaliza hotuba yangu hii, nieleze kwamba, pamoja na hatua hizi ambazo tunazichukua kupeleka maji katika maeneo ya miji, katika vijiji na katika maeneo mengine mengi, ni muhimu sana tuhakikishe kwamba maji hayo yatakuwepo leo, kesho na kesho kutwa na kwamba rasilimali hii ya maji tuliyonayo sasa, tutaweza kuwakabidhi wajukuu zetu na wenyewe

waendelee kuitumia. Yapo matatizo makubwa sana ambayo yanakabili rasilimali hizi za maji. Tatizo la kwanza, ni uharibifu wa mazingira. Tumekuwa tunakata sana miti katika maeneo yote. Ukaangalia kwenye ramani utakuta sehemu yote ya katikaki ya Tanzania imepakwa rangi ya kijani kwamba kuna miombo *woodlands* huko ndani, tuna misitu ya miombo mikubwa kupita miombo yote Duniani kote. Hivi sasa ukienda huko kwenye hiyo Miombo, miti yote imekatwa na mito na vyanzo vya maji vingine vinavyotokea huko, vinaanza kuwa ni vya kipindi cha mwaka, wakati wa mvua maji yanapita, wakati wa kiangazi maji yanakauka. Kwa hiyo, ni lazima tuchukue hatua kubwa ya kuvihifadhi vyanzo hivi na kuhakikisha kwamba chanzo cha nishati ya kutumia majumbani kinaondoka kutoka mkaa na kuwa chanzo kingine.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametupatia gesi. Hatua ya kwanza ambayo tungeishughulikia ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wa Tanzania wanakopeshwa matenki yale madogo ya gesi na majiko ya gesi ili wabadili mfumo wa nishati ya kupikia nyumbani na matumizi ya nyumbani kutoka mikaa na kwenda kutumia gesi ili kuhifadhi misitu yetu na vyanzo vyetu vya maji. Tusipofanya hivyo hivi sasa, tutachelewa treni na tukifika *station* itakuwa imepita na sisi wote tutakuwa na matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia tuangalie na kupambana na mabadiliko ya Tabianchi. Tuchukue hatua mbalimbali kuwasaidia wananchi ambao wanatumia ardhi oevu, waweze kuwa na maji mbadala ili kuweza ku-*save* vyanzo vyetu vya maji.

Mheshimiwa Spika, tunayo maoni mengi ambayo tumeletewa na mengi yako kwenye *book* kubwa hapa, kama nilivyoleza, tutaleta kitabu ambacho tumeweka pamoja maoni yote haya na maswali na changamoto, tumezipatia majibu kama ambavyo tunayaelewa ili wote tukiondoka tuwe na uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, sasa nachukua fursa hii kuliomba Bunge lako Tukufu watupitishie bajeti ambayo tumependekeza ili tuweze kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, Mheshimiwa Kabwe Zitto kwanza!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutaka Mwongozo wako. Kabla Wizara ya Maji haijanza kueleza maelezo yake na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Fedha alisimama kutoa Kauli ya Serikali kuhusiana na suala ambalo lilikuwa limeahirishwa la utafutaji wa fedha kwa ajili ya Wizara ya Maji. Sasa ulimwomba Waziri wa Fedha aji-*commit* kusema ni kiasi gani na Waziri wa Maji pia amesema ni kiasi gani ambacho Serikali imekitafuta. Kwa mujibu wa taratibu zetu za Bunge, Kauli ya Serikali ni lazima isambazwe kwa Wabunge. Waziri wa Fedha hakuwa sehemu ya wachangiaji katika Wizara ya Maji. Amekuja kulipa Bunge taarifa baada ya *consultations* ambazo zimefanyika katika kipindi cha *weekend* hii ambayo imepita. Naomba taarifa hii ili iwe rasmi, naomba nikumbushe kwamba, mwaka juzi tulitaka fedha ziongezwe Wizara ya Usafirishaji na Bunge likapiga makofi sana hapa, fedha zile hazikuongezwa hata senti tano, pamoja na kwamba tulipitisha hapa Bungeni. Hivyo, ni lazima kupata taarifa rasmi ya Serikali, ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini pili lazima tuone mabadiliko haya kwenye vitabu, kama *amendments* za vitabu, tuone hizo fedha na tuweze kujua hizo fedha sasa zinakwenda wapi. Kwa sababu Kamati imeanisha maeneo ambayo tunataka fedha hizi ziende, yako wazi wazi, kwa Waziri wa Fedha katika

taarifa yake alitakiwa kuanisha kama namna ambavyo Kamati ya Maji imeanisha ili tukitoka hapa tuwe na taarifa kamili ya Serikali na wasije wakatufanya kama walivyofanya wakati wa Wizara ya Usafirishaji, tulisema shilingi bilioni 94 zimeongezwa lakini hazikuongezwa.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka mwaka 2011, Bunge hapa lilikubali kwamba nyongeza ya fedha ambazo zitatokana na nyongeza ya ushuru wa mafuta ya taa, itaenda kwenye miradi ya umeme vijijini. Fedha hizo hazikwenda mpaka leo. Kwa hiyo, ni lazima tupate *commitment* ya uhakika na Waziri wa Fedha alete taarifa yake hapa, aiwasilishe kama Kauli na ipokelewe ili tuweze kuitumia kuwabana wasipopeleka fedha Wizara ya Maji, vinginevyo hapa tutakuwa tunacheza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Tundu Lissu!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Langu linalingana kidogo na Mheshimiwa Zitto lakini naomba niweke mkazo kwenye Kanuni inayohusika. Kanuni ya 49(3), Waziri mwenye kutoa Kauli atawajibika kutoa nakala ya Kauli yake kwa Wabunge wote wakati inapowasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametoa Kauli bila hata kusoma, hakuwa na chochote alichokuwa anakisoma wakati akitoa kauli ya Serikali. Maana yake ni kwamba hata wewe huna alichokuwa anakisema, achilia mbali Waheshimiwa Wabunge wote. Naomba Mwongozo wako kama ni sahihi kwa Waziri kuja kutoa kauli ya Serikali kwa maneno tu, wakati Kanuni zinaweka wazi kwamba anatakiwa agawe nakala kwa Wabunge wote wakati anapoiwasilisha. Tuambiwe kama hii ni sahihi, kama siyo sahihi tutaomba hatua stahiki zichukuliwe.

SPIKA: Mheshimiwa John Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (2) pamoja na Kanuni ya 101 (1). Kanuni ya 57 (2) inahusu utaratibu wa

kufanya mabadiliko kwenye hoja na Kanuni ya 101 inahusu utaratibu wa Bunge kupitisha Bajeti kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mtoa hoja anahitimisha hoja yake, kufuatiwa Kauli iliyotolewa na Waziri, naungana mkono kabisa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Tindu A. Lissu kuhusiana na ile kauli, lakini mimi niko kwenye majumuisho ya Waziri. Katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri, akaanza kutaja miradi iliyofanyiwa marekebisho akianisha kiwango cha fedha kwa ile miradi mbalimbali, bila sisi Wabunge kupewa nakala kama ilivyo kawaida ya Jedwali la Marekebisho, kifungu kwa kifungu, kwa maeneo ambayo mabadiliko yamefanyika ili kupata hakika marekebisho hayo yanahusu maeneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako kwa sababu kwa vyovyote vile maelezo yalitolewa hayakufata utaratibu wa Kanuni wa kufanya mabadiliko yanayokusudiwa, ni kwa nini sasa Kanuni ya 69(1) isitumike, ili ama Mbunge mmojawapo au wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, uweze kuruhusu kutolewa kwa hoja ya kuahirishwa kwa mjadala, ili Serikali ikakae tena, iweze kufanya mabadiliko kifungu kwa kifungu, kabla Bunge halijakaa kama Kamati tuletewe Jedwali la Marekebisho, tusiuziwe mbuzi kwenye gunia, ili hizi fedha kweli tuzione na tuone kweli zinakwenda wapi na zinakwenda kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni hizo.

SPIKA: Nashukuru kwa hiyo Miongozo, hivyo ndivyo nilikuwa nategemea mtauliza kwa sababu utaratibu huu wa kuwa na Kamati ya Bajeti ni mara yetu ya kwanza na *assumption* tuliyokuwa nayo kwa kuunda Kamati ya Bajeti ni kukaa na Serikali kupitia vifungu kwa vifungu pale ambapo tunafikiria kwamba, pengine tungependa nguvu zetu zielekee upande huu zaidi kuliko mahali pengine. Kwa hiyo, ndivyo walivyofanya wakati wa *weekend* tulipoachana hapa. Hizi hela zilizotolewa siyo kwamba zimepatikana

nyingine, zimetoka kwenye baadhi ya vifungu, tena naambiwa hata baadhi ya Wizara tulizopitisha, lakini yote hii ni *health*. Kwa hiyo, mtatategemea kwamba tunafanya *juggling* kuhamisha hapa, peleka huku, peleka hapa. Hiyo kazi haikuwa rahisi, hivyo ndiyo maana nilisema nilikuwa nategemea ninyi mtasema hivyo na ningeshangaa kama msingesema hivyo. Kwa hiyo, ni kweli hata Wizara tulizopitisha mafungu yao yamenyofolewa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini sisi tunachokisema, bajeti tunayoizungumzia sisi ni ile ya Waziri wa Fedha, hii *juggling* itaendelea, mnaweza kusema leo sisi maji hapa shilingi bilioni 184.5, imefanyika kweli. Sasa tunachokisema kwa maana ya Wizara hii, itabidi tuletewe *addendum* kwa sababu vinginevyo kifungu tutakachokuwa tunapitisha hapa siyo chenyewe lakini kwa maana ya kutazama bajeti nzima kufikia mwishoni ndiyo tutakwenda kwenye ile *Appropriation Bill*, maana hiyo ndiyo itaanza kubadilisha hata mafungu mengine. Kwa sababu ya muda tuliokuwa nao na ilibidi tufanye hiyo kazi, bado tunaweza kuitaka Wizara ikaweke mahali ambapo ilifikiria itaweka, kusudi tupate angalau mtazamo kwamba hii iliyosemwa ni kweli.

Kwa nini Waziri wa Fedha hakusambaza Kauli ya Serikali, ni kwa sababu tumemtaka asubuhi aweze kusema, kwani huyu asingeweza kusema kama hana maneno mengine yoyote, lakini hiyo haizuii Waziri wa Fedha kuleta Kauli iliyoandikwa.

Kwa maana hiyo, basi mimi ningependa tutumie nafasi hii Waziri wa Maji na Waziri wa Fedha wajaribu kuona ni maeneo gani ambayo wamefanyiwa mabadiliko ili tutakapokuja mchana kupitisha vifungu tuwe na hakika kwamba ni eneo linalohusika. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

(Saa 5.35 Asubuhi Bunge lilisitishwa
Mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Serikali asubuhi, tulikuwa na kazi mbili ambazo tulitaka tuwe na uhakika nazo. Moja, ilikuwa ni kujaribu kupata maelezo ya Waziri wa Fedha aliyokuwa ametoa hapa kwa maandishi. Ameleta na nakala aliyonipa mimi ina *covering letter.* Kwa hiyo, msije mkaona kwamba aaah, mbona haijasainiwa hapa? Ina *covering letter*, ndiyo hii ninayo. Kwa hiyo, ni yale aliyosema asubuhi, ndiyo yale ambayo ameandika.

Hiyo ya kwanza, ya pili, katika vitabu vyetu vya *recurrent expenditure* na *developments votes*, kumefanyika *addendum*s, maandiko ya kuweka humu ndani kubadilisha vifungu fulani. Lakini kama tulivyoeleza, Bajeti kamili ya Serikali ni ile atakayotoa Waziri wa Fedha. Hapa ni *provisionary,* hata tunapopitisha huwa ni *provisionary,* kwa sababu hata waliponyofoa fedha nyingine kupata hizi, hata mafungu mengine yamekuwa *affected*.

Kwa hiyo, yale yatakuwa yanaonekana pale tutakapofika Wizara inayohusika, lakini mwisho wa jumla ya fedha zote zilizopitishwa zitapitia kwenye *Appropriation Bill*. Kule ndipo tutakapokuwa tumesema nini kimetokea wapi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kama tungekuwa tulianza vizuri na Bajeti *Committee* mapema, labda haya yangekuwa hayakutokea. Lakini nilishawaambia, wakati tulipokuwa tunafanya *briefing* kwamba utaratibu tuliojianzishia wenyewe kwa siku za mwanzo tutakuwa na *teething problems*, utakuwa na matatizo ya hapa na pale. Lakini hayo siyo matatizo ya udhaifu wa utaratibu, ni namna yenyewe tu. Kwa mfano, sasa imekuwa jana na leo kuweza ku-*fit in* vifungu vile, siyo rahisi. Bado tunamwagiza Waziri wa Maji akikaa vizuri na watu wake aweze kutoa tena maelezo kwa kirefu kuhusu mradi mmoja baada ya mwingine kusudi muweze kuufanyiwa kazi mnakokwenda.

Kwa hiyo, naomba mwelewe hivyo kwamba tumefanikiwa kupata nyongeza ya fedha, lakini ni katika

kuchukua vifungu vingine. Sasa mtu asidhani kwamba mchezo huu unaweza kuendelea *indefinitely,* kwa sababu kwa mujibu wa Katiba yetu inatuzuia kufungua Bajeti Kuu. Tunaweza kugombana gombana humu ndani kwa ndani lakini siyo zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, mimi nawashukuru sana Wizara kwa kuweza kufanya hayo, na ninaomba tunapojielekeza kwenye fungu, tutakwenda taratibu kusudi muweze kuelewa nini kinachoendelea.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 49 - Wizara ya Maji

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*..... Tsh 3,661,296,000/=

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Jenista Mhagama. Wengine sikuwaona wamesimama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi. Fungu ni hilo hilo kama lilivyosemwa na ninasimama kwenye Mshahara wa Mheshimiwa Waziri na lengo langu ni jema tu, siyo kwamba nataka kuondoa Mshahara. Maelezo yangu ni kama yafuatayo:-

Kwanza kabisa nakubaliana na hoja iliyoletwa leo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuhakikisha kwamba Wizara hii ya Fedha inaongezewa fedha ili kwenda kutatua matatizo ya maji katika nchi nzima kama Sera ya Maji inavyosema na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyosema. Nakubaliana na naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa sikivu na kuamua maamuzi magumu ya kuongeza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fedha hii itakwenda kutatua tatizo la maji na hasa Vijijini kutoka asilimia 55 mpaka

kwenda kwenye 66 kwa kuongeza idadi ya Vijiji. Lakini kwa uzoefu tulionao, nataka sasa hapo Serikali inisikilize vizuri na inisaidie kujibu hapa Bungeni. Kwa uzoefu tulionao, miradi hii mikubwa yote katika nchi yetu ya Tanzania, pamoja na fedha hizi tunazoziongeza tukiamini zinakwenda kujibu matatizo haya, zinaathiriwa sana na tatizo la Sheria ya Manunuzi tuliyonayo mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ile isiporekebishwa, kazi hii nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi haitafanyika na wananchi wa Vijijini na Mijini hawatapata maji. Huo ni uhakika nilionao. Sheria ile ina upungufu mkubwa, na unaona kabisa kwamba inasababisha utekelezaji wa miradi kutokufanikiwa kwa sababu ya urasimu na udanganyifu mkubwa ulioko katika eneo la manunuzi na hata ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali imesema hivyo.

Je, Serikali kupitia Waziri wa Maji leo, anatuambiaje Waheshimiwa Wabunge, lakini na Watanzania wote wanaofurahia maamuzi haya ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kutatua tatizo la maji, ni lini watatuletea ile Sheria ya Manunuzi yenye utata mkubwa na inayosaidia kutokufanikiwa kwa miradi mingi yenye nia njema ya Serikali ya Chama chetu ibadilishwe na kiu hii ya upatikanaji wa maji na hasa maeneo ya Vijijini iweze kutekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo hayo kutoka kwa Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri mjiandae, mtajibu kwa pamoja baadaye. Mheshimiwa Clara **Diana** Mwatuka.

Waheshimiwa Wabunge, tunatumia kifungu cha 101(3).

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa dukuduku langu nililonalo kutokana na Bajeti hii kwa lile ambalo nililifikisha juzi katika kuchangia kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu, nilikuwa nimezungumzia au kulalamikia juu ya hali ya Kusini kulivyosahauliwa kwa kila mambo, na nikaelezea kwamba maji kule ni shida, akina mama wanalala visimani, Wilaya ya Newala, maji wanakunywa, wanamwomba Mungu kwamba mvua inyeshe haraka hata kama wakati wa kifuku bado ili wapate maji kwa kuwa hawana maji mengine mbadala. Mabomba yamekuwa shida, na nikaeleza kwamba maji wanayokunywa kule, wageni mnapokwenda mnapewa ya kwenye chupa, ya viwandani. Mgekuwa mnapewa yale, msingeyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaomba vilevile kwamba afadhali wangepatiwa dawa wasafishe yale maji. Vilevile nikaomba kwamba kule Masasi miradi ndiyo, ilipelekwa ya Vijiji kumi; visima vile kumi havitoi maji. Nikaeleza kwamba vijana wanachimba na wanafanya miradi, visima vifupi tu. Sasa: Je, Serikali inasemaje juu ya hili? lendelee kubaki vilevile Kusini kama Kusini au kwa safari hii kwa Bajeti hii mtawarekebishia? Naomba jibu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa John Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba ufafanuzi kupitia kifungu cha Mshahara wa Waziri na iwapo ufafanuzi hautaridhisha, nitaomba hoja ya kuondoa Shilingi kwenye Mshahara wa Waziri ili hili jambo nitakalolieleza liweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye ukurasa wa tatu, ilipendekeza kwamba Serikali itenge jumla ya Shilingi bilioni 529 kama mchango wa kutosha kwa mwaka huu wa fedha katika kupunguza ukubwa wa tatizo la maji nchini. Katika majumuisho na katika kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali imekubali kutokana vilevile na maoni ya Kamati kuongeza kiasi cha Shilingi bilioni 184.5 ambayo ni hatua kiasi, lakini bado haijafikia kiwango ambacho Serikali ilipaswa kutenga kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ambao umeridhiwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa zaidi siyo tu kutengwa kwa fedha, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, kwenye aya ya 188 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 88 wa Kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri; mwaka 2012 baada ya kutambua ukubwa wa tatizo la maji, kulitengwa Shilingi bilioni 140 za masuala ya maendeleo kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mujibu wa hotuba ya Waziri mwenyewe, mpaka ilipofikia mwezi Machi, 2013, ikiwa muda umepita takribani asilimia 75 ya muda wa utekelezaji wa mwaka wa fedha, fedha ambazo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikuwa ni Shilingi bilioni 29 peke yake, ambazo kwa mujibu wa takwimu za Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni asilimia 20.7 peke yake ya kiwango cha fedha ambacho kilipaswa kutengwa. Kwa hiyo, hakikufikia hata robo kwa maana ya asilimia 25, wakati mpaka hatua hiyo, kama kweli tumedhamiria kuondoa matatizo ya maji ilipaswa kuwa zimetengwa angalau asilimia 75 ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata hakikisho kutoka kwa Waziri wa Fedha ni kwa vipi safari hii imejipanga kwamba fedha zitatolewa kwa wakati ili kweli tuweze kutekeleza kwa vitendo adhima ya kuondoa matatizo ya maji nchini?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ole-Sendeka.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na usikivu wa Serikali wa kukubali kutenga Shilingi bilioni 184 katika miradi ya maendeleo ya maji na kwa imani kwamba hii inaweza kusaidia kutatua pia matatizo ya fedha zilizokuwa zinawekwa kwenye bajeti kila mwaka na bahati mbaya fedha zilikuwa hazipatikani, ikiwemo ile Shilingi bilioni 1.8 katika Vijiji vile ambavyo vinalazimika kuhama kuanzia mwezi wa Saba kuhamia Wilaya nyingine za Simanjiro kwa ajili ya ukosefu wa maji na shule nyingine kulazimika kufungwa; nilikuwa nimetoa pendekezo la kutumika kwa fedha za Benki ya *Society*

General, mchakato ambao Mheshimiwa Waziri anaujua kabisa kwamba ulikuwa umefikia katika dakika za ukingoni, ili kuondoa adha ya watoto wanaopinda miguu pale Mererani na katika Kata zinazozunguka za Naisinyai, Indiamtu na Shambarai pamoja na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Hai na maeneo ya Wilaya ya Arumeru Mashariki, ili kuhakikisha kwamba tunaokoa maisha ya watoto hawa ambao sasa wanageuka kuwa vilema na kuzingatia kuwa tunaweza kupata maji kutoka Mlima Kilimanjaro au Mlima Meru kwa kutumia fedha hizo.

Nilitaka kujua, nini msimamo wa Serikali katika kuhakikisha kwamba adha hii ya watoto wanaopinda miguu kutokana na maji yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu inaweza kutumika? Inaweza kuchukua hatua gani zinapaswa kuchukiliwa sasa ili kuondokana na adha hiyo na fedheha hiyo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Iddl Azzan.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane tu na wenzangu kuipongeza Serikali kwa ongezeko hili la Shilingi bilioni 184, nikiamini kabisa kwamba tatizo la maji angalau kwa kiasi fulani litaondoka hapa nchini. Kwa sababu Sera ya Maji inataka kila mwananchi apate maji safi na salama, na kwa kuwa Serikali imeshaanza kuchukua hatua za kukabiliana na hali hiyo kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama, naomba Serikali itueleze tu, yapo maeneo ambayo miradi hii itakamilika mwaka 2014 na maeneo mengine itakamilika mwaka 2015, lakini kipindi hiki cha mpito yapo maji ambayo yanapatikana siyo kwa wingi, ni maji machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo liko karibu nchi nzima lakini Dar es Salaam ni zaidi. Nataka kufahamu Serikali inachukua hatua gani kwa wale ambao wanahujumu maji haya machache yasifike kwa wananchi ama kwa mabomba kupasuka ama kwa kufanya biashara

haramu ya kuuza maji, kufunga pampu kubwa na kuchukua maji yote badala ya kwenda kwa wananchi yanakwenda kwa hao wanaouza maji? Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo katika kipindi hiki cha mpito kabla ya miradi hii haijakamilika 2015?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Machali, nilikuona.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninaamini kabisa kwamba siyo Sera ya Serikali kuwa na baadhi ya Watendaji ambao wana-*lack integrity* katika kuhakikisha miradi ambayo imekusudiwa na Serikali inakwenda kama ilivyokusudiwa. Katika mchango wangu nilichangia nikauliza juu ya mradi mmoja ambao umekuwa unasuasua, nimetoa kama mfano na maeneo mengine Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakichangia, wakionyesha kutokuridhishwa na hasa hii miradi ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia.

Nilikuwa naomba kauli ya Serikali isaidie kuweza kufahamu, Serikali iko tayari kumsimamisha yule Mkandarasi ambaye kuna mradi mmoja niliutaja hapa, kule Kasulu ambaye ameonekana kwa kipindi cha miezi sita na inakwenda kwisha mwezi ujao itakapofika tarehe tisa, kwa kuwa hajafanya kazi ambayo kwa kweli kwa kiwango kile na Mhandisi wa maji ameonyesha mfano mbaya wa kushindwa kuweza kusimamia mradi ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate ufafanuzi kwa kuwa nimezungumzia hilo na hiyo nimeitoa tu kama *case study,* lakini ni *concern* ya Wabunge wengi. Nini hatima ya Serikali katika kuweza kumwondoa Mkandarasi yule, pamoja na kuwachukulia Watendaji wote ambao wameonyesha utovu wa nidhamu katika kusimamia miradi ya maji ambayo inatekelezwa hapa nchini ili kuweza kuleta ufanisi?

MWENYEKITI: Makandarasi kama huyo, siyo *necessarily* huyo, hilo litakuwa Sera. Ukiona unakwenda pake yako nyumbani, haiwezekani.

Mheshimiwa Suleiman Nchambi!

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sera ya Maji ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi...

MWENYEKITI: Naona ungehama huo mstari wa huko nyuma, husikiki. Naomba usogee mbele.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sera ya Maji ni kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya maji safi na salama na kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuzingatia Sera hiyo iliona ni vyema kuanzisha miradi mikubwa ya maji itakayoweza kusaidia Watanzania wengi ambao watafikiwa na huduma ya maji safi na salama, moja ya miradi hiyo mikubwa ni mradi wa maji toka Ziwa Victoria ambao unahudumia wakazi wa Mji wa Shinyanga na Kahama na baadaye maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huo kwa awamu ya kwanza ulikamilika na wananchi wananufaika na maji hayo, na awamu ya pili ilikuwa ni mradi wa takiribani bilioni 13 ambao ungeweza kuwanufaisha wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa kiasi kikubwa ili Sera ile ya Maji ambayo iliwekwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa nia njema kabisa ya kuwahudumia Watanzania wote iweze kukamilika na kuwafikia Watanzania wengi na baadaye wote; naomba sasa nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Watanzania hawa waliko Kishapu ni sawa na Watanzania waliokuwa Shinyanga na Kahama na maeneo mengine ambao wanapata huduma ya maji safi na salama:-

Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kunihakikishia katika marekebisho haya ya Bajeti yaliyofanyika mpango huo

wa kuyapeleka maji ya Ziwa Victoria, utakamilika kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu?

MWENYEKITI: Naomba mjiwekeze kwenye Sera zaidi kuliko kwenye maeneo yenu. Mheshimiwa Laizer!

MHE. LAIZER M. LEKULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa Serikali ielewe kwamba miradi yote nchini 10% inakwenda kwa ajili ya manunuzi. Kwa hiyo, hili jambo alilozungumzia Mheshimiwa Jenista, huo utaratibu na sheria ziletwe haraka sana kwa sababu fedha za Serikali zinakwenda kwa ajili ya manunuzi. *(Makofi)*

Suala la pili ni uwiano.....

MWENYEKITI: Kwa hiyo, ni moja tu. Sasa usizungumze la pili, kwani la kwanza lilishaulizwa.

MHE. LAIZER M. LEKULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwiano nimelalamika sana hapa katika bajeti hii na bajeti zilizopita, nikisema kwamba Wilaya ya Longido ina matatizo makubwa ya maji.

Serikali katika nyongeza hii haikutambua kabisa Wilaya ya Longido kwamba tuna matatizo ya maji. Maji yameongeza maisha magumu kwa wananchi wa Longido. Sasa sijui Serikali inatusubiri na sisi tuandamane kama watu wa Ubungo ndiyo tufikiriwe! Kwa sababu kwanza Ubungo ina matatizo madogo kuliko Longido.

Sasa kama ni maandamano ya wananchi wa Longido na sisi tuanze kuandamana ndiyo tupate maji; naomba katika bajeti hii na sisi Longido tukumbukwe kwa sababu sikuona popote kwamba jibu la wananchi wa Longido wanapata ufumbuzi wa maji. Sisi ni watu kama watu wengine ambao wamewekewa pesa kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, kama mnaendelea kudai miradi ya kwenu, basi nitaifunga orodha hii. Mheshimiwa Zitto!

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati inatoa taarifa yake hapa, ilionyesha tofauti kubwa iliyopo katika mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya Wizara ya Maji kati ya maeneo ya Mijini na Vijijini, na Kamati ikawa imeomba Serikali iweze kuangalia ni namna gani ya kuweza kurekebisha jambo hili.

Napenda Waheshimiwa Wabunge niwaonyeshe kwamba kabla ya mabadiliko haya ambayo Bunge limeyawezesha kupatikana, maeneo ya Vijijini ambayo ndiyo yana 74% ya Watanzania wote, fedha zilizokuwa zimetengwa za miradi ya maji zilikuwa ni Shilingi bilioni 75 tu na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Vijijini wanisikilize kwa makini sana. Mijini zilikuwa zimetengwa Shilingi bilioni 254.

Baada ya marekebisho haya na kuongezeka kwa fedha hizi kidogo ambazo tumezipata, tungepaswa kupata zaidi kama jinsi ambavyo Kambi ya Upinzani ilivyokuwa imependekeza, sasa hivi fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya Mijini ni Shilingi bilioni 266, fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya Vijijini baada ya nyongeza ni Shilingi bilioni 237. Asilimia 74 ya Watanzania wanaoishi Vijijini wametengewa takribani sawa na 24% ya wananchi ambao wanaishi Mijini.

Napenda Waziri atoe kauli hapa kwa sababu *trend* hii imeendelea miaka yote. Watu wote tunafanya kazi, tunatoa kodi na kodi zinakusanywa, lakini fedha zinakwenda Mijini kwa sababu watu wa Mijini wanajua kupiga kelele zaidi kuliko sisi wa Vijijini. *Trend* hii tusipoiuzuia, maendeleo Vijijini hayatakuwepo. *(Makofi)*

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukubaliane hapa na Waziri atoe *commitment* yake kwa sababu hili ni suala la kisera, kwamba mgawanyo wowote wa fedha za bajeti unaokuja, uhakikishe Vijijini wanapata 70% na Mijijini wanapata 30% ya mgawo wa maji.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeeleweka. Tunaendelea na mwisho ni Mheshimiwa Blandes!

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nataka kuzungumzia kwamba kwenye mchango wangu nilijitahidi sana kuzungumzia tofauti kubwa sana ya mgawanyo wa fedha hizi za maji na kusema kweli nilizungumzia miradi ya maji inayokwenda kwa Mheshimiwa Waziri, nikazungumzia kwamba ni fedha nyingi, yaani nilisema Shilingi bilioni 30 lakini leo katika mabadiliko haya zinasomeka Shilingi bilioni 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba sana kwamba katika Shilingi bilioni 32 hizi amege kiasi fulani kiende katika Jimbo la Karagwe. Nataka majibu, kwa nini sioni Karagwe hapa?

MWENYEKITI: Sasa hilo suala la siyo la kisera. Naona nifunge. Waheshimiwa Mawaziri mwanze kujibu hoja moja moja na unaweza kusaidiana na Naibu wako. Aanze Waziri wa Fedha kuhusu Sheria ya Manunuzi.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kwa umakini wao wameeleza namna ambapo bajeti ikishaidhinishwa, miradi mingi inachelewa. Inaelekea kwamba Sheria ya Manunuzi haikidhi kuhakikisha kwamba tunakuwa na *value for money.* Katika hilo Serikali inachukua nafasi ya kupitia Sheria ya Manunuzi ili tuelekee kuwa na sheria inayokidhi manunuzi ambayo baadaye tunapata *value for money,* yaani thamani ya manunuzi ifanane na fedha tuliyotoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itachukua uamuzi wa kuipitia ile sheria na tutaileta hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mawaziri!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Diana Mwatuka swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwatuka, anaonesha kwamba tumesahau Mikoa ya Kusini na nilidhani hii siyo sahihi sana ikajulikana hivyo kwa Watanzania, kwa sababu hata katika maelezo yetu leo tumeeleza kwamba moja ya mradi mikubwa ambayo Serikali imewekeza ni Mradi wa Mbwinji Masasi Nachingwea unaogharimu Shilingi bilioni 31 na utahudumia wananchi wa Vijiji vya Wilaya hizo mbili. Nikaeleza pia kwamba kuna mradi mkubwa uliojengwa mwaka 1957 wa Makonde unaohudumia Wilaya tatu, yaani Mtwara Vijijini, Newala na Tandahimba.

Sasa ni kweli tatizo la maji lipo na niseme tu kwamba tunalichukua, tutaendelea kuboresha huduma kwenye Vijiji alivyovisema na katika huu mgawo tulioongezewa fedha tutahakikisha vile Vijiji alivyovitamka Mheshimiwa Mbunge vinapata maji.

Pia niendelee na jambo lingine kisha nimwachie Mheshimiwa Waziri. Kuna hili suala la Mheshimiwa Azzan kuhusu upotevu wa maji Dar es Salaam na kwamba ni mikakati gani ya muda mfupi wakati tukisubiri ile miradi mikubwa ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ili kuona kwamba wananchi wanapata maji. Imeonekana kwamba upotefu wa maji ambao unafikia 50% Dar es Salaam, kati ya 50%, basi 30% zinatokana na watu kuiba maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri.....

MWENYEKITI: Ongeza sauti au sijui vipi!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Nasema hivi, imeonekana kwamba katika 50% za upotevu wa maji Dar es Salaam, basi 30% kati yake zinatokana na watu kujiunganishia kiholela, wizi, kuweka mabomba ndani ya nyumba, kuweka matenki na kuuza bila vibali. Kwa hiyo, tulianzisha Kampeni ya kusaka wezi wote hawa na inakwenda vizuri sana na mpaka sasa hivi tumekamata watu zaidi ya 86 ambao baadhi yao wamefikishwa Mahakamani na taratibu za kusikiliza kesi zao zinaendelea.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba naomba sana Watanzania na Wanasiasa kwamba wakati tunataka maji yaongezeke kwa wananchi wa Dar es Salaam, basi tusaidiane pia kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanalinda miundombinu hii wala hawaibi wala kubomoa ili wananchi wengi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni la Mheshimiwa Blandes. Nafahamu kwamba anapata shida kwake kwenye Mji wa Omurushek kuhusu maji na ndiyo maana anafikia hatua kwamba pengine tungemega hizi Shilingi bilioni 32 ili ziende kwake. Nataka kumhakikishia kwamba tumesikia kilio chake na kwa kuanzia tayari kwenye awamu ya kwanza kuna Shilingi milioni 150 kwa ule Mji wa Omurushek na katika mgawo huu wa pili tutamwongezea tena fedha kwa ajili ya Mji huo wa Omurusheki na Vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kutupa nafasi hii. Maelekezo yote ambayo mfumo huu mpya umetupa yanasaidia kujenga historia ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika amesema kwamba Serikali iliombwa itenge fedha kufikia Shilingi bilioni 509.

Napenda kusema kwamba hivi sasa tunavyokwenda, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo baada ya ongezeko hili, imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 379.4 na kufika Shilingi bilioni 553.2, na fedha za ndani zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 138.2 kufika Shilingi bilioni 312.066.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri ijulikane kwamba fedha za nje katika bajeti hii sasa ni Shilingi bilioni 241.2 ukilinganisha na fedha za ndani Shilingi bilioni 312.1. Kwa hiyo, kwa hali ya bajeti tuliyonayo, Serikali imefanya juhudi kubwa

kutafuta fedha na kubadilisha hali ya bajeti ambayo tunayo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeulizwa hapa kuhusiana na swali la Mheshimiwa Ole- Sendeka kuhusu fedha za *ELIPS*. Tulitafuta fedha za *BADEA* na *OFID* kwa ajili ya kujenga mradi wa Orkesmet na ule mradi wa Mwanga. Fedha hizo zimepatikana na Serikali imetiliana sahihi na wafadhili hao kwa ajili ya utoaji wa fedha hizo. Wakati tunafanya hivyo, suala hili limechukua muda mrefu tangu mwaka 2006 na kwa hiyo, kulikuwa na haki kabisa kwa Serikali kuanza kutafuta njia mbadala za kupata fedha ya mradi huo, na wakati huo Serikali pamoja na Mheshimiwa Mbunge nami napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa kufanya kazi kubwa sana ya kushirikiana na kumleta huyo mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tuliyofikia sasa mwekezaji huo hatutamtumia kwenye mradi wa Orkesmet. Lakini nakubaliana sana na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba ni vizuri tuendelee kuongea na huyo mwekezaji ili ikiwezekana aweze kujenga mradi wa maji unaokwenda Mererani na maeneo yale ya *Kilimanjaro International Airport* na Wilaya ya Meru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Machali aliuliza swali hapa kuhusu mradi unaotekelezwa kule Kasulu kwenye kijiji kimoja. Nitakachoweza kufanya, nitatuma wataalamu waende kule waukague ule mradi ili watupe *report* ya utekelezaji wa yule Mkandarasi na kama amezembea, sitasita kumwondoa na wafanyakazi kama wamezembea, wanafanya kazi kwa mazoea na wenyewe tutashirikiana na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo yuko hapa anasikia. Kama kuna Mhandisi ambaye hatekelezi wajibu wake na Waziri wa TAMISEMI yuko hapa tutamshughulikia haraka iwezekanavyo. Kufanya kazi kwa mazoea katika hali hii ya utekelezaji wa miradi ya maji hakutavumilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi juu ya mradi wa maji kutoka Shinyanga kwenda Kishapu. Ni kweli mradi huu umeshasanifiwa na uko

tayari kwa utekelezaji. Mradi huu ulikuwa utekelezwe pamoja na miradi ya Tinde, Nzega, Tabora na miradi ile bado inasanifiwa. Mradi huu umekamilika na ninachoweza kusema ni kwamba tutaendelea kuutafutia fedha na *inshalah* tutapata fedha ili mradi huo uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna swali hili la uwiano wa Mijini na Vijijini. Ni kweli kwamba kwa muda mrefu kumekuwa na uwekezaji mkubwa katika Miji na hivi sasa kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu hapa kwamba kuna Miji mingi ambayo miradi imekamilika, lakini pia ipo Miji mingi ambayo miradi inaendelea kutekelezwa. Kwa mfano, tunatekeleza Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora mpaka Kigoma; tunatekeleza mradi Bukoba, Musoma na tunatekeleza miradi ya Lindi, Mtwara, Babati na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupanga ni kuchagua. Sasa eneo hilo nadhani tumefika mahali ambapo tunaelekea kulikamilisha na huku Mijini uwiano wa upatikanaji wa maji siyo kwa watu wanaokaa, lakini pia na viwanda, hospitali zetu na huduma nyingine muhimu ambazo na zenyewe ni lazima zipatiwe maji na ni muhimu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tumefikia mahali ambapo baada ya uwekezaji unaoendelea kukamilika, upatikanaji wa maji Mijini utafikia 95% kwa Miji mikubwa, lakini bado tutakuwa na Miji Mikuu ya Wilaya, tutakuwa na Miji midogo ambayo kwa ukweli na yenyewe ni sawasawa na Vijiji. Kwa hiyo, uwekezaji katika maeneo haya pamoja na Vijiji ndiyo yatakuwa makubwa katika uwekezaji wa maji na Serikali imeamua katika *big results now,* kwamba uwekezaji katika maji au kipaumbele katika uwekezaji wa maji kitakuwa Maji Vijijini. Kwa hiyo, tuimbeni wote “Maji Vijijini,” tupelekeni maji Vijijini, tuungane mkono ili tupitishe bajeti hii ili tupeleke maji Vijijini. Huko ndiko tunakokwenda. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Lekule Laizer; katika marekebisho haya ambayo leo ndiyo tunaongea juu ya marekebisho haya kwa mara ya kwanza,

yatakapokuwa yametekelezwa, Wilaya ya Longido itakuwa imeangaliwa kwa undani sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Lekule Laizer avute subira tu, kazi ya ukokotoaji wa miradi ambayo itatekelezwa ikikamilika, kila Mbunge atapewa nakala hiyo ili ajue miradi ambayo itakuwa inatekelezwa katika Wilaya yake ni mradi gani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, unataka nyongeza ya maelezo? Mheshimiwa Mnyika, kwanza samahani kidogo!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwongezea tu Mheshimiwa Mnyika, kuomba ile Shilingi yake abaki nayo Mfukoni.

Pamoja na bajeti ya Maji iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri leo kutoka kwenye Wizara, nilitaka kumkumbusha Mheshimiwa Mnyika kwamba akichukua randama ya TAMISEMI, kuna fedha zimetengwa za usimamizi wa maji zaidi ya Shilingi bilioni 12. Lakini ukichukua kitabu hiki cha maendeleo Mkoa kwa Mkoa, kuna fedha nyingi za maji tayari ambazo zimeshapitishwa kupitia Mkondo wa TAMISEMI, kwenda kwenye Mikoa.

Kwa hiyo, akijumlisha hizi; bahati mbaya sikuwa na nafasi ya kujumlisha, lakini ukijumlisha hizi Shilingi bilioni 12 na hizi zilizopo kwenye miradi Mkoa kwa Mkoa na hizi zinazisi zile ambazo mlifikiria kwamba ndiyo kiwe kiwango cha juu.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na ufafanuzi uliotolewa na nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tulijadajili hili jambo.

MWENYEKITI: Sema naondoa Shilingi tukuelewe!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Naondoa Shilingi!

MWENYEKITI: Haya!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuna eneo moja ambalo Mheshimiwa Waziri hakujibu kabisa. Kwenye ukurasa wa 88 wa hotuba yake inaeleza wazi, mwaka 2012 Bunge hili lilipitisha Shilingi bilioni 140 kwa ajili ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tunafikia mwezi Machi, 2013 ikiwa imebaki miezi mitatu tu kuelekea mwezi Juni ambapo ndiyo mwisho wa utekelezaji wa Serikali, fedha zilizotolewa ni Shilingi bilioni 29 peke yake, sawasawa na asilimia 20.7 peke yake. Yaani ni chini ya robo ya fedha, wakati mpaka kipindi hiki zilipaswa ziwe zimetolewa angalau asilimia 75 ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Hata kama tukiwa na matumaini sana ya kiwango cha fedha kilichoongezwa, kama fedha hazitatolewa kwenda kwenye miradi ya maji, hata ziongezwe kiasi gani, bado miradi ya maji haitatekelezwa kwa sababu fedha zitakuwa hazijafika. Sasa hili eneo Mheshimiwa Waziri hajasema neno lolote kwamba, sasa kuna mkakati gani wa kuhakikisha fedha zinazotengwa na Bunge kwenye miradi ya maendeleo; ukienda kwenye vifungu vya posho, utakuta fedha zimetoka kwa asilimia 70, asilimia 90, lakini kwenye miradi ya maendeleo fedha zimetoka kwa asilimia 20.7. Hili ni jambo zito ambalo linahitaji mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye hili suala la nyongeza ya fedha, Mheshimiwa Waziri ni vizuri akarejea kwenye hotuba yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ukitaka tukusaidie kwenye Shilingi ni hoja. Kwa hiyo, uwe *precise*.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Shilingi moja hii kwa masuala niliyahoji, nilihoji kiwango cha fedha kilichoongezwa kwamba ni kiwango kinachofurahisha, lakini bado hakijakidhi mahitaji. Vilevile nikahoji kwamba hata hicho kidogo hakitatolewa kwa wakati, nataka *commitment* kama zile fedha zinakuwa *ringfenced* au unatumika mkakati gani?

Sasa kwenye hiki kiwango sisi tunazungumzia fedha za ndani. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 43, aya ya 94 ya hotuba yake kwenye *program* ya *Big Results Now* inasema kwamba ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya maji, fedha zinazohitajika ni Shilingi trilioni 1.45. Sasa Shilingi trillioni 1.45 kwa miaka michache iliyobaki, unaweza kujua ni kiwango gani cha fedha za ndani kinachohitajika kuweza kutimiza lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni muhimu Wabunge wakatafakari kwa sababu wanazungumzia Ilani ya CCM. Ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010 ilisema kwamba ifikapo mwaka 2010 asilimia 65 ya wananchi Vijijini watakuwa na maji, asilimia 90 ya wananchi Mijini watakuwa na maji. Mwaka 2010 umefika, Ilani haijatekelezwa, asilimia hazijafikiwa. Sasa kama safari hii hatutakuwa wakali kukubaliana kwa pamoja, tuone kweli hizi fedha zinatoka na kwa kiwango kinachostahili, ni wazi hata hiyo ilani ambayo mmerudia tena, yaani Ilani ya 2005 – 2010 mmerudia kwenye 2010 – 2015.

MWENYEKITI: Naomba uniambie mimi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Nashukuru. Nakwambia Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba Ilani imerudia tena malengo yale yale yaliyopaswa kutekelezwa mwaka 2010. Kwa hiyo, ninachokisema hapa ni kwamba kama hakuna *commitment,* naomba kutoa hoja kwamba jambo hili lijadiliwe ili Serikali iweke *commitment* kwamba, kweli hizi fedha zitatolewa na zitatolewa kwa wakati. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

MWENYEKITI: Eeh, sawa mnajadili. Waache wajadili kwanza, dakika tatu tatu. Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Akunaay, Mheshimiwa Nkumba na Mheshimiwa Mwijage.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja moja ya msingi kubwa sana iliyozungumzwa na Mheshimiwa Mnyika, nayo ni kiasi cha fedha kinachotolewa baada ya Bunge kupitisha bajeti. Kupanga bajeti na kupitisha kwenye Bunge ni jambo moja, lakini kutolewa kwa fedha nako ni jambo tofauti. *(Makofi)*

Hoja ya Mheshimiwa Mbunge ambayo nataka kuiunga mkono ni vipaumbele. Mwalimu alisema Kupanga ni Kuchagua. Yawezekana ukapitisha bajeti kubwa, lakini matumizi yakawa ni makubwa, zikajitokeza *disasters* mbalimbali na zikatumia fedha nyingi na pengine sekta nyingine zikawa zinakosa fedha. Lakini kama wote tunakubaliana kwamba maji ni uhai na kwamba bila maji hakuna uhai, na tunakubaliana kabisa kwamba ipo haja ya kuweka kipaumbele kwenye Sekta ya Maji, nataka tu kuiomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu, na Mheshimiwa Mnyika namshukuru sana kwa kusoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM japo amesoma kinyume nyume kidogo, kwamba katika mipango ya mwaka huu fedha nyingi katika kipindi cha bajeti ya mwaka uliokwisha imeelekezwa mno kwenye barabara na mitambo ya kukodi ya umeme. Safari hii elekezeni fedha nyingi kwenye maji na maji Vijijini.

Kwa hiyo, tunataka *commitment* ya Serikali katika hili na mimi naunga mkono pendekezo la kuhakikisha kwamba Serikali inatoa kauli ya kuhakikisha kwamba, Sekta ya Maji itapewa kipaumbele kuliko maeneo mengine ambayo ni ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Akunaay!

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwamba pamoja na kwamba bajeti ya awali ilikuwa ni Shilingi bilioni 365 na baada ya Wabunge

kulalamika kwamba fedha hiyo haitoshi, imeongezwa mpaka Shilingi bilioni mia tano na ushehe; hoja ni kwamba:-

Je, kuna uhakika gani kwamba fedha hizo zitafika au ni kuondoa tu kwamba hii bajeti ipite kama ilivyotolewa mfano kwamba iwapo mpaka mwaka huu mwezi wa Tatu, bajeti ya mwaka 2012 kwenye miradi imetekelezwa kwa asilimia chini ya 20? Je, bajeti hii ambayo imepita kwa ugumu kiasi hiki, tuna uhakika gani kwamba fedha hizi zitafika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ambayo iko mbele yetu ni kuhusu uhai wa maji na kila siku tumetamka hapa kwamba maji ni uhai. Je, kwa hali hii, kweli maji ni uhai? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Waziri!

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Maji ni uhai na hatuwezi kuukabidhi uhai wetu kwa mtu yeyote.

Nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika na kwa hoja hiyo napenda niipe ushauri Serikali yangu kwamba lile wazo letu la kuanzisha Mfuko wa Maji tulikazanie. Tutafute vyanzo, kama ni njia gani tutaweza kutoza tozo zozote, tuwe na uhakika kwamba fedha itapatikana. Hatuwezi kuliacha suala la maji. *(Makofi)*

Pia niishauri Serikali yangu kwamba tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu, bomba la gesi lifike Dar es Salaam. Likishafika, ile *saving* ya fedha tunayotumia kwenye mafuta, trilioni karibu 1.6 tutakapokuwa tumefikia hapo mwaka kesho mwezi Mei basi hiyo fedha yote tuiweke kwenye maji. Wasiwasi wa Mheshimiwa Mnyika kwamba kipindi kimebaki kifupi, tutakwenda kwa *speed* kali na tutaweza kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri achukue ushauri wangu.

MHE. JUMA S. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika, niliomba nifanye marekebisho yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunawasilisha taarifa ya Kamati hapa Bungeni, takwimu alizozisema Mheshimiwa Mnyika zilikuwa zinahusiana na vikao vilivyokuwa vinafanyika Dar es Salaam. Lakini tulipokuwa hapa, Serikali kwa maana ya Wizara ilikwishaingiza Shilingi za ziada nyingine, na kwa sasa Shilingi bilioni 104 ambazo ni sawa na asilimia karibu 84, sisi kwenye Kamati tumekwisharidhika kwamba zimeishakwenda katika kutekeleza shughuli hizi. Kwa hiyo, siyo ile asilimia 29. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema tu kwamba pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Mnyika, kupanga ni kuchagua kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu; lakini nilikuwa naomba sana mambo mengine yote yanahitaji mfuko mmoja tu wa Serikali na yote ni muhimu. Tunazo barabara zetu Mijini na Vijijini, umeme Vijijini, Sekta ya Afya, Elimu; haya yote yanahitaji bajeti yetu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, lazima tuanze. Yale maombi ambayo yaliletwa na Kamati ya Shilingi bilioni 184.5 ambayo Serikali imeyaridhia ni vizuri tukayaunga mkono, tukaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imesikia kilio cha utofauti wa maji Vijijini na Mijini.

Maji Mijini kwa fedha hizi tunazoongeza, tumeongeza Shilingi bilioni 12.1 peke yake. Lakini kwenye miradi ya Vijijini kwa fedha hizi zinazoongezwa, tumeongeza Shilingi bilioni 161.7. Kwa hiyo, utaona jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba, sasa Sekta ya Maji maeneo ya Vijijini inapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kukubaliana na Mheshimiwa Mnyika, nilikuwa naomba tu hizi

taarifa nazo zizingatiwe katika kuhakikisha kwamba Serikali inafuatilia kikamilifu maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge wote hapa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lile alilosema Mheshimiwa Nkumba ndilo hilo nililotaka kusema kwamba, Serikali imeishatoa fedha ambayo ni juu zaidi kuliko kiwango ambacho Mheshimiwa Mnyika anasema. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba mradi wa *Big Results Now* utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu. Kwa kiwango cha bajeti ya maendeleo kilichotengwa sasa, ukizidisha mara tatu unapata Shilingi trilioni 1.659. Kwa hiyo, tuko kabisa njiani na kwenye kiwango cha utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuunge mkono Mheshimiwa Said Nkumba na Waziri wa Fedha, kwamba tangu mwezi Februari na mpaka *early March*, Serikali kuanzia wakati ule mpaka mwisho wa mwezi Machi imepeleka Shilingi bilioni 75 kwa Wizara ya Maji kwa fedha za ndani na Shilingi bilioni 80 fedha za nje.

Kwa hiyo, katika utoaji wa fedha, Serikali imeendelea kutoa kama ambavyo imeahidi. Nategemea kwamba mpaka tufike mwisho wa mwaka wa fedha tutakuwa tumepata fedha zote za maendeleo. Kwa vyovyote vile, fedha zote zinazohitajika kwa miradi ya maji Vijijini, zimeshatolewa kwa maana hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baada ya Mfuko wa Maji kuanzishwa, ni vizuri tuanze kufikiria vyanzo vya fedha za uhakika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Namuunga mkono Mheshimiwa Mwijage na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wanapendekeza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekaza kwamba, hoja ya Mheshimiwa Mnyika sasa ikataliwe kwa sababu kila hatua iliyotaka kuchukuliwa, imechukuliwa na hakuna sababu tena ya kwenda katika hatua ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu kidogo kwa sababu kitabu hiki tumepewa mwezi Aprili wiki iliyopita, Jumatano na ni cha Mheshimiwa Waziri, na ameandika yeye mwenyewe kwenye aya ya 188 ya hotuba yake kwamba: "Ilipofika mwezi Machi, mwaka 2013 fedha ambazo zilikuwa zimetolewa ni Shilingi bilioni 29 peke yake kati ya Shilingi bilioni 140, sawasawa na asilimia 20.7."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo yaliyotolewa hapa, napata shida kidogo kuwa na hakika kwamba hizo fedha zimetolewa kwa wakati. Lakini nilichokiomba zaidi ni kwamba, tupate *commitment* ya Serikali kuwa hizi fedha zilizoongezwa sasa hivi, kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba zinatoka kwa wakati. Kuna baadhi ya wakati Bunge linaamua ku-*ringfence* baadhi ya fedha ili kuhakikisha kweli hizi fedha hazitatumika kwingine na zitatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hii ni hoja ya kawaida sana, haina sababu yoyote ya Mheshimiwa Waziri kuikataa. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wenzangu wapige kura kuikubali hii hoja.

MWENYEKITI: Aah, ngoja kwanza. Huo mkakati kwa mfano wafanyaje? Hebu eleza vizuri hapo. Ili kukuhakikishia kabisa, wafanyaje?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hizi fedha ziwe *ringfenced* na kuwekewa kipaumbele cha kwanza katika fedha za maendeleo.

MWENYEKITI: Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba Serikali inapoidhinishiwa fedha na Waheshimiwa Wabunge, inakuwa imepata mamlaka ya kuzitumia katika maeneo ambayo imeomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, nachukua nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, fedha mnazoidhinisha zitatumika kule ambako mmeelekeza na kwa kiwango ambacho mmeidhinisha.

MWENYEKITI: Haya, nitawahoji. Hakuna shida, ninawahoji tu, hakuna tatizo. Wanaosema kwamba hizi...

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa ngoja kwanza tumalize.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Naomba nitoe taarifa kwa Waziri wa Fedha.

MWENYEKITI: Unajua, ngoja nisimame, wewe ukae. Ndiyo maana nakuuliza, ku-*ringfence* maana yake nini? Kwa hiyo, haina tatizo, hii ni *commitment* ya Serikali. Kwa hiyo, suala kwamba mnaungana na Mheshimiwa Mnyika, ndivyo wanavyofanya Serikali.

Sasa wanaosema kwamba Serikali ijihakikishie kwamba, hizi fedha zinatumika, waseme ndiyo.

WABUNGE: Ndiyooooooo!

MWENYEKITI: Wanaosema siyo lazima kujihakikishia, waseme siyo. *(Kicheko/Makofi)*

Eeh, ninachojaribu kusema ni kwamba, anachosema Mheshimiwa Mnyika ndiyo maana ya bajeti. Asubuhi tumesema hapa na Waziri wa Fedha hawezi kutueleza hivi hivi, alete maandiko. Ameleta! Hili ni zoezi mojawapo ya *rinfencing*. Tumekuja hapa tumesema aah, tuone kwenye vitabu, tumefanya. Kwa hiyo, anachokisema Mheshimiwa

Mnyika ni kuongeza kwamba, jamani tuhakikishe fedha zinatolewa. Ndiyo hivyo! Kwa hiyo, mimi nadhani hakuna nongwa.

Kwa hiyo, wanaosema hoja ya Mheshimiwa Mnyika ikubalike waseme ndiyo.

WABUNGE: Ndiyooooo.

MWENYEKITI: Wanaosema isikubalike.

WABUNGE: Siyooo.

MWENYEKITI: Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .....Tsh.1,383,129,000/=

MWENYEKITI: Naomba tukiwa kwenye *stage* hii, mjaribu kutulia ili niwaone wanaosimama. Mtaangalia kutakuwa na maandiko tofauti tofauti hapo na kuangalia *addendum*. Haya, Mheshimiwa Gekul!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika hicho kifungu cha 1002 na katika marekebisho tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri, naomba nipate ufafanuzi kuhusu fedha ambazo zimeongezwa Shilingi milioni 200. Katika fungu hili kwa ujumla zimeongezwa Sh. 10,700,000,000/= na kwa *specific* kifungu hiki cha 1002 ni Shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zinaonekana zimewekwa tu, lakini haijaoneshwa ni kasma gani ndogo ambayo fedha hizi zinakwenda. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya kina, pamoja na kwamba ametuletea

marekebisho au ongezeko la fedha, lakini hata sasa hizi fedha wameziweka tu katika upande wa *OC,* haioneshi ni za usafiri, *training* au kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu hayataridhisha kwa mujibu wa Kanuni ya 102 (2) nitoe hoja ya kuondoa Shilingi kwa sababu hizi fedha Shilingi bilioni 10 ni nyingi. Nishauri Wabunge wenzangu tuziondoe fedha hizi tuzipeleke upande wa maendeleo badala ya kuziweka huku kwenye *OC*.

MWENYEKITI: Naomba usikilize kwanza. Wewe uliza ni za kazi gani? Halafu utajibiwa huwezi kenda mbele wakati nyuma hujafika. Mheshimiwa Waziri, umeliewa swali lake? Ni ile *OC* kwa ajili ya umeme. Unahitaji arudie? Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa fedha hizi Shilingi bilioni 10 unaoneshwa kwenye jedwali la nyongeza ukurasa kwanza hadi ukurasa wa pili na Idara ambazo zinaongezewa hizo fedha zimetajwa pale ikiwemo Idara ya Utawala na Raslimali za Watu, Kitengo cha Fedha na Uhasibu, Idara ya Sera na Mipango, Kitengo cha Usimamizi na Ununuzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, halafu kuna Idara ya Usimamizi wa Raslimali za Maji, Idara ya Huduma za Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini, Idara ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na jumla yake inaonesha pale kwamba ni Shilingi bilioni 10.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri hakunijibu. Labda nirudie tu kwamba, nimeona wamepanga katika hizo Idara; Idara ya Sera na nyingine ambazo amezitaja na jumla wakapata Sh. 10,700,000,000/= lakini katika hizo Idara kuna *specific* au *sub votes*. Kuna *training*, *allowances*, mafuta na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupachika tu milioni 200 katika Idara, haituoneshi sisi Wabunge kwamba, hizi fedha sasa zimeongezeka katika *Sub-vote* ipi. Ndiyo nikashauri kwamba, kwa sababu hizi fedha zinaonekana zina-*hang* tuzipeleke kwenye miradi ya maendeleo kuliko kupoteza hizi bilioni 10,700,000,000/= wakati tu zimewekwa kwenye Idara, hazijulikani ni fedha za *training* au za mafuta au za kitu gani.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimemwelewa Mheshimiwa Gekul. Fedha hizi kwa ujumla zitatumika si kwa ajili ya hiki kifungu pekee, lakini hizi shilingi bilioni 10 zitatumika kwa ajili ya kulipia umeme katika miradi ile mikubwa ya Taifa ambayo ni kama ule Mradi wa Lake Victoria-Shinyanga, Mradi wa Wanging'ombe, Mradi wa Maswa, Mradi wa Handeni na Miji ile ambayo ipo kwenye *grade* b au *grade* c ambayo umeme wake unalipwa na Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 5.3 zinahitajika kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haki za ajira au zinaitwa stahili za ajira za wafanyakazi wa Wizara ya Maji ni shilingi bilioni 2.8. Hizi ni stahili zao kwa mfano, kama wamepandishwa daraja na wamelipwa mshahara bila kulipwa *arrears* tangu siku ya kupandishwa au kila baada ya mwaka mmoja wanapokwenda likizo wanalipiwa gharama za kwenda likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na gharama za kuendesha Chuo cha Maji ambazo kila mwaka ni shilingi bilioni 0.9 na fedha za kulipia mikataba ya Kimataifa ambayo Wizara ya Maji inashirikiana kwa mfano, kama *Nile Basin Initiative*, kama *Lake Victoria Equatorial Lakes* na dhamana zingine za Kimataifa ambazo Serikali imeingia mikataba. Halafu pango la nyumba hapa Dodoma, gharama za kuendeshea ofisi na gharama za usimamizi wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutatenga fedha ya miradi peke yake, bila kuweza kwenda na kuhakikisha kwamba inatekeleza, haiwezekani tukawa na uhakika kwamba kweli utekelezaji utakwenda kama tunavyofikiria.

MWENYEKITI: Naomba usome *Addendum* hii.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Planning*... ... ... Sh. 2,320,332,000/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizia kifungu hicho kasma 270600 *Current Grants to Non-Financial Public Agencies* ambacho mwaka wa fedha uliopita kilikuwa billioni 1.9 na mwaka huu kimeshuka mpaka shilingi bilioni 1.5. Hii ni kasma inayohusu kuiwezesha Taasisi ya Uendelezaji Maji kwa maana ya Chuo cha Maji pale Rwegarulila na kuwezesha wakala wa uchimbaji visima *DDCA* kwa ajili ya uchimbaji wa Visima.

Sasa ningependa kupata ufafanuzi kwa sababu kiwango kinaonesha hapa kimeshuka, lakini kwenye *addendum* tuliyopewa kuna nyongeza ya kifungu cha 1003, Idara ya Sera na Mipango kwa ujumla wake imeongezewa shilingi bilioni 1.2. Naomba kupata ufafanuzi iwapo hizi bilioni 1.2 zimeelekezwa kwenye matumizi ya hicho Chuo cha Maji pamoja na Wakala wa kwenda kuchimba visima au zimeelekezwa kwenye hivi vifungu vingine vya posho na matumizi mengine. Kwa hiyo, nahitaji *commitment* kwamba, zielekezwe pale ambapo zitakwenda kweli kusaidia huduma ya maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kifungu hiki kwa mwaka 2012/2013, kilitumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za *DDCA* yaani Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa pamoja na Chuo cha Maji. Lakini mwaka huu *DDCA* wana kasma yake, kwa hiyo, hizi fedha zilikuwa ni kwa ajili Chuo cha Maji na zilikuwa zimepungua kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Sasa baada ya kuongezewa hizo fedha zingine ndiyo maana zimeonekana kwenye hii sehemu ya Mipango, *Policy and Planning* kwamba kuna fedha za nyongeza ambazo zitakuja tena kwenye shughuli hizi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – *Government Communication Unit* ... ... Sh. 160,010,944/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ... ... Sh. 224,033,008/=

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naulizia *item* 221100, *Travel out of country* ndani ya miaka miwili haikuwekewa fedha. Lakini nashangaa kwamba safari hii imeweka milioni 1.5. Nataka kujua hii safari ya nje ya milioni 1.5 ni safari gani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, safari zote za nje zimekuwa *centralized* zipo kwenye kasma ya utawala. Hii milioni moja nadhani ni vitu vidogo vidogo vya maandalizi kwenye hiyo Idara. Lakini sehemu kubwa ya fedha zipo kwenye kasma ya Utawala ambayo tayari tumeshaipitisha.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*... ... ... Sh. 1,215,078,856/=

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye *sub-vote* 1006 *Procurement Management Unit item* 220800 *Training domestic*. Kwenye *column* hiyo ya mwaka huu wa fedha hawajaweka *figure* ila imeandika *Mate of the* na ukijaribu ku-*totalize* hizo unakuta kwamba unapata jumla pamoja na nyongeza ya sasa ni shilingi bilioni 1,211,078,856 inakuwa na pungufu na *total* aliyo-*indicate* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua kwenye hiyo *row* ya *Training domestic*, hiyo *mate of the* ni *amount* gani ipo hapo. Kwa sababu ukijumlisha pia hiyo *figure* iliyotajwa kama jumla yake siyo sahihi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *typing error* hapo ni milioni nne.

MWENYEKITI: Wapi, kwenye *mate of the*. Tumia *microphone*.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni milioni nne pale palipoandikwa *mate of the*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 – *Management Information System* ... ...Sh. 209,762,043/=

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye sub-vote 1007 sub- item 221000 *Travel in country* ukisoma kwenye hiyo *row* kuna maneno na *figures* zimetolewa, inawezekana na *typing error*. Lakini kuna *figure* ya 22,986,893, lakini pia nilivyojaribu kujumlisha zote na hiyo milioni 22, bado nilikuta kwamba *figure* ambayo wameitoa ya mwisho ni tofauti. Ukijumlisha hapo pote unapata 22,298,336. Sasa utaona kwamba, figure iliyowekwa hapo ni pungufu na *figure* halisia ukijumlisha hizo *items* zote.

MWENYEKITI: Mmeiona hiyo. Umekiona kifungu anachosema *travel in country,* kuna maneno halafu na hesabu ndogo pale. Sasa *according to her* anasema hii hesabu ni ipi mbona huku kwenye *total* haifiki. *Sub-vote* 1007, lakini *item* 221000 pale kuna maneno maneno tu, *Travel in country*.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejumlisha sana, hii *discrepancies* sijaiona.

MWENYEKITI: Hebu soma vizuri. Kuna maneno *ent And Pla* 22,986,893, mmeiona lakini.

NAIBU WAZIRI MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumlisha *total* inafika kwa sababu kuna 89, ukija 22, ukija 50, ukija 30 inafika kwenye hiyo 200.

MWENYEKITI: 209?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Ndiyo 209.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 – *Internal Audit Unit*... ... ... Sh. 598,310,812/=

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipatiwe ufafanuzi kwenye kasma ndogo ya *other operating expenses,* zimeongezeka kwa asilimia...

MWENYEKITI: Hebu taja *item number.*

MHE. PAULINE P. GEKUL: 229900. Zimeongezeka kutoka 21,150,000 hadi 60,000,000, naomba nipate ufafanuzi kwa nini fedha hizo zimeongezeka kwa asilimia hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha *other operating expenses* ni kifungu kinachoshughulikia shughuli kama za mazishi na shughuli za ushauri mbalimbali. Sasa mwaka uliopita kulikuwa na madeni, kwa hiyo kimeongezeka ili kiweza kulipa hayo madeni.

MHE. CHARLES P. J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu kizima, *concern* yangu ni kiasi cha pesa nataka kujua kama *Audit* imezingatia ongezeko la pesa. Kwa sababu *concern* yangu ni kwamba, hawa watu wa *Audit* wata-*cover* kazi ambazo tuna mashaka nazo zilizopo kwenye Halmashauri zetu.

MWENYEKITI: Tafadhali, nenda kwenye *item* halafu tutakuelewa vizuri zaidi.

MHE. CHARLES P. J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuongoza twende 410700, kwa sababu kwenye *feasibility studies* ndiyo mambo yanaharibikia hapo, ime-*consider* miradi mipya ambayo wataiongeza.

MWENYEKITI: Mmeiona hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Hii ni ya kuandaa miradi mbalimbali, makabrasha, *documents* mbalimbali za Idara. Kwa vyovyote vile fedha zilizoongezeka zitaongezeka kwenye kifungu hiki kwa sababu kazi zitakuwa zimeongezeka.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - *Water Resources Assessment and Exploration*... ... ...Sh. 5,907,104,956/=
Kif. 2002 - *Central Stores*... ... ...Sh. 199,391,000/=
Kif. 2003 – *Water Laboratory* ... ... .Sh. 2,041,429,048/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – *Urban Water Supply and Sewerage* ... ... Sh. 5,650,567,000/=

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Sub-vote* 3001, kifungu kidogo cha 229900 *ion Department expenses* yaani miaka yote iliyopita, kwa mfano, mwaka wa mwanzo kabisa ule ilikuwa milioni 1.9, unaofuata milioni tano, lakini mwaka huu 61,508,000, kwa nini tofauti imepanda namna hiyo, kuna nini hapo?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezewa fedha katika nyongeza mpya. Kabla kilikuwa na shilingi bilioni 1.6 kimeongezewa bilioni nne na

sasa kimekuwa bilioni 5. 6. Lakini ukiangalia *trend* ya kifungu hiki utakuta ilikuwa inashuka kutoka bilioni 2.7 mwaka wa fedha unaokwisha kwenda bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa ambalo lilikuwa linatengewa fedha nyingi katika kifungu hiki ni *basic salaries and Pensionable Posts* ambapo imeshuka kutoka bilioni 2.4 mpaka bilioni 1.2. Sasa nyongeza hii na hii ni Idara ya huduma ya maji safi na uondoaji wa maji taka Mijini. Nyongeza hii ya bilioni nne inakwenda wapi, wanaajiri watu wapya, wanastaafu watu wapya na kama iliwekwa tu bila kuangalia hivyo, kwa nini sasa fedha zote hizi zisiende kuongezwa kwenye maji vijijini ili ku-*boost* bajeti ile ya maji vijijini?

Swali hapa ni zile ulizouliza kwanza basi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu...

MWENYEKITI: Bado tuna Mheshimiwa Mbunge mmoja. Mheshimiwa Felister Bura samahani!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *sub-vote* hiyo hiyo 3001, *item* namba 220200, *Utilities, Supplies and services* mwaka huu wa fedha walitengewa milioni 60, lakini mwaka ujao wa fedha kuna *zero zero*. Naomba Maelezo.

MWENYEKITI: Nina wasiwasi ni typing *errors* au *something*. Waheshimiwa Mawaziri mnaweza kuanza kujibu wa kwanza mpaka wa tatu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *utilities* inachukuliwa na sehemu kubwa kwenye fungu la utawala kwa ajili ya kulipa gharama za simu, umeme na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye hii kasma ya 229900 kwamba kwa nini zimeongezeka kutoka milioni tano mpaka milioni 61, *Department expenses* kama

nilivyoainisha ni kwamba, kwenye Idara kunakuwa na shughuli mbalimbali ambazo hizo *services* huwa wanazipata wakati mwingine bila kulipa. Kwa hiyo, kuna madeni na ndiyo hiyo wameongeza ili waweze kulipa hayo madeni kwa mwaka huu.

MWENYEKITI: Lile la Mheshimiwa Zitto, hela zimesambazwa wapi?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimjibu Kabwe Zubeir Zitto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tutaanzisha Ofisi za Kanda, kwa hiyo, tutaajiri wafanyakazi wapya ili kuhakikisha kwamba usimamizi kule kwenye Wilaya unakuja haraka na Wilaya ambazo hazina Wahandisi zinapata msaada wa kuandaa miradi haraka ili iweze kutekelezwa kama ambavyo tumepanga, ndiyo maana kasma hii imeongezewa fedha.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 – *Rural Water Supply* ... ... .Sh. 4,012,567,332/=

MWENYEKITI: Lazima fedha zisomwe kwanza ndiyo mnasimama, hata mkisimama kabla ya hapo *no way.* Mheshimiwa Riziki!

MHE. RIZIKI OMAR JUMA Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kidogo kwenye kifungu kidogo cha 229900, *other operating expenses,* mwaka uliopita walikuwa wametengewa 2,500,000. Safari hii ongezeko kubwa sana milioni 34,750,000 naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Naomba muwe mna-*note*. Mheshimiwa Paresso!

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante limeshaulizwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, limeshaulizwa.

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo cha 210100 kwenye *Basic Salaries and Pensionable Posts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitafute ufafanuzi kwenye kifungu hiki kwa sababu kinahusiana kabisa na suala la *Rural Water Supply* na kilio kikubwa cha Wabunge ni Maji Vijijini.

MWENYEKITI: Ahaa! Mheshimiwa Lugola hii inahusiana na *Basic Salaries* and *Pensionable Posts,* basi. Kwa hiyo, huwezi kuuliza chochote kingine zaidi ya hapo, tafadhali. Huku tumeondoka kwenye mshahara wa Waziri, kwa hiyo, huwezi kuuliza tu kwa sababu hiyo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kile kifungu 410700, *Feasibility Studies Project Preparation and Design.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ndio linahusika na *Rural Water Supply* usambazaji wa Maji Vijijini na kifungu hicho kidogo ndicho chenye wataalam wetu ambao wanatusaidia kusimamia upembuzi yakinifu na maandalizi ya miradi yote ya Maji Vijijini. Kwenye marekebisho hapa tunaona kwamba, Kurugenzi hii imeongezewa karibu shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kitu kimoja, katika kifungu hiki, fedha iliyotengwa ni sh. 15,000,000/= tu kwa hao wataalam ambao watakwenda kutayarisha hiyo mipango yote ya miradi ya Maji Vijijini. Sasa fedha hii Mheshimiwa Waziri naomba akubaliane na mimi, kwenye fungu hilo dogo kwa fedha hii nyingi tuliyoiongeza iende na eneo hilo ili kuondoa matatizo ya ucheleweshaji ya mipango

ya miradi ya Maji Vijijini kama yanayovikuta vijiji vyote vikiwemo vijiji vyangu kule vya Igawisenga, Maweso na kwingineko.

MWENYEKITI: Hapana swali lenyewe unataka kuuliza hiki kifungu kimeongezewa, sio tena wewe useme, maana yake laah!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu limeulizwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, naona maswali ni mawili tu mtu wa kwanza na huyu wa mwisho.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu, *Other Operating Expenses*. Idara hii ya Maji Vijijini tulishaanza kuiangalia kwamba tuiwekee fedha kwa wingi ili kuweza kusimamia miradi vizuri na ndiyo maana hizi fedha zikawa zimeongezeka kwa sababu lazima kuiangalia miradi yote katika Halmashauri zote na kuona hatua zake ilizofikiwa. Kwa hizi fedha ambazo zitakuwa zimeongezeka nazo tutaongeza tena hapa ili tuweze kusimamia vizuri hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii *Feasibility Studies Project Preparations and Design,* kwanza nakubali kwamba, katika fedha zilizoongezwa kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama tutaongeza, lakini lengo kubwa la hapa vile vile ni kuandaa *documents* mbalimbali za miradi hii katika ngazi ya kiofisi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4002 - *Water Sector Program Coordination Unit*... ... ... Sh.196,758,000/=
Kif. 5001 - *Water Development and Management Inst.* ... ... Sh. 213,255,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 6001 - *Drilling and Dam Construction Agency*... ... ... Sh. 659,429,000/=

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu au kupata ufafanuzi. Katika kifungu hiki inaonesha kwamba, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya mishahara tu. Je, Kitengo hiki cha *Drilling and Dam* hakina kazi zozote inayofanya?

MWENYEKITI: Mmeona hiyo kitu?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni Kitengo kipya cha *DDCA,* ndio kimeanzishwa. Pamoja na fedha zilizoandikwa hapa chenyewe kinajiendesha kibiashara, kwa hiyo sehemu ya mapato yake yatatumika kwa kuendesha shughuli zake.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kif. 1001 – *Administration and Management*... ... ... Sh. 5,835,000,000/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru niko kwenye kifungu hicho cha 1001, kasma 3308, *Water Sector Institutional Strengthening.* Kifungu hiki mwaka huu wa fedha kinaombewa jumla ya shilingi bilioni 5.8, kati ya hizo shilingi bilioni 3.5 zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ufafanuzi kuhusu hizi fedha za ndani. Kwa sababu naelewa katika hizi shilingi bilioni 3.5 kati ya hizi fedha shilingi bilioni tatu ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la Wizara. Shilingi bilioni tatu kwa kule ambako wanachimba kisima kwa wastani wa shilingi milioni 30 kwa kisima kimoja ni sawa sawa na visima 100. Maana yake ni fedha za kuchimba visima vingi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi sababu ya Wizara katika mazingira kama haya ambapo tunakimbizana idadi ya vijiji, ni kwa nini hizi shilingi bilioni tatu za kujenga Ofisi ya Wizara zisingeondolewa kwenye kujenga Ofisi ya Wizara, yenyewe ikasubiri na fedha hizi zikapelekwa kwenye miradi ya maji na kwa maana ya kwenda kuchimba visima vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo ufafanuzi hautaniridhisha, kwa nini hasa tutenge shilingi bilioni tatu nitaomba nitumie kanuni ya 102 kutoa hoja ya kuweza kuhamisha hizi fedha kutoka kwenye kifungu hiki cha kujenga Ofisi ya Wizara na kuzielekeza kwenda kuchimba visima katika vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji haiko yenyewe, inafanya kazi na jamii pamoja na Serikali kwa ujumla. Pale Wizara ya Maji ilipo pamepimwa kwa ajili ya kujenga *flyover* ya ule mradi wa Mabasi ya Mwendo wa kasi na kuondoa msongamano wa magari pale Ubungo. Kwa hiyo, Wizara ya Maji lazima iondoke, iandae Ofisi mahali pengine na kulingana na fedha za kodi za pango zilivyo sasa, ni rahisi zaidi kwa Serikali *in the long time* itenge fedha ijenge mahali pengine pa kukaa, badala ya kwenda kupanga.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa kutumia kanuni 102 kuhamisha shilingi bilioni tatu kutoka kwenye kasma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ubungo na naelewa kwamba *flyover* inajengwa pale, naelewa kipande ambacho kitachukuliwa na *flyover* na naelewa kwamba Wizara ya Maji katika lile eneo ina ofisi mbalimbali. Kuna Ofisi za Wakala wa Visima, kuna Ofisi ya Chuo cha Maji, kuna ofisi za miradi na kuna ofisi za Wizara yenyewe. Naamini kabisa na kwa ujenzi wa mradi unavyoendelea tukiamua kuacha kutenga hizi shilingi bilioni 3 safari hii Ofisi ya Wizara ya Maji itaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tuna tatizo hapa la visima, tuna tatizo la maji na tuna tatizo la fedha kwa ajili ya wananchi kupata huduma ya maji ningeomba Wabunge wenzangu tukubaliane kwamba, nitoe hoja ili fedha hizi zihamishwe kutoka kwenye hiki kifungu cha 1001 zipelekwe kwenye kifungu cha 4001, *Rural Water Supply and Sanitation* kwenye mradi ule wa 3216, Mradi wa Kupanua na Kukarabati Miradi ya Maji Vijijini ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii imesambaa kwenye Halmashauri nyingi ikiwemo baadhi ya hiyo miradi iko ndani ya Jimbo la Ubungo lenyewe maeneo ya pembezoni kama ya Goba, Msumi, lakini kwenye kila Halmashauri hapa nchini kuna hilo tatizo la kwamba kuna miradi inaendelea lakini haijakamilika. Kwa hiyo, tuzichukue hizi shilingi bilioni tatu ziende kule, zikaongeze idadi ya vijiji ambavyo vitachimbiwa visima badala ya kwenda kujenga Ofisi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wabunge wa CCM wataunga mkono hili jambo kwa sababu Serikali hii ilisema...

MWENYEKITI: Achana na Wabunge.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kwa sababu Serikali hii ilisema itahamia Dodoma, sasa ni kwa nini kuendelea kujenga majengo ya Wizara Dar es Salaam wakati ambapo Serikali ilisema inahamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, kifungu hiki kihamishwe, kipelekwe kwenye kifungu nilichokisema.

MWENYEKITI: Na mwaka gani wajenge ofisi?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Waanze kujenga ofisi kuanzia mwaka wa fedha unaofuata.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ingekuwa rahisi kuelewa kwamba, kama itabidi tusianze

ujenzi sasa kila mwaka itabidi tulipe shilingi bilioni moja na nusu mpaka bilioni mbili kwa ajili ya malipo mpaka hapo tutakapokuwa na mahali pa kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

MWENYEKITI: Shilingi bilioni moja unalipa kwa nini?

WAZIRI WA MAJI: Kwa ajili ya pango.

MWENYEKITI: *Rent.*

WAZIRI WA MAJI: Ndiyo. Anachosema Mheshimiwa Mnyika kwamba yeye anajua, kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mnyika hatoki Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeletewa michoro, inalazimu tuondoke pale. Naomba Waheshimiwa Wabunge wakatae hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwa sababu...

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Hoja ya Mheshimiwa Mnyika ya kuondoa fedha za ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Maji na kupeleka katika Miradi ya Maji Vijijini ilikataliwa na Bunge)

MWENYEKITI: Jamani Maji Vijijini ni Maji Vijijini, lakini tukianza kutafuta Maji Vijijini wala tusile na tusinywe, basi tena Maji Vijijini litakuwa tatizo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Policy and Planning*... ... ... Sh. 20,114,100,000/=

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye kifungu kidogo cha 3436, kinachohusiana na *Monitoring and Coordination of WSDP*. Kuna shilingi bilioni 11,257,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi hapo kwa sababu juzi juzi hapa tumepitisha fedha za kufuatilia miradi ambapo tulisema tuanzishe *Presidential Delivery Bureau* kwenye Ofisi ya Rais. Sasa na hapa naona kuna shilingi bilioni nyingi sana ambazo zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji. Mimi niliomba fedha za maji...

MWENYEKITI: Ahaa! Unaharibu hoja yako. Kwa nini sasa na hapa zimetengwa, basi.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Sawa, kwa nini zimetengwa? Naomba maelezo vinginevyo hapa nitaondoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tunaomba mtusaidie kujibu hapo. Mheshimiwa Waziri, mna hoja mnatakiwa kujibu hapa.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya fedha zile za *PEMADU* sio kukagua miradi ya maji ina kazi zake zingine na zilielezwa wakati wa mjadala wa bajeti ile. Fedha hizi tunazotenga hapa ni kwa ajili ya ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya maji.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration*... ... ...Sh. 19,465,143,000/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory*... ... ... Sh. 4,483,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage*... ... ... Sh. 266,196,615,000/=

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho 3001 kuna mradi namba 3438, ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Zimetengwa hapa shilingi bilioni sita, jumla; shilingi

bilioni tatu za ndani na shilingi bilioni tatu za nje kwa ajili ujenzi huo. Napenda kufahamu kwa sababu ili Dar es Salaam iwe salama kwa maji na tupate maji ya kutosha ni lazima tuwe na bwawa hili la Kidunda na kuna mgogoro mkubwa sana wa wananchi wa Kidunda kuhusu fidia kabla mradi huu haujaanza. Nataka kufahamu wananchi wa Kidunda tayari wameshalipwa fidia ili mradi huu uweze kuanza?

MWENYEKITI: Mwambie watalipwa fidia. Naomba m-*note* maswali wanayoulizwa.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *sub-vote* 3001, *item* 3306, *Rehabilitation and Expansion of Urban Water Supply*. Nauliza, hizi fedha zilizotengwa hapa shilingi bilioni 86,656,615,000 ndio zitakazojenga maji pale Magu au ni fungu linalofuata la *sub-vote* 4001? Ahsante?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho, kasma 3437 *DWSSP*.

MWENYEKITI: Aliuliza mwenzio, hajajibiwa.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Ni kifungu tofauti aliuliza Kidunda.

MWENYEKITI: Ahaa 3437, kimeshaulizwa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitajielekeza kwenye *item* 3307, *Expansion of Urbarn Water Supply*. Naona kuna fedha nyingi tu ambazo zimetengwa, jambo ambalo ni zuri.

Nina swali moja kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri upo tayari kuweza kutueleza kwamba ni miji gani ambayo fedha hizi zimekusudiwa kwenda kufanya kazi?

MWENYEKITI: Nimempata anasema ni *UN Habitant*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya hizi fedha ambazo zimepatikana baada ya majadiliano kati ya Wabunge na Serikali inaonesha kwamba mradi Na. 3307 kukarabati na kupanua miradi ya Maji Mijini chini ya *WSDP* imeongezewa shilingi bilioni nane na kuipelekea kuwa na shilingi bilioni 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri anifafanulie kwamba, ni sawa kweli kuongeza hapa au fedha hii ingeweza kwenda kwenye *sub-vote* inayofuata ya vijijini, kwa sababu *already* mijini kuna fedha nyingi sana ambazo zimetengwa?

MWENYEKITI: Naomba ujibu swali la Mheshimiwa Machali, la Mheshimiwa Zitto ni hilo hilo katika *sub-vote* hiyo hiyo. Mheshimiwa Mnyika tayari umeshauliza. Mheshimiwa Waziri niliokuwa nao wamemalizika, naomba uwajibu Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Dkt. Limbu na Mheshimiwa Machali.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa nijibu swali la Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, Mbunge wa Kinondoni juu ya suala la bwawa la Kidunda. Tunaelewa kwamba, kuna mgogoro wa kulipa fidia kule Kidunda, lakini fedha kwa ajili ya kulipa wananchi wa Kidunda zimeshatengwa na zimepelekwa ili wananchi hao walipwe mwezi huu unaoanza kesho kutwa. Kwa hiyo, hiyo ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa pia kuna wananchi ambao watahitaji kulipwa wakati wa kujenga barabara inayounganisha bwawa la Kidunda na barabara kuu. Fedha hizi zimetengwa pia katika bajeti hii inayokuja ambayo tunapitisha na ndizo hizo ambazo zipo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Limbu ameuliza kwamba, fedha za Magu ziko wapi. Fedha za Magu ziko kwenye kasma 3306. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Limbu kwamba mradi wa Magu uko pamoja katika Mradi

wa Magu, Lamadi, Misungwi na Mwanza na kwa ajili ya kuondoa majitaka, mradi wa Mwanza, Bukoba na Musoma.

MWENYEKITI: Bado swali lingine la Mheshimiwa Machali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mheshimiwa Machali kwamba, ni miji gani, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba tutaiainisha na tutaleta kwa ajili ya Wabunge kujiridhisha kwamba ni miji gani itakayokuwa imepewa fedha kutoka kwenye kasma hii.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - *Rural Water Supply*... ... ... Sh. 237,149,362,000/=

SPIKA: Ngoja niwaandikeni, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Rajab na Mheshimiwa Muhagama.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kidogo nimuulize Waziri jambo moja la msingi sana. Katika mchango wangu wa msingi nilizungumzia...

SPIKA: Kiongozi wa Kambi ya Upinzani tuko kwenye Kamati ya Matumizi, kwa hiyo tunaomba uwe *very specific*.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Nakwenda katika *sub-vote* 4001, katika mradi 3216 kupanua na kukarabati miradi ya maji vijijini ambayo inaendelea. Pia katika michango yangu huko awali nilizungumzia maafa yanayopatikana Jimboni langu katika Vijiji vya Zarau na Mtakuja ambako maji yaliyoko sasa hivi yalipimwa na kujulikana yana sumu kwa maana ya *fluoride* na maafa haya yamesababisha watoto kulemaa, kwa kupinda miguu na mifupa. Je, katika hili fungu ambalo limeongezewa Mheshimiwa Waziri anatoa

commitment gani kwa wananchi wa Vijiji vya Mtakuja, Tindigani, Zarau na Sanya Station kuwa vijiji hivi vitakuwa katika fungu hili?

SPIKA: Hatuulizi swali namna hiyo. Tunauliza hizi hela katika kifungu ulichosema ni za kufanyia nini? Je, hayo mambo yako humo? Basi. Mheshimiwa John Cheyo!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, 3223 *Borehole* Drilling hii pia imeongezewa fedha karibu bilioni 24. Sasa nauliza kusambaza maji ya Bwawa la Nkoma ambalo limekaa zaidi ya miaka 13, je, baadhi ya fedha zitatatumika kutoka hapa?

MHE.ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Naomba nizungumzie *sub-vote* 4001, *item* 3341 inahusu ujenzi wa Same–Mwanga-Korogwe. Ninachoomba ni Waziri atoe ufafanuzi ambao kwa kweli nitauelewa kwamba, ujenzi wa Same- Mwanga – Korogwe kwa awamu kwa mara ya kwanza alisema ni bilioni 56.1, fedha ambazo wachangiaji wake ni *OPEC* ambao wametoa *USD* milioni 12 na *BADEA USD* milioni 10 na Serikali 20,900,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi utolewe ambao utaeleweka kwa Wabunge kwamba hizi fedha za *OPEC* ziko wapi kwa sababu hazionekani kwenye hiki kitabu, zinazoonekana ni za *BADEA* ambazo ni 11,400,000 na bilioni 20,900,000,000 ya Serikali. Sasa hebu tuambieni mmeweka wapi hizo za *OPEC* na Mheshimiwa Waziri mwenyewe amezungumza hapa kuwa tayari mmesainiana na wenzetu wa *OPEC* kuhusu uchangiaji wa Dola milioni 12 ambayo ni kama bilioni kumi na tisa na *point*. Wakati wameshatangaza kwenye gazeti la tarehe 24 kwa ajili ya kufanya tenda.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, hiyo kengele umepigiwa wewe. Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa kifungu hiki tayari kilishatajwa, lakini nakwenda katika maeneo mengine.

SPIKA: Taja, tukusikie.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, 3223, nataka kujua fedha hizi zilizotengwa ni zile zile fedha ambazo itapewa ile *agency* mpya?

SPIKA: Naomba ukae, Kanuni hairuhusu hatujibu hicho. Mwingine ni nani, Mheshimiwa Kamili tayari, Mheshimiwa Mbowe tayari, Mheshimiwa Cheyo tayari. Sasa namwita Mheshimiwa Zitto kwanza.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma hiyo hiyo, kifungu 3280, Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira ambacho kimeongezewa shilingi bilioni 118, napenda Mheshimiwa Waziri anifafanulie katika fedha hizi ndiyo na fedha za Mradi wa Kijiji cha Mwandiga zimo?

MHE.MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ambalo niliuliza lilikuwa ni kifungu namba 3216 na tayari lilishaulizwa, kwa hiyo, ninazingatia Kanuni.

MHE.JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye ile *sub- vote* 3216 ambayo ni kwa fedha zilizoongezwa leo...

SPIKA: Limeshaulizwa hilo, Mheshimiwa Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu huu mradi wa Same - Mwanga – Korogwe. Kama tulivyosema kwenye maelezo yetu kwamba, mradi unagharimu dola milioni 56.1, zimetengwa bilioni 32 na Serikali yetu inatakiwa ichangie dola milioni 34. Sasa ule mradi umegawanywa katika loti tatu na hizo loti tatu ndizo zinazochukua hizo fedha bilioni 32 kwa kazi zinazoanza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutoa fedha zote, fedha zinatengwa kulingana na kazi zinazofanyika. Mradi umepangwa kujengwa kwa miezi 18, kwa hiyo, hata hizo zingine ambazo anasema zipo, zitaingizwa kwenye vifungu hapa kulingana na kazi ambazo zitakuwa zimepangwa kwa mwaka huo unaokuja.

SPIKA: Kuna lingine, Mheshimiwa Waziri wa Maji!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimjibu mtani wangu hapa anasema swali la msingi na mimi ninamjibu jibu la msingi, ni mtani wangu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza wakati namjibu Mheshimiwa Ole-Sendeka kuhusu azma yetu ya kuangalia kama eneo lile ambalo lina maji hayo mabaya linaweza kupatiwa maji kutoka Mlima Kilimanjaro au Mlima Meru kwa ajili ya maeneo yale ambayo tatizo hili la *fluoride* ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tumeanzisha Kituo cha Utafiti pale Ngurdoto na hivi sasa wana *test membrane* ambazo zina *filter fluoride* katika *molecule* zile ambazo zinapatikana eneo lile na inaelekea kuwa kazi hiyo inaonesha matumaini. Labda baada ya miezi miwili au mitatu, tunaweza kutoa matokeo ya kazi hiyo kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bwawa la Nkoma, lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vijiji ambavyo viko kwenye hiyo Miradi ya Vijiji vya Kutoa Matokeo ya Haraka sinavyo hapa, isipokuwa niseme jambo moja; kwanza vijiji vyote vilivyokuwa kwenye Miradi ya Vijiji Kumi vyote kama Mwandiga ipo *for sure* na yenyewe iko hapo na itatekelezwa. Utekelezaji huu utahusu pia vijiji vingine ambavyo vitagawiwa shilingi bilioni 53.3 kwa uwiano ambao ni wa kawaida unaofuatwa. Nashukuru sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya matumizi baada ya kujadili taarifa ya Makadirio na matumizi ya fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kukubali nyongeza iliyopendekezwa, hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Maji na wataalam wao, lakini na Waheshimiwa Wabunge wa *Budget Committee*, Kamati ya Sekta ya Maji na pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuelewa kwenu. Sasa mjue huu ndiyo mwanzo, lakini siyo kwamba fedha zilizoongezwa zimetoka nje ya bajeti ambayo tunayo, ni hiyo hiyo tuliyo nayo. Naomba Waheshimiwa Wabunge muelewe hivyo.

Pia muelewe kuwa tunapopita Wizara kwa Wizara, hii ni *provisional,* tutakapofika kwenye *Appropriation Bill* ndiyo tutakuwa na bajeti ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, nawaomba msije mkajenga hoja kuwa tunadai tu ndiyo maana sisi tulijaribu kuangalia namna ambavyo tunaweza kuishauri Serikali namna gani ambayo tunaweza kuongeza mapato.

Waheshimiwa Wabunge kazi hii hatujaifanya vizuri ya namna ya kuishauri Serikali kuongeza mapato, kwa sababu siku zote tutakuwa na haya, lakini ukweli ni kuwa kama mapato hayaongezeki tutakuwa na matatizo.

Kwa hiyo, niwashukuru sana kwa kazi mliyoifanya ni nzuri sana na nadhani tunakwenda vizuri.

Kwa kuwa muda uliopo hautoshi kwa Waziri kusoma hotuba yake kwa sababu anahitaji saa nzima na hapa haiwezi kutosha, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.50 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 30 Aprili, 2013, saa Tatu Asubuhi)